Mbinu za Kukabili Uathirikaji na Ustahimilivu wa Umaskini

Mwongozo kwa Lugha Nyepesi wa Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania mwaka 2002/03

Kamati ya Utafiti na Uchambuzi

Oktoba 2004

Mbinu za Kukabili Uathirikaji na Ustahimilivu wa Umaskini

Mwongozo kwa Lugha Nyepesi wa Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania mwaka 2002/03

Kamati ya Utafiti na Uchambuzi

Oktoba 2004

Yaliyomo

DIBAJI ..... **iii**

1. UTANGULIZI **1**
TzPPA ya mwaka 2002/3 ilihusu nini? 1
Nani walifanya utafiti, wapi na vipi? 1
Je, matokeo ya TzPPA yatatumikaje? 2
Kitabu hiki kinatueleza nini na kimepangwa vipi? 2

2. UMASKINI, USTAWI NA AINA ZA UATHIRIKIAJI **3**
2.1. Umaskini na Ustawi 3
2.2. Uathirikaji kwa Umaskini 3
2.3. Kitu gani kinawafanya baadhi ya watu kuathirika na umaskini zaidi kuliko wengine? 4
Sababu zinazoleta umaskini 4
Vipengele vinavyokwaza 6
Vikwazo 7
2.4. Mitego ya Umaskini 8

3. MAZINGIRA NA UATHIRIKAJI **9**
3.1. Mishtuko na Mifadhaiko inayohusiana na mazingira 9

4. MAREKEBISHO YA UCHUMI NA UATHIRIKAJI **16**
4.1. Kuondoa msaada wa Serikali katika masoko na uzalishaji 17
4.2. Mipango ya mikopo iliyotayarishwa vibaya 19
4.3. Nafasi chache za ajira 20
4.4. Kupungua kwa upataji wa rasilimali ikiwemo ardhi 20

5. UTAWALA NA UATHIRIKAJI **22**
5.1. Utozaji kodi 22
5.2. Huduma na uongozi duni 24
5.3. Usalama, sheria na utaratibu 24
5.4. Sera zisizofaa 25
5.5. Rushwa 27

6. AFYA, VVU/UKIMWI NA UATHIRIKAJI **29**
6.1. Kuwa na afya mbaya 30
6.2. Unyanyapazi na utengaji 32
6.3. VVU/UKIMWI 33

7. MZUNGUKO WA MAISHA NA UATHIRIKAJI **36**
7.1. Utotoni 36
7.2. Miaka ya kuzaa 37
7.3. Kuzeeka 40
7.4. Kifo 42

8. MILA NA DESTURI NA UATHIRIKAJI 44
8.1. Masuala yanayoathiri vikundi mahususi vya jamii 45
8.2. Mifumo ya mila na imani 49

9. MAHITIMISHO 53
9.1. Utangulizi 53
9.2. Sababu zinazoleta umaskini 54
9.3 Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko 54
Vipengele Vinavyozuia 55
Vikundi vilivyo hatarini zaidi 56
Hatua za kujiokoa 56
9.4. Athari za Upunguzaji Umaskini 57
Kupunguza mishtuko na mifadhaiko: Kukabili sababu zinazoleta umaskini 58
Kuimarisha uchaguzi wa mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko 58
Hatua za kujiokoa, Ulinzi wa Jamii 58

FAHARASA: Maana za maneno yaliyotumika katika kitabu hiki 60

Ramani ya Tanzania Bara inayoonyesha Sehemu ambamo Utafiti wa TzPPA ulifanyika 62

DIBAJI

Kijitabu hiki kimetoa mwongozo wa lugha nyepesi wa Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania (TzPPA) mwaka 2002/2003. Tathmini hii iliyoandaliwa na serikali ilikuwa na lengo la kupata ufahamu wa kina kuhusu vipengele mbalimbali vinavyowaingiza watu katika umaskini, namna wanavyoathirika na kustahimili. Uathirikaji ni matokeo ya mwingiliano wa mambo mengi yanayowaingiza watu katika umaskini ikilinganishwa na uwezo walio nao na unaofaa kukabiliana na matatizo mbalimbali. Tathmini ilishirikisha jamii katika kutafuta sababu zinazowafanya watu waathirike na umaskini badala ya kuangalia dalili za umaskini peke yake, kama vile ukosefu wa chakula na malazi.

Tathmini hii shirikishi kuhusu uathirikaji na ustahimilivu wa umaskini imegundua kuwa zipo sababu mbalimbali zikiwemo za kijamii, siasa, mila, uchumi, mazingira, umri, afya na utawala ambazo huwatumbukiza watu katika umaskini. Sababu hizo huwafanya watu wapate mishtuko na mifadhaiko ya maisha na kuwafanya wawe maskini ikilinganishwa na hali waliyokuwa nayo hapo awali. Tathmini inatoa wito wa kushughulikia uathirikaji na ustahimilivu wa umaskini kama mbinu mojawapo ya kufanikisha utekelezaji mkakati wa kupunguza umaskini.

Kufuatia kuandaliwa kwa kijitabu hiki katika lugha nyepesi, inatarajiwa kwamba watu wengi watapata ufahamu juu ya mbinu za kukabili uathirikaji na ustahimilivu wa umaskini. Aidha ufahamu utakapojengwa watu wengi wa ngazi zote watawezeshwa kushiriki kikamilifu katika kutekeleza, kusimamia na kutathmini Mkakati wa serikali wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA).

Tunawakaribisha wadau wote kusoma mwongozo huu wa lugha nyepesi wa TzPPA ya mwaka 2002/2003 ili kubuni mbinu mpya na bora zaidi za kuondoa umaskini. Maana za baadhi ya maneno yaliyotumika katika kijitabu hiki (Faharasa) yamewekwa mwisho ili kuleta ufahamu zaidi. Maoni yote na taarifa zaidi zinaweza kupatikana kwa kutumia anuani zilizopo nyuma ya kijitabu.

1. UTANGULIZI

Sura hii inaeleza:

- Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania (TzPPA) ya mwaka 2002/3 ilihusu nini;
- Nani waliofanya utafiti, wapi na vipi;
- Matokeo yatatumikaje; na
- Mpangilio wa kitabu hiki.

TzPPA ya mwaka 2002/3 ilihusu nini?

Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania ya mwaka 2002/03 ni shughuli iliyomo ndani ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa Umaskini wa Serikali. Katika mwaka 2002/3 mfumo huu ulipewa jukumu la kuchunguza:

- Vipengele vya kawaida na vyenye nguvu vinavyowaingiza watu katika umaskini;
- Namna watu mbalimbali wanavyoathirika na vipengele hivi, kwa nini na kwa matokeo gani; na
- Watu gani wako katika hatari kubwa ya kuwa maskini zaidi kesho kuliko walivyo leo.

Kwa maneno mengine, uchunguzi ulipewa jukumu la kutafuta maana na asili ya ***uathirikaji wa watu kwa umaskini*** nchini Tanzania hivi leo.

Nani walifanya utafiti, wapi na vipi?

NANI: Kwa sababu ya umuhimu wa kazi ya Tathmini Shirikishi ya Umaskini (TzPPA) katika Mkakati wa Serikali wa Kupunguza Umaskini, shughuli hii inatekelezwa na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa kusaidiwa na Kamati ya Utafiti na Uchambuzi (KUU). Ingawa TzPPA ni shughuli ya Serikali, inatekelezwa kwa ushirika wa Serikali na asasi za taaluma, pamoja na Asasi zisizo za Serikali (AZISE) za kitaifa na kimataifa. Mkabala huu wa ushirikiano umewezesha TzPPA kunufaika kutokana na namna nyingi za uzoefu na juhudi za kukamilishana.

Washirika wa Tathmini Shirikishi ya Umaskini (TzPPA)

- Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji
- Wizara ya Fedha
- Idara Kuu ya Takwimu
- Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii
- Concern kwa Jitihada za Maendeleo Afrika
- Taasisi ya Utafiti wa Jamii na Uchumi (ESRF)
- Taasisi ya Mitaala ya Maendeleo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Maarifa ni Ufunguo
- Umoja wa AZISE za Wafugaji
- Mradi wa Utunzaji Kumbukumbu na Utafiti wa Wanawake
- ActionAid-Tanzania
- AMREF
- Care-Tanzania
- Concern Duniani
- Save the Children, UK

WAPI na LINI: Shughuli za TzPPA zilikusanya na kuchambua taarifa kuanzia Machi hadi Julai 2002 katika jamii 30 za mijini na vijijini Tanzania nzima. Maeneo hayo yameonyeshwa katika ramani iliyoko nyuma ya kitabu hiki. Jamii hizi ni pamoja na watu wanaoishi kwa kutegemea kilimo, uvuvi, ufugaji na aina mbalimbali za kazi za mjini.

VIPI: Vikundi vya utafiti, vilivyojumuisha wajumbe wa ushirika wa TzPPA na Serikali za Mitaa, walitumia hadi majuma matatu kuandaa, kuhakiki na kuchambua takwimu pamoja na wanajamii kwa kila eneo la utafiti. Kwa sehemu kubwa taarifa ziliandaliwa na kuchambuliwa wakati wa kufanya kazi na vikundi vidogo vya watu ili washiriki wote kuwawezesha kupata muda kuzungumza na kusikika. Washiriki hao ni pamoja na wanaume na wanawake, watoto, vijana wa kike na wa kiume, wazee, walemavu, maskini na wenye uwezo n.k.

Hitimisho lililofikiwa katika vikundi hivi vidogo, liliwasilishwa baadaye katika mikutano ya jamii iliyokuwa wakati mwingine na watu zaidi ya mia saba! Katika mikutano hii mikubwa, watu walipata fursa ya kujifunza kutoka kwa majirani zao na kuyafanya matokeo kuwa bora zaidi kwa kupanua maoni yao au kupendekeza mabadiliko. Baadaye, watafiti na wanajamii kwa pamoja waliwasilisha matokeo kwa ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mtaa za Wilaya na Vyama vya Kiraia kama fursa ya mwisho ya kupima iwapo kazi yao imefanikiwa au haikufanikiwa kupata “picha kubwa” n.k.

JE, MATOKEO YA TzPPA YATATUMIKAJE?

Kitabu hiki hakina orodha ya vitu – kama vile shule mpya au pampu za maji – ambavyo watu wanahitaji katika jamii zao. Wala hakionyeshi nini kifanyike ili kukomesha umaskini. Kwa kweli ni kazi ngumu sana kwa mkabala huo rahisi kufanya mambo mengi mazuri. Badala yake, kitabu hiki kinatoa taarifa zinazowapa watu fursa ya kuzungumzia na kuamua namna bora zaidi ya kutafsiri sera au kushawishi utungaji sera na hatua zinazoonyesha hali zao halisi.

Kwa maneno mengine, kitabu hiki kinaeleza baadhi ya sababu muhimu kwa nini watu wengi bado wangali maskini nchini Tanzania. Ufahamu wa kina kuhusu umaskini utapatikana kutoka kwa waathirika kutokana na namna wanavyotoa maoni yao na ufumbuzi. Kwa kusoma muhtasari huu mtu yeyote anaweza kuainisha njia nyingi za kupunguza umaskini. Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Vyama vya Kiraia vimekwishaanza. Kwa mfano, Timu ya Usimamizi wa Manispaa ya Wilaya ya Ilala, imetumia matokeo ya TzPPA kutaarifu maamuzi ya bajeti, kubuni mikakati mipya kuhimiza fursa sawa ya kusoma kwa watoto wa kike na wa kiume, na kuunda vipengele vya wazi kwa ajili ya kutoa msaada wa kipaumbele kwa kaya zilizo maskini hasa vijijini.

KITABU HIKI KINATUELEZA NINI NA KIMEPANGWA VIPI?

Kitabu hiki ni “mwongozo wa lugha nyepesi” kwa muhtasari kutoka kwenye Ripoti Kuu ya TzPPA. Ripoti kamili ina mifano mingi ya utafiti na iliyochambuliwa kwa kina. Hata hivyo, kitabu hiki na Ripoti vinatoa taarifa ya namna moja. TzPPA pia imetoa seti ya Makala za Muhtasari wa Sera zinazolenga mada mahususi, kama vile uhusiano kati ya elimu na uathirikaji, afya na uathirikaji, n.k. Makala zote hizi, pamoja na taarifa nyingine nyingi kuhusu TzPPA na umaskini nchini Tanzania zinapatikana katika tovuti zifuatazo:

- http://www.esrftz.org/ppa
- http://www.tzonline.org
- http://www.tanzaniagateway.org

Baada ya utangulizi huu, Sura ya 2 inaangalia maana ya “uathirikaji” na kwa nini ni muhimu kuuelewa na kushughulikia. Kisha Sura ya 3 hadi ya 8 zinaangalia aina kuu za ugumu wa maisha zinazowaingiza watu katika dimbwi la umaskini na namna wanaume, wanawake na watoto wa kawaida wanavyoshughulikia kulinda ustawi wao. Sura ya 9 inatoa hitimisho na kujadili matokeo ya upunguzaji umaskini endelevu nchini Tanzania. Mwisho kitabu kinaishia kwenye faharasa inayotoa muhtasari wa maana ya maneno na mawazo muhimu.

2. UMASKINI, USTAWI NA AINA ZA UATHIRIKAJI

Sura hii inaeleza namna serikali ilivyopanua uelewa wake kuhusu umaskini na uathirikaji kwa kuzungumza na kusikiliza sauti za raia wa kawaida kupitia TzPPA.



2.1. UMASKINI NA USTAWI

Umaskini unahusu zaidi ya mtu kuwa na fedha au kutokuwa nazo mfukoni. Kwa hiyo, watu wanasemaje kuhusu kutaka maisha mazuri? Majibu yanaweza kupangwa katika mafungu:

Ustawi wa vifaa	Maana yake ni kuwa watu wanahitaji kuwa na chakula cha kutosha, maji safi, zana za kuendeshea maisha, nyumba n.k.
Ustawi wa mwili	Maana yake ni kuwa watu wanataka kujisikia wazima, wenye afya na nguvu.
Ustawi wa kijamii	Maana yake ni kuwa watu wanataka kujisikia wanatunzwa na kujaliwa na familia na marafiki, na kuishi mahali penye amani na uelewano.
Usalama	Maana yake ni kuwa watu wanataka kujisikia salama kimwili na kuwa na imani kuhusu ustawi wao wa baadaye.
Uhuru wa kuchagua na kutenda	Maana yake ni kuwa watu wanataka kupata elimu bora, kuwa na stadi za kutosha za maisha na kuweza kushiriki katika maamuzi yanayoathiri maisha yao.

"Umaskini" ni kutotimiza mahitaji hayo ya msingi *leo*.

2.2. UATHIRIKAJI KWA UMASKINI

Watu wanatumia neno "Uathirikaji" kwa njia tofauti. Hii inasababisha utatanishi. Kwa mfano, mara nyingi tunasikia vijana wakielezwa kuwa hatarini zaidi kuathiriwa na VVU/UKIMWI. Wanachojaribu watu kusema ni kuwa vijana wamo katika uwezekano mkubwa mno wa kupata ugonjwa huo kuliko wengine.

Tunaweza pia kuzungumzia uathirikaji wa watu kwa umaskini. Kwa hali hii, tunazungumzia kuhusu *uwezekano wa watu kuwa maskini zaidi kesho kuliko walivyo sasa*.

Njia moja ya kuangalia tofauti kati ya umaskini na uathirikaji ni kuufikiria umaskini kama ufafanuzi wa namna mambo *yalivyo sasa* na uathirikaji kama namna mambo *yanavyotarajiwa kuwa baadaye.*

2.3. KITU GANI KINAWAFANYA BAADHI YA WATU KUATHIRIKA NA UMASKINI ZAIDI KULIKO WENGINE?

Uathirikaji ni matokeo ya mwingiliano wa mambo mengi yanayowaingiza watu katika umaskini ikilinganishwa na uwezo walio nao na unaofaa kukabiliana na matatizo mbalimbali.

Pengine hii inaweza kueleweka kwa urahisi kwa kufikiria tukio ambapo watu wanajitahidi kupanda ngazi ya ustawi. Kadri wanavyojitahidi kwenda juu, watu wanakabiliwa na mambo tofauti yanayotishia kuwarudisha chini. Katika kukabiliana na hali halisi wanajaribu aina zote za mbinu za kuwazuia wasianguke. Kwa mfano, wanaweza kujaribu kukwepa kutumbukia upande mbaya, kushirikiana na wengine ili kupata msaada wa pamoja n.k.

Wale watu wenye njia chache zaidi za kukabili mambo mabaya (kama ugonjwa au wizi wa mali) yanayoweza kuwatokea wako katika hatari ya umaskini kuliko wengine.

SABABU ZINAZOLETA UMASKINI

Mambo yanayowatishia watu kutumbukia katika umaskini yanaitwa **sababu zinazoleta umaskini**. Hizi ni pamoja na mishtuko ya maisha (kama vile ugonjwa wa ghafla) na mifadhaiko (kama vile kuathiriwa pole pole kwa maliasili). Njia mojawapo ya kufikiria kuhusu tofauti kati ya mishtuko na mifadhaiko ni kwamba ya kwanza inaharibu rasilimali na ustawi wakati ya pili inazimomonyoa. Mishtuko na mifadhaiko muhimu zaidi iliyoainishwa na wanajamii wanaoshiriki katika kipindi chote cha TzPPA imo katika makundi sita yafuatayo:

Kundi	Maelezo
Mazingira	Sababu zinazoleta umaskini ni pamoja na mishtuko mbalimbali (kama vile mafuriko) na mifadhaiko aina tofauti (kama ilivyo kwa kuathirika pole pole kwa misitu, udongo, uvuvi na malisho). Sababu zinazoleta umaskini zinazohusiana na mazingira zinaathiri ustawi wa mali wa watu, afya zao na kuwa na imani ya ustawi wa baadaye.
Marekebisho ya uchumi mkubwa	Kukosa maamuzi ya kitaifa kuhusu uchumi mkubwa yanaathiri viwango vya ajira, faida ya shughuli za maisha ya vijijini, gharama za kupata huduma muhimu, n.k. Kutokana na utandawazi baadhi ya maamuzi ya uchumi mkubwa yaliyofanywa na nchi nyingine (kama vile uamuzi wao wa kufidia bidhaa zao za kilimo) pia yanawagusa watanzania wa kawaida na kuwaletea mishtuko na mifadhaiko.
Utawala	Sababu nyingi za kuleta umaskini zinahusika moja kwa moja na majukumu ya serikali katika kusimamia utawala. Hizi ni pamoja na mishtuko (kama vile utozaji wa bei ya juu na aina nyingine za rushwa) na mifadhaiko (kama vile kodi za usumbufu na kutengwa kisiasa).

Hali ya afya	Utapiamlo, kuumia maradhi (hasa VVU/UKIMWI) na aina nyingine za maradhi ya mwili na akili mara nyingi huathiri mali za watu, ustawi wa mwili na jamii.
Hatua za maisha na hali inayohusiana na umri	Watu wako hatarini kuathiriwa na baadhi ya sababu zinazoleta umaskini kutokana na mahali walipo katika hatua za maisha. Kwa mfano, watoto, wanawake wa umri wa kuzaa na wazee wote wanakabiliwa na hatari maalumu za kiafya.
Imani za mila na desturi na tabia	Njia mbalimbali za kimila zinazotumika kufanya mambo, huleta matatizo na vikwazo vya mahali katika maisha ya baadhi ya watu – hasa wanawake na watoto.

HATUA ZA KUKABILI

Wanawake, wanaume na watoto mara nyingi wanajitahidi kuzuia kutumbukizwa katika umaskini wa ustawi nao. **Hatua za kukabili** zilizochaguliwa kwa makini kutoka katika uchaguzi uliyopo, zimedhamiria, zina ubunifu na mara nyingi ni pamoja na:

- Kuzuia sababu za kuwa maskini zisitokee;
- Kuwa mbali na watu wengine;
- Kupunguza athari ya wale wasioweza kuwazuia au kuwaepuka; na
- Kuhimili matokeo.

Kuzuia, kupunguza kasi na kuhimili

Mishtuko na mifadhaiko mingi inaweza kuzuiwa isitokee. Hivi ndivyo wakulima wenye wasiwasi wa mmomonyoko wanavyojaribu kufanya wanapojenga matuta. Pia inaweza kuonekana kwa kile watu wanachofanya wakati wanapowekeza katika kutumia vyandarua. Hizi na hatua nyingine zilizokwisha tarajiwa zinavyofanyakazi na hivyo kutekeleza jukumu muhimu katika kupunguza uathirikaji wa watu.

Hata hivyo, baadhi ya sababu zinazoleta umaskini haziwezi kuzuiwa. Katika hali kama hiyo, watu wanatumia nguvu zao katika kutuliza au kupunguza athari ya mishtuko na mifadhaiko. Baadhi ya juhudi hizi zinafanywa kabla matatizo hayajatokea. Kwa mfano wafugaji wanakuwa na aina mbalimbali za makundi yao ya mifugo na wakulima wanalima mazao mahususi ili kumudu kaya zao wakati wa ukame. Watu pia wanajaribu kujenga misingi ya rasilimali ili iwafae wakati wa uzeeni – kile wanachokiita watu wa Mchinga II (Wilaya ya Lindi Vijijini), akiba ya ujana, au “kuweka akiba tangu ujana”.

Kinyume chake mikakati mingine ya kutuliza, kama vile matumizi ya mbolea za kemikali ili kufidia upungufu wa rutuba ya ardhi; huanza wakati mishtuko na mifadhaiko inapojitokeza.

Ingawa shughuli hizi hazizuii kutokea kwa shida, hupunguza makali ya kutokea kwake. Kwa hiyo, watu lazima wavumilie matokeo yake. Katika ngazi ya mtu mmoja mmoja na kaya, hii imesababisha watu kuuza rasilimali (ikiwemo mali inayozaa kama vile ng’ombe au ardhi) ili wapate fedha na pia kuwaachisha watoto shule ili wachangie katika mapato ya familia. Katika ngazi ya jamii, imewasababisha watu wakusanye rasilimali ili waweze kuwatunza mayatima wa VVU/UKIMWI. Mikakati hii ya kuhimili, huwasaidia watu kuishi, lakini pia kuunda hatua muhimu katika kuwaandaa kuondokana na sababu zinazoleta umaskini na kurejesha ustawi wao.

Mbinu za kukabili	Lengo	Mfano
KUZUIA	**Kuzuia mambo mabaya yasitokee tangu mwanzo**	• Panda mazao kwa mzunguko na kutia mbolea ya mboji ili kurutubisha ardhi • Lala kwenye vitanda vyenye vyandarua ili kuzuia malaria
KUPUNGUZA KASI	**Punguza athari ya ugumu wa maisha**	• Hifadhi chakula endapo ukame utasababisha upungufu wa chakula msimu ujao • Kuwa na njia mbalimbali za kujipatia maisha endapo faida ya shughuli moja itapungua
KUHIMILI	**Kuyafanya matokeo ya hali ngumu yawe bora**	• Kukopa fedha au rasilimali nyingine ili kufidia mahitaji ya muda mfupi • Wachukue mayatima ili wasife njaa

VIPENGELE VINAVYOKWAZA

Sababu mbalimbali zinazoleta umaskini – kama vile ugonjwa na kupungua rutuba ya udongo – zinatoa wito wa kuchukua hatua mbalimbali. Suala ni iwapo watu wataweza kuchukua na kutekeleza hatua zinazofaa ambazo hazitahatarisha ustawi wao au wa watu wengine hapo baadaye. Jibu mara nyingi linategemea:

- Rasilimali walizonazo; na
- Vipengele vinavyoelekea kukwaza au kuzuia matumizi yao.

Rasilimali

Rasilimali za mtu ni pamoja na uhusiano, uwezo wao na vitu vyote wanavyomiliki au wanavyoweza kutumia. Rasilimali pia zinafikiriwa kuwa aina ya "mtaji". Aina sita za rasilimali au mtaji zitakazosaidia watu kukabili sababu zinazoleta umaskini ni:

Aina ya Rasilimali	Maelezo
Mtaji wa Asili	Hii inahusu ardhi, maji, na viumbe hai (kama vile malisho na misitu) wanavyotumia watu kukidhia mahitaji yao kwa ajili ya kupikia, kujengea na mavazi. Wakati mwingine hujulikana kama rasilimali za mazingira. Thamani ya mtaji wa asili huongezeka kutokana na maarifa na stadi za kuugeuza kuwa bidhaa za matumizi na/au kuuza. Baadhi ya aina za mtaji wa asili (kama vile maji na miti) zina uwezo wa kujirejeshea viwango vyao kwa upya kadiri muda unavyopita. Mtaji wa asili usiyoweza kurudishiwa upya kama dhahabu, huenda moja kwa moja mara baada ya kutumiwa.
Mtaji wa Fedha	Hii inahusu fedha katika mfumo wa akiba, malipo, zawadi au mikopo. Mtaji wa fedha unafaa sana kwa sababu ni rahisi kubadilisha kuwa chakula, elimu, dawa, ardhi, zana n.k.
Mtaji wa Siasa	Watu wenye ushawishi juu ya maamuzi ya kisiasa yanayoathiri maisha yao wanasemekana kuwa na mtaji mzuri wa siasa. Hii ni muhimu sana hasa inapohusisha vikundi vya kijamii na mifumo ya soko. Mtaji wa siasa unategemea vipengele vingi vinavyojumuisha tabaka, kabila, jinsia, umri, kazi ya kuendeshea maisha na ulemavu.
Mtaji wa Watu	Rasilimali hii ni nguvu kazi ya mtu au kaya. Inaathiriwa na kiwango cha maarifa, stadi na elimu watu walicho nacho. Elimu na mafunzo ni muhimu kwa kuendelezea aina hii ya mtaji unaoweza kutumiwa katika kutumia vizuri rasilimali nyingine. Afya pia ni muhimu kwa kutumia mtaji wa watu.
Mtaji wa Vitu	Hii inahusu vitu vilivyotengenezwa ili kusaidia watu kuendeshea maisha. Mifano ni pamoja na zana za kilimo, nyavu za kuvulia na barabara.
Mtaji wa Jamii	Watu wanaoweza kushirikisha wanafamilia na jamii mbalimbali wakati wanapohitajika, wana mtaji wa jamii mzuri. Watu wa Tanzania mara nyingi wana mitandao mikubwa ya familia, marafiki, walezi na wateja. Hawa wanaunganisha miji na vijiji na mara nyingi wameenea katika kanda nyingi za hali ya hewa na misimu mbalimbali.

Maskini wana rasilimali chache, na matokeo yake wana uchaguzi na fursa chache kuliko wale wenye uwezo. Ndio maana wanaathiriwa zaidi na kupungua katika ustawi.

VIKWAZO

Kuwa na rasilimali nyingi haina maana zinaweza kutumiwa kukabili sababu zinazoleta umaskini. Watu wanajishughulisha ndani ya mazingira magumu na tata yanayoweza kuzuia kile kinachoweza kufanyika na kwa gharama yoyote - kwa kile walichonacho. Mazingira hayo yanaonyesha:

- Sifa za mtu, kaya na jamii; na
- Hali ya utamaduni wa jamii, siasa, uchumi na mazingira.

Kwa mujibu wa wanajamii ambao wameshiriki katika zoezi la TzPPA, baadhi ya vipengele vinavyokwaza ni:

Vipengele vinavyokwaza	**Maelezo**
Kukosa matumaini	Baadhi ya watu wanakata tamaa wanapopata mishtuko, mifadhaiko ya maisha na kuwepo njia chache za kudumisha ustawi wao. Inapotokea hivyo, watu wanashindwa kutumia ipasavyo rasilimali walizonazo. Katika baadhi ya matukio kukosa matumaini kunasababisha matumizi ya dawa za kulevya, wakati mwingine, husababisha uvivu kwa vijana wasiotaka kufanya kazi.
Rushwa, utawala mbaya wa umma na sera	Washiriki wa TzPPA mara kwa mara wamekuwa wakitaja rushwa, umbali wa kwenda kwenye huduma za jamii, na sheria/sera kama ni kero. Kwa hiyo wanajamii wamehitimisha kuwa: • Huduma za jamii ni muhimu sana katika juhudi zao za kuepuka kuwa maskini zaidi. Ingawa mara nyingi wanakabili changamoto mbalimbali katika kupata rasilimali hizi, kikwazo kikubwa ni *rushwa*. Hali kama vile utoro wa walimu na wanaotoa huduma za afya, uhaba wa dawa muhimu na mabomba na pampu za maji zilizoharibika, nazo zinazidi kufanya *umbali halisi wa kuelekea katika huduma za jamii* kuwa mrefu sana kuliko mafanikio ya kitakwimu yaliyoonyeshwa katika Utafiti wa Bajeti ya Kaya wa 2000/1.

	• *Sheria, sheria ndogo na kanuni* huathiri mara kwa mara uchaguzi wa watu kwa njia mbalimbali. Mfano ulio wazi ni ule wa sheria zinazokataza moja kwa moja baadhi ya hatua za kuchukuliwa na adhabu za kutisha patokeapo ukiukaji. Hii mara nyingi huhalalishwa kwa vile serikali inahitaji kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali za pamoja, kulinda afya ya umma n.k. Hata hivyo, watu wanaelewa kuwa baadhi ya sheria zinapendelea kwa sababu zinadumisha maslahi ya wachache.
Tabia na utamaduni wa jamii katika umiliki, madaraka na upendeleo	Baadhi ya mila na desturi hudumisha mfumo unaoonyesha nani wanaomiliki rasilimali zinazoonekana na namna zinavyotumika, nani anayepata stadi zenye thamani na nani anayeshawishi maamuzi muhimu. Kwa maneno mengine tabia ya utamaduni wa jamii katika *umiliki, madaraka na upendeleo* inakwaza uchaguzi uliopo kwa baadhi ya watu huku ikikuza wa wengine. Tabia hizi zipo katika kaya, jamii na katika ngazi ya juu na husababisha uathirikiaji wa vikundi vinavyohitaji msaada maalumu.

Baadhi ya vipengele vinavyokwaza, kama vile matatizo ya uchumi-mkubwa, huathiri watu wote. Vipengele vingine, kama vile kanuni za utamaduni zinazopunguza nguvu za jumuiya za wanawake au kubagua watu wenye ulemavu, huathiri tu baadhi ya watu wa vikundi vya kijamii. Matokeo yake ni kwamba makundi yalioathirika yanashindana na mzigo mkubwa zaidi wa matatizo yaliyolimbikizwa ambayo pia yanaathiri uwezo wa kukabili mishtuko na mifadhaiko.

Makundi ya kijamii yenye *uwezo mdogo* wa kukabili mishtuko na mifadhaiko ndio walio hatarini zaidi na yanajumuisha:

- Watoto (hasa mayatima);
- Wanawake wenye umri wa kuzaa / wanawake wenye watoto wadogo;
- Wajane;
- Wazee;
- Walemavu;
- Watu wenye maradhi sugu;
- Watu katika kaya zilizoathiriwa na VVU/UKIMWI; na
- Mafukara.

2.4. Mitego ya Umaskini

Watu waliomo katika makundi ya jamii yaliyo hatarini zaidi kukabili mishtuko na mifadhaiko wanazo njia chache za kutanzulia matatizo yao. Mara nyingi hawana la kufanya zaidi ya kushindwa kuwekeza katika elimu na/au kuuza waliochonacho (kama zana, ardhi au mifugo) ili kupata njia ya kuendeshea maisha. Vitu hivi mara nyingi vinawatia watu katika “mtego wa umaskini” na kushindwa kujinasua bila msaada. Kutokea mara kwa mara kwa mitego ya umaskini ni kikwazo kikuu katika kutimiza malengo ya maendeleo ya Tanzania na sehemu kubwa ya sababu ya watu kuhofia uathirikaji.

3. MAZINGIRA NA UATHIRIKAJI

Mishtuko na mifadhaiko inayohusiana na mazingira inaleta tishio kubwa la moja kwa moja kwa ustawi wa watu. Kwa mfano, ukame unaathiri mifugo na uzalishaji wa kilimo. Wakati huo huo, husababisha shida zaidi za uendeshaji wa shughuli za kila siku za kaya (zikiwemo "shughuli muhimu za kila siku" kama vile kupika na kufua). Hii inamuathiri mtu kimwili, pamoja na ustawi wa vifaa.

Uathirikaji wa mazingira unaweza kuleta matatizo makubwa kwa uwezo wa watu kushughulikia sababu mbalimbali nyingine zinazoleta umaskini. Ndio maana mazingira hayana budi kuwa jambo kuu la kuzingatiwa kwa ajili ya mikakati, na shughuli za kutekeleza mikakati hiyo, ili kupunguza kiuendelevu umaskini nchini Tanzania.

Sura hii inalenga kushughulikia mambo mawili yafuatayo:

- Washiriki wa utafiti wa TzPPA wamejifunza nini kuhusu mishtuko na mifadhaiko yenye nguvu na inayoendelea inayohusiana na mazingira kueleza; na
- Kueleza namna watu wanavyojaribu kumudu hali halisi hizo, kwa matokeo gani na kwa nini.

3.1. MISHTUKO NA MIFADHAIKO INAYOHUSIANA NA MAZINGIRA

Wanajamii walioshiriki katika TzPPA waliainisha mishtuko na mifadhaiko mingi inayohusiana na mazingira. Kutokana na taarifa ya jumla ya hali ya umaskini Tanzania, iliyo muhimu zaidi ni ukame na uharibifu wa mazingira. Sababu zote zinazoleta umaskini zilizoainishwa na wanajamii zinaweza kupangwa katika makundi manne yafuatayo:

1. Hali mbaya ya hewa au isiyotabirika
2. Uharibifu wa mazingira
3. Uchafuzi wa mazingiria na
4. Wanyama pori, wadudu waharibifu na maradhi

3.1.1. Sababu zinazoleta umaskini zinazohusiana na hali ya hewa

Watu wengi wana imani kuwa tabia za hali ya hewa hivi sasa zinazidi kuwa mbaya na zisizotabirika. Na hatuna uhakika iwapo hii ni kweli au si kweli na kama ni hivyo, iwapo hali hiyo ni kwa Tanzania nzima au hapana. Hata hivyo, hatujui iwapo mafuriko, ukame, na mvua zisizo na uhakika huwatumbukiza watu katika umaskini.

Mafuriko

Mafuruko ni ya kawaida katika maeneo ya bondeni/yenye mvua kubwa nchini. Hata hivyo, kutokea kwake, ukubwa na muda wa mafuriko haya na maeneo mengine mara nyingi husababishwa na binadamu. Mafuriko kama yale yaliyofuatia mvua za El Nino za mwaka 1997/8 hayatabiriki sana na huathiri maeneo ambayo hayakuzoea na yenye maandalizi duni ya kushughulikia tukio hilo.

Katika hali zote hizo, mafuriko yanaweza kuathiri ustawi wa watu kwa njia mbalimbali. Njia hizo ni pamoja na:

- Kuharibu mazao na kuwazuia wakulima wasipande;
- Kuharibu nyumba;
- Kueneza maradhi miongoni mwa binadamu na mifugo; na
- Kuharibu mahali pa kazi, barabara na madaraja.



Mfano wa mafuriko unadhihirisha namna mishtuko na mifadhaiko ya kimazingira inavyoweza kuathiri zaidi ya njia za maisha ya watu na kiwango cha umaskini wa kipato.

Ukame

Ukame unaweza kuharibu mazao yanayomwagiliwa maji ya mvua. Unaweza pia kukausha mikondo ya maji na visima ambavyo watu wanategemea sana kumwagilia mazao mengine na kujikimu wao wenyewe na wanyama wao. Wakati mazao yanapoharibika na mifugo inapokufa, bei za mazao ya kilimo zinaelekea kupanda wakati zile za mifugo zinashuka. Hii inadhihirisha hoja muhimu nyingine ambayo ni: *Utokeaji wa mishtuko ya kimazingira una matokeo tofauti kwa njia tofauti za kuendeshea maisha.*

Aidha kuhusu athari yake kwa namna watu wanavyojiendeshea maisha yao, ukame unaleta matatizo ya kiafya na ongezeko la idadi na ukubwa wa mioto ya misitu. Mioto hii inaharibu mali na mifumo ikolojia muhimu watu wanayoitegemea kwa chakula, dawa, n.k. – hasa wakati wa uhaba wa chakula.

Mvua zisizo na uhakika

Wakati mwingine mvua zinawahi sana au kuchelewa mno. Hii inaweza kuleta maafa kwa maisha ya watu kama yalivyo mafuriko na ukame. Kama ilivyoelezwa na mmoja wa utafiti wa TzPPA wa kijiji cha Mwakizega (Wilaya ya Kigoma Vijijini):

> *"Unaingia gharama za kutayarisha shamba, unapanda mbegu, halafu mvua hazinyeshi, au zinachelewa sana -- na mazao yanaharibika".*

Si mvua zilizowahi wala zilizochelewa ambazo mara nyingi zinahesabiwa kuwa ni "maafa ya asili". Hata hivyo, athari yake inaweza kuwa ya uharibifu. Hii inaonyesha kuwa "maafa" yanahitaji kufanyiwa tathmini na kuelezwa kwa msingi wa namna yanavyoathiri kaya na si kwa msingi wa ukubwa au muda.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Mipango ya mkoa ya upandaji miti upya na udhibiti wa vyanzo vya maji, pamoja na mambo mengine inaweza kuzuia au kukomesha mishtuko na mifadhaiko inayohusiana na hali ya hewa. Hata hivyo, watu wengi wanadhani kuwa ni matukio yasiyoepukika ya Mungu. Matokeo yake, mtu mmoja mmoja na asasi huzingatia zaidi kupunguza athari ya sababu hizi zinazoleta umaskini au kushughulikia matokeo yake. Mifano ya kila moja ni pamoja na:

Kupunguza Athari	**Kuendelea Kuishi**
Kujiwekea akiba ya chakula ili kukidhi mahitaji ya wakati wa shida.	Kuuza raslimali ili kununua chakula, kujenga upya nyumba, n.k.
Kuwa na njia mbalimbali za kuingizia mapato ya kaya ili watu wasitegemee sana hali nzuri ya hewa.	Kutegemea sana "mbinu za kijamii za kusaidiana" au kupokea misaada ya dharura kutoka Serikalini au Vyama vya Kiraia.
Kujenga mifereji mizuri ya umwagiliaji maji na upitishaji maji.	Kuhama ili kutafuta kazi ya mshahara.

3.1.2. Uharibifu wa Mazingira

Zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wanaishi vijijini ambapo maisha yao yote yanategemea sana matumizi ya moja kwa moja na/au kubadili mtaji asilia wa mahali. Aidha wanategemea maliasili kwa kupikia, kufua, kujazia vyakula vinavyolimwa, kujitibu, kujenga na kukarabati nyumba zao na kutengeneza vifaa.

Ingawa maisha ya wakazi wengi wa mijini hayategemei moja kwa moja mtaji asilia, wanategemea kwa kiasi fulani katika maisha yao ya kila siku. Hata miji kama ya Dar es salaam, kaya nyingi zinatumia kuni au mkaa kama nishati kuu. Kwa hiyo, kupungua kwa vyanzo vya maliasili, humwathiri *kila mtu* nchini Tanzania. Ndiyo maana washiriki wa TzPPA wamekuwa na wasiwasi sana na kupungua kwa ubora na wingi wa:

- Uvuvi;
- Udongo;
- Malisho;
- Misitu/uoto wa ardhi;
- Rasilimali asili zisizo za misitu; na
- Maji.

Uvuvi

Katika mwambao wa bahari na maziwa ya maji baridi, watu wamekuwa wakilalamika kuhusu kupungua sana kwa idadi ya samaki. Hata wengine wanasema kuwa baadhi ya aina za samaki waliokuwa wakipatikana sana hivi sasa ni adimu au wametoweka kabisa na sababu hazieleweki. Wavuvi wa Mwanza wanaamini kuwa ni kutokana na uchafuzi na uvuvi kupita kiasi. Wakati huo huo, watu wa kijiji cha Ikombe (Wilaya ya Kyela) wanadhani ni matokeo ya kuvua karibu sana na upwa na uharibifu wa mazalio makuu ya samaki.

Kwa kiasi fulani baadhi ya uharibifu huu wa makazi na mazingira ya samaki husababishwa na mbinu zilizopigwa marufuku wanazotumia kwa sababu wana shauku kubwa ya kulisha familia zao wakati wa msimu wa mvua. Hii inasababisha wasiwasi mkubwa na muhimu, hasa:

Watu wasio na rasilimali za kutosha wana uchaguzi finyu wa kukabiliana na mishtuko na mifadhaiko. Ndiyo maana watu maskini wanalazimishwa kwa urahisi kuchukua mikakati ya muda mfupi ya maisha inayoharibu matarajio yao ya muda mrefu.

Udongo

Wakulima wengi walioshiriki katika TzPPA wameeleza kuanguka kwa uzalishaji wa kilimo kutokana na kupungua kwa ubora wa kiwango cha udongo. Walitoa maelezo ya aina mbili kuhusu kukua kwa tatizo hili. Tatizo la kwanza ni mmomonyoko wa udongo. Na tatizo la pili ni kubadili bila ya mpangilio teknolojia za "mapinduzi kijani" kwa mbinu za kilimo za asili (kama vile kuacha kulima shamba kwa muda) na kusababisha udongo kutegemea sana mbolea za kemikali.

Malisho

Wafugaji wanadhani kuwa malisho mabaya zaidi pia ni matokeo hasa ya kutoweka kwa mikakati ya udhibiti wa rasilimali wa kiasili. Hata hivyo, wanasema matokeo hayo yanatokana na mabadiliko ya mitindo ya umiliki wa ardhi unaozuia kutumika kwa mbinu za asili. Kusema kweli makundi ya mifugo hivi sasa ni madogo kuliko yalivyokuwa zamani, lakini kukosekana kwa eneo la malisho kumepunguza makundi ya mifugo kiasi cha kuangamiza maeneo makubwa ya malisho ya zamani kama yale ya Tambarare za Wembere.

Hoja mbili muhimu sana zilizotolewa na wanajamii kuhusu maliasili wanazozitegemea ni pamoja na:

1. Inakuwa vigumu sana kupata maliasili kwa watu wanaozitegemea kwa maisha yao.
2. Kule kukosa na kupungua kwa ubora wa maliasili muhimu kunaathiri faida na hata kumudu maisha. Hii inaathiri msingi wa rasilimali za watu na uwezo wa kukabili sababu mbalimbali zinazoleta umaskini.

Misitu na Rasilimali asili zisizo za misitu

Misitu na rasilimali za porini zisizo za miti (ikiwemo vyakula, chakula cha mifugo na dawa) pia ziko hatarini. Uvunaji usio endelevu wa rasilimali hizi na bidhaa nyingine za mazingira – mara nyingi unafanywa na watu wenye uwezo wanaoweza kuwekeza katika misumeno ya umeme, malori ya kubebea mkaa, n.k. – ina maana pia kuwa inazidi kuwa vigumu zaidi kupata fursa ya kuvuna kwa watu walio maskini sana.

Maji

Kutokupata maji ya kutosha lilikuwa suala la kipaumbele miongoni mwa wanajamii katika maeneo ya ukame na katika maeneo ya mjini kama vile Dar es Salaam, ambapo mahitaji ya maji ya kila siku mara nyingi yanagharimu zaidi kwa upande wa muda na fedha kuliko uwezo wao.

Watu wengi walikuwa na shaka kuhusu ubora wa maji yao ya matumizi ya nyumbani, ambayo yanaathiriwa na kupenya kwa maji ya chumvi katika mwambao (kutokana na udhibiti mbaya wa rasilimali) na kuchafuliwa na maji taka ya kibiolojia, kilimo na viwanda. Baadhi ya sababu muhimu sana zinazoleta umaskini zilizohusishwa na washiriki wa utafiti na upataji mdogo wa maji safi zinawasilishwa katika jedwali lifuatalo:

1. *Upatikanaji* mdogo unaweza kusababisha kupungua kwa uzalishaji	Wakati watu wanalazimika kutenga muda zaidi kwa ajili ya kuchota maji, wanapata muda mchache kwa mambo mengine. Kwa kuwa wanawake na watoto kwa kawaida ndio wanaopewa jukumu la kuteka maji kwa ajili ya matumizi ya kaya, ina maana kuwa wanawake hawapati muda wa kutumia kwa shughuli nyingine za uzalishaji na watoto wanakosa muda wa majukumu yao mengine na michezo (ambayo ni sehemu muhimu sana ya makuzi ya utoto). Katika maeneo ya ukame, vijana mara nyingi hupewa jukumu la kunywesha mifugo. Iwapo hakuna maji karibu, hawana budi kupeleka mifugo yao hadi vyanzo vya mbali. Safari ndefu hupunguza kiwango cha uzalishaji maziwa, na huwa mbali kufikiwa na wanakaya waliobaki nyumbani.
2. *Upatikanaji* mdogo unaweza kuongeza matumizi ya kaya	Gharama ya kununua maji katika Kata ndogo ya Sokoni (Manispaa ya Wilaya ya Kinondoni) ni Tsh. 100 kwa ndoo ya lita 20, lakini hufika Tsh. 500 wakati wa ukame au wakati wa tatizo la maji. Bei hizi huwa

	zinakatazwa. Kwa mujibu wa washiriki wa utafiti, watu wanazoea kwa: • Kutumia maji kidogo kuliko wanavyohitaji; • Kupunguza matumizi ya mahitaji mengine ya msingi; na • Kununua maji machafu (hasa yaliyotekwa katika visima vifupi vyenye chumvi nyingi na/au kiwango kikubwa cha uchafu wa kibiolojia). Kila moja ya njia hizo, hutatua tatizo moja na kuzusha jingine kama vile kupungua kwa lishe na kuwa hatarini kuambukizwa maradhi yanayosababishwa na maji.
3. *Upatikanaji* mdogo unaweza kusababisha kuzuka kwa migogoro ya kijamii	Watu wanahitaji maji kwa ajili yao na wakati mwingine kuendeshea maisha yao. Iwapo watu wengine watakoseshwa au kunyimwa na watumiaji wengine au kutokana na rushwa, mgogoro utaibuka. Iwapo hautatanzuliwa, utasababisha aina ya ugomvi uliotokea katika kijiji cha Twatwatwa (Wilaya ya Kilosa) mwaka 2000. Katika maeneo mengine kulikuwa na ushindani kati ya watumiaji/matumizi ya maji ya vijijini kikiwemo kijiji cha Fukayosi (Wilaya Bagamoyo) ambapo TzPPA ilifanyiwa majaribio. Wakati huo huo wakazi wa Kata ndogo ya Sokoni (Manispaa ya Kinondoni) wamedai kuwa viongozi wanachangia kuharibika kwa mabomba ya umma na kuwasababisha watu wategemee maji ya binafsi ambayo ni gharama. Bila ya kujali iwapo ni kweli au uwongo, tatizo hili la muda mrefu linasababisha kutoridhika na huathiri uwezo wa viongozi na raia kushirikiana katika kuboresha hali ya mahali.
4. *Ubora* usiofaa unasababisha ongezeko la afya mbaya	Wakati watu wasipopata maji safi na salama, wanakuwa katika hatari ya kupata maradhi ya ngozi na maradhi yanayotokana na vyanzo vichafu. Hii huathiri ustawi wa miili yao na ustawi wa mali iwapo watalazimika kusamehe kazi na/au kutumia fedha chache kwa matibabu.

3.1.3. Uchafuzi

Washiriki wa TzPPA walihitimisha kuwa uchafuzi kutokana na taka za viwanda, umma na binafsi huchafua mazingira yao na kuathiri ustawi wao. Walitaja mifano ya uchafuzi wa hewa, maji na ardhi, kuwa unaathiri afya zao na maisha.

Taka za Viwanda

Katika maeneo ya utafiti manne kati ya matano ya mijini, washiriki waliona kuwa uchafu wa viwandani unatia sumu katika mazingira yao. Kwa mfano, watu wa Kata ndogo ya Pongwe (Manispaa ya Wilaya ya Tanga) walilalamika kuwa uchafu wa hewa unaotolewa na kiwanda cha karibu cha Saruji cha Pongwe ulisababisha matatizo ya kupumua na maumivu ya kifua. Wakati huo huo, wanajamii wa Kata ndogo za Kigoto na Ibanda (Manispaa ya Mwanza) waliamini kuwa viwanda vya karibu vilikuwa vikichafua vyanzo vya maji na kusababisha matatizo ya tumbo na maradhi ya ngozi.

Taka za Umma

Watu wa Dar es Salaam walikuwa wepesi kuainisha maeneo ya taka ngumu yanayodhibitiwa vibaya kama tatizo jingine kubwa. Kwa mfano, wanajamii wanaoishi na kufanyakazi kandokando ya soko la Tandale katika Kata ndogo ya Sokoni (Manispaa ya Kinondoni) wameona kuwa taka zilikuwa hazichukuliwi mapema na kusababisha marundo makubwa ndani ya soko. Hii ilisababisha harufu mbaya iliyowakimbiza wateja na kupunguza biashara na thamani za mali. Watu pia waliona kuwa marundo ya taka za nyumbani yalikuwa vyanzo vya maradhi na kusababisha mazalio ya panya wanaoambukiza maradhi.

Taka za Nyumbani

Washiriki waliainisha utupaji taka za nyumbani kuwa ni tatizo – hasa taka za binadamu. Katika maeneo ya vijijini, tatizo hili wakati mwingine hutokana na kukosa maarifa kuhusu afya na usafi bora.

Katika maeneo mengi ya mijini kuna matatizo kutokana na msongamano na kukosekana na kwa njia salama za kutapisha vyoo au kupunguza matanki ya maji machafu. Ni vigumu sana kuchimba choo katika maeneo ya msongamano mkubwa. Katika makazi ya mijini yasiyopimwa watu hawana uteuzi zaidi ya kutupa uchafu wa mwilini na mwingineo kwa kuweka katika mifuko ya plastiki na kutupa kando ya barabara, kati ya mifereji ya maji machafu au katika marundo ya taka za umma.

Ongezeko la ukubwa wa tatizo la aina hizo tatu za uchafuzi linaonyesha namna "maendeleo ya uchumi" – yanayoonekana kwa uzalishaji mkubwa wa viwanda, kukua kwa soko na ongezeko la watu – linaweza kuleta madhara makubwa kwa maisha ya watu wengi na njia za kuendeshea maisha iwapo halitarekebishwa.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuzuia

Utekelezaji wa sheria za serikali na za kimila utazuia vitisho vikubwa kwa idadi na ubora wa maliasili nchini Tanzania. Sheria hizi zinaweza kupiga marufuku au kuzuia. Kwa maneno mengine zinaweza kuidhinisha baadhi ya hatua za kuchukuliwa (kama vile kujenga vyoo vya shimo ili kutunza usafi na usalama wa vyanzo vya maji) au kukataza (kama vile ukataji wa mikoko inayoleta kivuli kwa samaki wanaokua).

Kupunguza Kasi

Iwapo maliasili inayotegemewa watu inapunguza idadi na/au ubora, watu hujaribu kupunguza athari kwa njia mbalimbali. Baadhi ya njia zilizo muhimu sana ni:

- Kuongeza mbolea ya kemikali mashambani;
- Kubadili zana za uvuvi na/au mbinu;
- Uhamaji;
- Kuwa na aina nyingi za shughuli; na
- Kushirikiana kuboresha utafutaji wa maji.

Kuhimili

Njia ambayo watu wanadai kuitumia kushughulikia kushuka kwa ubora na/au kiwango cha maliasili wanayoitegemea ni kukubali upungufu kama vile, upungufu wa mavuno, upungufu wa samaki, upungufu wa maziwa, n.k. Kwa watu wengi waliozoea kuishi kwa vitu kidogo, hii italeta shida kubwa – hasa kwa watoto wanaolazimika kuwa na upungufu wa kudumu iwapo watapata mlo duni/kutegemea maji machafu katika kipindi chao muhimu cha kukua.

3.1.4. Wanyamapori, wadudu waharibifu na maradhi

Wanyamapori

Washiriki wa utafiti katika maeneo yanayopakana na Hifadhi za Wanyamapori na Hifadhi za Taifa wameainisha wanyamapori kama tembo, mamba, na fisi kuwa ni tishio kubwa kwa ustawi wao. Hata hivyo, hata watu katika baadhi ya jamii nyingine za vijijini wameona kuwa ni tatizo kubwa.

Awali ya yote, watu walikuwa na wasiwasi kuhusu wao wenyewe na watoto wao kuuawa na wanyama pori wakubwa. Katika baadhi ya maeneo, watu walihisi kutishiwa kila walipokwenda kutafuta kuni, maji au huduma za mbali nje ya maeneo ya watu. Ingawaje watu wanaendelea na shughuli zao za lazima, wanahofu hasa kuhusu usalama wa watoto wao.

Wanyama wa hatari na waharibifu pia wanaathiri maisha ya watu. Wanafanya hivyo kwa:

- Kuua mifugo;
- Kuharibu mazao; na
- Kuwatisha watu wanaohudumia mashamba ya mbali au uvuvi nyakati fulani za mwaka.

Kila moja ya matokeo haya huathiri ustawi wa mali, hasa uhakika wa chakula wa kaya.

> Watoto wengi wanaoishi kitongoji cha Mihondo, Kijiji cha Ndogowe (Wilaya ya Dodoma vijijini) wameacha kusoma. Hii ni kutokana na kuogopa kukutana na wanyama pori wakali wakitembea kwa saa tatu au zaidi kwenda shule.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Watu wanaweza kuepuka hatari ya wanyamapori kwa kutoenda mahali wanakoishi, lakini hii itamaanisha kuepuka sehemu za kutafuta kuni, maji na kusafiri.

Wanyama wenye matatizo wanaweza kuwindwa na kuuawa kabla ya hawajasababisha madhara zaidi. Watu mara nyingi hawajui haki zao na kuhofu kuwa wataweza kufungwa iwapo wataua wanyama. Lakini sheria inaruhusu kuua wanyama waharibifu. Hata hivyo, msaada wa Serikali unahitajika kwa sababu wanakijiji hawana zana na mafunzo ya kuua kwa usalama wanyama wakubwa wa hatari.

Maradhi ya wadudu na maradhi ya mimea na mifugo

Wafugaji wanasema kuwa vimelea na aina nyingine za maradhi ya wanyama vinaongezeka. Baadhi ya sababu za ongezeko hili ni:

- Kupungua kwa uogeshaji;
- Matumizi ya dawa za kuulia wadudu zilizopunguzwa nguvu;
- Wadudu wanakuwa sugu kwa kemikali; na
- Kushindwa kuhamisha mifugo kwenye malisho yasiyoambukizwa kutokana na sheria na mfumo mpya wa umiliki wa ardhi.

> "Tangu kuondolewa kwa huduma za majosho ya umma, ni matajiri tu ndio wanaoweza kuwalinda ng'ombe wao kutokana na maradhi.
> Kwa mfano pampu ya kunyunyizia ni Tsh. 80,000, dawa ya kuulia wadudu ni ghali…ni matajiri tu ndio watamudu. Maskini hawawezi kulinda mifugo yao isiugue."
>
> - Mwanaume wa Kijiji cha Chakana, Wilaya ya Igunga

Familia za wakulima zimeeleza matatizo ya aina hiyo kutokana na ongezeko la wadudu waharibifu na maradhi ya mazao. Kwa mfano migomba katika Kijiji cha Makongora (Wilaya ya Muleba) hivi sasa inakufa kutokana na ugonjwa mpya wa kuvu ya "panama"; na mavuno ya mpunga yanapungua katika kijiji cha Kasanda (Wilaya ya Kibondo) kutokana na kuenea kwa ugonjwa mpya usiojulikana.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Wafugaji wanaweza kujaribu kuzuia maradhi kwa kuwachinja wanyama, kuwaogesha au kuwanyunyizia dawa, kuchoma nyasi mara kwa mara, kuepuka maeneo yaliyo hatarini zaidi (kama vile yenye mbung'o), na kuwahamishia wanyama katika malisho yasiyo na wadudu. Hata hivyo, mbinu hizi zina matatizo. Chanjo, kuogesha na kunyunyiza dawa ni ghali mno kwa wafugaji wengi, na taratibu mpya za umiliki wa ardhi husababisha kutotekelezeka kwa zile hatua nyingine.

Wakulima nao wana matatizo ya kugharamia dawa ghali kwa mazao yao. Hii husababisha dawa na kemikali kuongezewa maji ili kuwa nyingi. Kuna njia mbalimbali za kiasili za kuhifadhi mazao baada ya kuvunwa. Mara nyingi ni nafuu na hutumia vifaa vinavyopatikana katika eneo. Pamoja na nafuu hizo mbinu asilia hazitumiwi kama inavyotakiwa.

Wakulima na wafugaji wanakabiliwa na matatizo makuu mawili ya kukosa taarifa na fedha. Wakati mwingine hawajui la kufanya na wakati mwingine wanajua lakini hawamudu gharama.

4. MAREKEBISHO YA UCHUMI NA UATHIRIKAJI

Marekebisho ya uchumi mkubwa tangu katikati ya miaka ya 1980 yamebuniwa ili kuiwezesha nchi iwe katika njia ya maendeleo endelevu. Hii imehusisha kurekebisha na kuunda upya sekta mbalimbali za uchumi, hasa biashara na fedha.

Marekebisho yamefanikiwa kwa upande wa baadhi ya viashiria vya msingi kwa maendeleo ya uchumi. Kwa mfano kumekuwa na ongezeko la mazao ya kilimo, mapato ya kodi, pato la taifa na akiba ya fedha za kigeni. Pia mfumuko wa bei umepunguza.

Bahati mbaya, maendeleo kwa kiwango kikubwa hayakutafsiriwa wakati wote kuwa manufaa yanayoonekana katika ngazi ya jamii na kaya.

Marekebisho ya uchumi mkubwa yanajumuisha:

- Kurekebisha asasi ili taratibu na kanuni ziwe rahisi kufuata
- Kupunguza gharama za utendaji
- Kufungua zaidi biashara ya ndani na ya nje
- Kurudisha uimara wa fedha
- Kuimrarisha mauzo ya nje
- Kuongeza akiba ya ndani
- Kuwianisha viwango vya ubadilishanaji fedha za kigeni

Washiriki wa utafiti wameainisha mambo manne makuu yanayosababisha mishtuko na mifadhaiko ya uchumi ambayo yalikuwa yakiwaathiri watu maskini:

1. Kuondoa msaada wa serikali katika masoko na uzalishaji;
2. Mipango ya mikopo iliyotayarishwa vibaya;
3. Kupungua kwa fursa za ajira; na
4. Kupungua kwa upataji wa rasilimali ikiwemo ardhi.

Marekebisho yameleta bidhaa nyingi sokoni. Lakini wengi wetu tunazishangaa. Hatuna fedha za kuzinunua.

- Kijana mmoja wa Rufiji

Haya yanaelezwa pamoja na uchaguzi wa mbinu za kukabiliana na watakazotumia watu katika vipengele hivyo.



4.1. KUONDOA MSAADA WA SERIKALI KATIKA MASOKO NA UZALISHAJI

Kutokana na marekebisho ya uchumi mkubwa, serikali imeacha hatua kwa hatua kuendesha shughuli za uzalishaji na masoko. Hii imewaathiri watu katika maeneo makuu matatu:

1. Mabadiliko katika mfumo wa soko;
2. Kukosekana kwa udhibiti wa bei; na
3. Ukosefu wa huduma za ugani za kutosha.

Mabadiliko katika Mfumo wa Soko

Washiriki walionyesha kuwa mishtuko na mifadhaiko mingi ya uzalishaji wao na mapato imetokana na kujitoa kwa Serikali kutoka katika uzalishaji wa moja kwa moja na masoko. Shughuli hizo kwa sasa zimeelekezwa katika soko huria.

Mfumo wa masoko wa ushirika ulikwisha wakati Serikali ilipolegeza udhibiti wake katika uchumi. Pamoja na mambo mengine, hii imemaanisha kuwa bei ya pembejeo za kilimo, mazao na mifugo zimekuwa hazitabiriki. Bei za pembejeo kama vile mbolea za kemikali na dawa za kuulia wadudu zimepanda, lakini mazao yameshuka bei. Hii ina maana kuwa watu wenye rasilimali chache wako hatarini kuingia katika umaskini. Aidha kutokana na mabadiliko haya, uzalishaji umeshuka, na hivyo wakulima wanapata mapato kidogo na ustawi wa kaya zao unashuka.

> Mkulima wa pamba wa kijiji cha Nzanza (Wilaya ya Meatu) alipiga hesabu kuwa kama angetumia dawa za kuulia wadudu za kiwango kilichopendekezwa na kuuza mavuno kupitia chama cha ushirika, atapata hasara ya Tsh. 4,500 kwa eka.

Athari nyingine ya marekebisho haya ni kwamba wakulima wadogo wanashindwa kushindana na shughuli kubwa za kilimo na waagiza bidhaa wenye uwezo mkubwa. Kwa sasa kuna masoko machache ya kuaminika kwa mazao ya biashara na ya chakula, mifugo na bidhaa nyingine zitokanazo na kilimo. Wafanyabiashara wengi binafsi (wakiwemo madalali au watu wa kati) wanaweza kuingia katika mfumo mpya wa soko, ingawa hii haina maana ya kuwanufaisha wazalishaji wadogowadogo. Katika baadhi ya matukio, wazalishaji wadogowadogo wameathirika kwa sababu watu wa kati wanauza mazao ya wakulima na kuwapa sehemu ndogo tu ya faida. Inapotokea hivyo, ni watu wachache tu wanaonufaika lakini wakulima wadogowadogo wanakuwa maskini zaidi kuliko walivyokuwa awali.

MBINU ZA KUKABILI MISHTUKO NA MIFADHAIKO

Kuna njia kuu nne ambapo watu binafsi, kaya na jamii wanaweza kushughulikia mishtuko na mifadhaiko hii.

Kutafuta masoko yanayoweza kutoa bei nzuri	Hii ni rahisi iwapo watu wanaishi karibu na vituo vya biashara, ingawa itakuwa ghali kusafirisha mazao au mifugo. Ni matajiri tu watakaomudu njia hii.
Kutegemea watu wa kati (madalali)	Watu wa kati (madalali) wana taarifa nzuri kuhusu bei za sehemu mbalimbali na wana uhusiano na vituo vya biashara. Tatizo ni kwamba hawatoi bei nzuri, hasa kwa wakulima wadogo.
Kuhamasisha kupatikana kwa mifumo mizuri ya bei na masoko	Hii inahusu kufanya mawasiliano na viongozi wa ngazi ya juu serikalini. Huu ni mkakati wa muda mrefu na huenda usifae kila wakati.
Kubadilisha mazao au mifugo yenye thamani kubwa na rahisi kuuza	Wazo ni kuacha mazao ya biashara kama korosho, pamba na kahawa kwa ajili ya mazao ya chakula kama vile mahindi, muhogo n.k. Njia hii mara nyingi inahitaji maarifa mapya mengi na inaweza kuwa ghali kuanza.

Kukosekana kwa udhibiti wa bei

Wakati wa msimu wa mauzo ya korosha mwaka 2000/01 bei zilishuka kutoka Tsh. 800 kwa kilo mpaka Tsh. 250 tu. Hii ilifanyika bila kujali kuwa Bodi ya Korosho Tanzania imepanga bei ya Tsh. 540 kwa kilo.

Kwa kuwa udhibiti rasmi wa bei umeondolewa, bei zimepungua na hazitabiriki. Siku hizi, pamoja na kuwa na wateja wengi mbalimbali, wafanyabiashara binafsi bado wanaweza kupanga bei kwa kiwango cha chini kuliko kilichopendekezwa na serikali. Washiriki wengi wangependa kuona mfumo utakaosaidia kupunguza mishtuko na mifadhaiko hii kwa wakulima – vinginevyo watalazimika kuacha kilimo na watakabiliwa na umaskini.



Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna njia kuu tatu ambazo watu binafsi, kaya na jamii wanafanya kukabili mishtuko na mifadhaiko hii:

Kuchujua pembejeo	Mbolea ya kemikali au dawa ya kuulia wadudu zinaweza kuongezwa kuwa nyingi kwa kuchujuliwa na maji. Hata hivyo itamaanisha kwamba kazi yake itakuwa dhaifu, uzalishaji utabaki katika kiwango kidogo na wadudu na maradhi yatakuwa sugu. Huu ni mwitikio wa muda mfupi ambao utaifanya hali iwe mbaya zaidi baada ya muda mrefu.
Kutumia mbinu nafuu zaidi	Jamii nyingi zimeacha kuogesha mifugo badala yake wamekuwa wakiwanyunyizia dawa. Hii ni njia rahisi ya kudhibiti wadudu kwa muda mfupi lakini haijathibitishwa kufaa zaidi.
Kutumia vizuri mbinu za asili	Wakulima wanaweza kushinda matatizo ya rutuba ya udongo kwa kutumia mbinu asilia, kama vile kutumia samadi ya ng'ombe, uchanganyaji mazao, upandaji kwa zamu au kilimo cha kuhamahama. Lakini tatizo la ongezeko la watu na utaratibu mpya wa umiliki wa ardhi hufanya iwe vigumu kutumia mbinu hizo za kiasili.

Huduma chache za ugani

Sera za uchumi zimehimiza kupunguza matumizi ya serikali na kusimamisha ajira serikalini. Hii imesababisha kuwepo kwa huduma chache za kilimo za ugani. Miongoni mwa mambo mengine, hii ina maana kwamba wakulima wengi hawajanufaika na mbinu mpya na wanaendelea kutumia mbinu za zamani na hivyo kutoendelea. Aidha ina maana kwamba mifumo ya kilimo na mifugo haiwezi kumudu milipuko ya maradhi.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna njia kuu nne ambazo watu binafsi, kaya na jamii wanafanya kukabili mishtuko na mifadhaiko hii:

Watu wanabahatisha wenyewe	Wakulima na wafugaji wanajaribu madawa na dawa mbalimbali za kuulia wadudu mpaka wagundue inayofaa. Mara nyingi njia hii ni ghali, inayochelewesha na ya hatari.
Kupata ushauri kutoka mbali	Hii inahusisha kusafiri mpaka kwenye vituo vya kata, wilaya au mkoa ili kupata ushauri wanaouhitaji. Hii inatumia muda na fedha na watu huenda wasipate ushauri wanaouhitaji.
Kushawishi uimarishwaji wa huduma za ugani	Kuwashawishi viongozi na wanasiasa kuhakikisha kuwa wanaajiriwa wafanyakazi bora katika ngazi ya chini. Ni jamii zenye mipango mizuri ndizo zinaweza kufanikiwa katika hatua hii.
Kupata msaada kutoka vyama vya kiraia	Baadhi ya jamii zimenufaika kwa kuwa na Asasi zisizo za Serikali (AZISE) na Vyama vya Kiraia (VVK) vilivyosaidia kupata wataalam wa ugani wanaofaa. Lakini hii haitokei mahali pote.

4.2. Mipango ya mikopo iliyotayarishwa vibaya

Sera za uchumi kwa sekta ya fedha zinalenga kupatikana kwa huduma za mikopo kwa maeneo ya vijijini na mijini. Hata hivyo, sera hizo zimesababisha kubinafsishwa kwa asasi za mikopo na ukopeshaji (kama vile Benki ya Biashara ya Taifa na Benki ya CRDB). Hii, kama ilivyoelezwa na washiriki wa utafiti, imesababisha uhaba wa upatikanaji wa mikopo na viwango vikubwa vya riba, ambavyo kwa upande mwingine imezuia uwezo wa watu kukopa na kuwekeza.

Hata hivyo, serikali imeanzisha huduma ya mkopo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (MCDGC). Hii inaipa kila wilaya na manispaa Tsh. milioni 1 mpaka 1.5 ili kuwawezesha wanawake kupata mikopo ya gharama nafuu. Aidha Halmashauri za Wilaya pia zinaombwa kutenga asilimia 10 ya mapato yao kuwakopesha wanawake na vijana. Hata hivyo, kero zifuatazo zimetajwa kuhusu huduma hizo:

- Huduma nyingi hutumiwa vibaya, zina gharama kubwa za uendeshaji, na haziwafikii idadi kubwa ya walengwa;
- Riba za mkopo ni kubwa;
- Mamlaka chache za Serikali za Mitaa ndizo zilizofanikiwa kutenga asilimia 10 ya mapato yao kwa madhumuni haya; na
- Kuna matatizo ya urejeshaji mikopo kwa sababu taratibu ni ngumu kuzifuata.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna njia kuu tatu ambazo watu binafsi, kaya na jamii wanafanya kukabili mishtuko na mifadhaiko hii:

Kutumia akiba binafsi	Badala ya kukopa, watu wanachukua kutoka katika akiba zao za mauzo ya mifugo, mavuno yaliyopita au uvuvi. Hata hivyo, akiba hizi ni ndogo kutokana na uzalishaji mdogo.
Kutumia akiba ya kikundi	Wanawake mara nyingi wanatumia mipango ya akiba ya kikundi (inayojulikana kama *mchezo*). Hata hivyo kiasi kilichopo katika mipango hii ya kijamii na isiyo rasmi kinaweza kuwa kidogo sana na mikopo kukosekana wakati watu watakapohitaji.
Kukopa kutoka kwa ndugu na marafiki na kulipa vitu	Huu ni mfumo wa kawaida na unahusu mikopo midogo yenye masharti nafuu ya kulipa. Hata hivyo inategemea watu kuwa na ndugu au marafiki walio tayari kutoa mikopo inapohitajika.

4.3. Nafasi chache za ajira

Nafasi za ajira katika sekta ya umma zimepungua kutokana na kile kilichotajwa na washiriki wa utafiti kuwa ni upunguzaji wafanyakazi, kusitisha ajira na kuyauza makampuni ya umma kwa sekta binafsi. Haya ni matokeo ya marekebisho ya uchumi mkubwa. Hata hivyo, nafasi za ajira zimekuwepo katika sekta isiyo rasmi na ya binafsi, lakini si za kutosha kulingana na idadi ya watu wanaotafuta ajira. Hii ni kwa sababu mahitaji ya ajira yameongezeka sana.

Ongezeko hili la mahitaji ni matokeo ya watu wengi kukimbilia mijini kutoka vijijini kutafuta ajira hasa kwa vijana. Wengi wao wamekimbilia mijini na hivyo kusababisha msongamano na ongezeko la ukosefu wa ajira mijini. Vijana wengi wanatumbukia katika uhalifu, ulevi, umalaya na maisha yasiyo na msimamo na kusababisha ugumu wa maisha. Kutokana na hali hiyo mifumo ya misaada ya asili kati ya jamii ya mijini na ile vijijini imekufa.

Kama njia mbadala ya kupata ajira, watu wameanzisha biashara katika sekta isiyo rasmi katika maeneo ya mijini. Hata hivyo, wanajihisi hawako salama kwa sababu kuna sheria ndogo zinazofanya shughuli kama hizo zisiwe halali katika baadhi ya maeneo. Wafanyabiashara ndogondogo wanalalamikia kusumbuliwa na maofisa wanaowafanya wakimbie na kuacha biashara zao ziibiwe na wezi wa mitaani.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna njia kuu tatu ambazo watu binafsi, kaya na jamii wanafanya kukabili mishtuko na mifadhaiko hii:

Kuanzisha shughuli binafsi	Watu wasiopata ajira ya kuwafanyia wengine kazi waanzishe shughuli zao, kwa mfano useremala, ushonaji, ulimaji bustani za mboga mjini au kuuza chakula. Hata hivyo, shughuli hizo zote zinahitaji ustadi na mtaji ili kuanza kuzitekeleza.
Kujiunga na mafunzo na programu za namna ya kuanzisha biashara	Katika nyakati hizi za mabadiliko ya haraka watu wanahitaji mafunzo maalumu ili kujiandaa kuendesha maisha katika soko la sasa la ajira. Kunahitajika programu nyingi za namna hii.
Kujiingiza katika shughuli zisizo halali	Baadhi ya watu waliokata tamaa wanafanya shughuli zisizo halali kama vile kuiba na biashara ya ngono.

4.4. Kupungua kwa upataji wa rasilimali ikiwemo ardhi

Maisha ya watu yanategemea sana rasilimali wanazozitumia. Kati ya rasilimali muhimu ni pamoja ardhi, mifugo, zana, vifaa na upataji teknolojia. Watu wanapokosa rasilimali za kutumia kuendeshea maisha, wanaongezekewa na hatari ya kutumbukia katika umaskini.

Hivi sasa Serikali haidhibiti tena bei za teknolojia na zana na vifaa vya kisasa, kwa hiyo ni ghali sana kwa watu kumudu. Watu wanaamua kutumia vifaa hafifu kama vile majembe madogo ya mkono na mitumbwi ya asili, na kuwasababisha wasizalishe kiasi cha kutosha kwa ajili ya kaya zao.

Kutokana na kushindwa huku kupata rasilimali mpya, watu wengi wanaweza tu kumudu mashamba madogo.

Ardhi ni moja ya rasilimali muhimu sana. Kutokana na marekebisho ya uchumi, njia za kupata na kumiliki ardhi zimebadilika sana tangu miaka ya 1990. Matokeo yake, hata ardhi ya vijijini imekuwa na soko kwa hiyo inanunuliwa na kuuzwa kama bidhaa sokoni. Ardhi inayouzwa ya biashara huwa ni ghali sana kwa watu maskini kumudu kununua. Mfumo wa asili wa urithi wa ardhi haufanyikazi vizuri tena, kwa hiyo watu wanahitaji fedha nyingi kununulia ardhi. Aidha ardhi inazidiwa na ongezeko kubwa la watu.

> Kukosa ardhi ni sawa na kuishi kama mhamiaji. Kama utashindwa kununua ardhi, utalazimika kupanga vyumba kuliko kujenga nyumba yako.
>
> - Kibarua katika Kijiji cha Misufini (Wilaya ya Same)

Washiriki wameona kuwa uhusiano wa madaraka kati ya watu unaathari kwa namna rasilimali zinavyodhibitiwa na kutumiwa. Umri na jinsia hushawishi upataji na usambazaji wa rasilimali.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna njia kuu tatu ambazo watu binafsi, kaya na jamii wanafanya kukabili mishtuko na mifadhaiko hii:

Kukodi nyenzo za kufanyia kazi	Hii ni njia nzuri lakini si kila mtu anaweza akamudu.
Kununua nyenzo za kufanyia kazi za zamani	Hii inafaa kama hatua ya muda mfupi, lakini vifaa vya zamani havidumu kwa muda mrefu na lazima vibadilishwe.
Kuuza nguvu zako upate fedha ya kununua nyenzo za kufanyia kazi	Watu wenye afya njema mara nyingi wanatumia nguvu zao kama rasilimali. Wakati mwingine vijana walioko vijijini wanafanya kazi kama vibarua kwenye mashamba ili kupata fedha za kununua vifaa.
Kugawa upya ardhi kwa wale wanaohitaji sana	Serikali chache za vijiji zimetumia njia hii. Ni wazo zuri lakini inahitaji dhamiri ya kisiasa ambayo mara nyingi haipo. Jamii lazima zijiandae vizuri ili kuleta mabadiliko ya mwenendo uliopo.

5. UTAWALA NA UATHIRIKAJI

Baadhi ya wanajamii waliochangia katika TzPPA walikuwa na mawazo kuwa serikali kwa kiasi fulani ilikuwa inajaribu na kupanua shughuli zake. Hata hivyo, wakati wa utafiti, washiriki hao walionyesha kuwa na wasiwasi. Ubora wa shughuli za serikali utahitajika zaidi hasa kuhusu:

- Utozaji kodi;
- Udhibiti wa rushwa;
- Huduma za jamii za kutosha na nzuri; na
- Uwazi na uwajibikaji.



5.1. UTOZAJI KODI

Serikali inakusanya fedha kutokana na ada za huduma, ushuru, na kodi. Kutokana na *mapato* haya, Serikali inagharimia shughuli mbalimbali – kama vile uboreshaji wa miundo mbinu na kutoa huduma za jamii.

Sehemu ya watu walioshiriki katika TzPPA walifikiri kuwa kazi iliyokuwa ikifanywa na serikali ilifanywa kwa kiwango cha kuridhisha na kwa kiasi fulani wameelewa nia ya serikali kuwa na mapato yake.

Hata hivyo, hawakuridhishwa na *wingi* wa kodi zinazotozwa, *namna* zinavyotozwa na *wakati* zinapotozwa.

Hatua za kodi za kuwasaidia maskini:

- Kuondoa kodi katika pembejeo za kilimo
- Kuondoa kodi kwa dawa na vifaa vya kuokoa maisha
- Kuondoa kodi nyingine mbalimbali katika sekta ya kilimo
- Kuondoa VAT kwa uwekezaji unaohusu elimu

Kwa mujibu wa wanajamii, idadi ya ada, ushuru na kodi zinazotozwa na serikali ni nyingi mno. Zimewatia umaskini watu moja kwa moja na kuwa vikwazo vya kuingia katika uchumi wa soko huria. Wakati kodi husika si kubwa, lakini tatizo linakuja pale zinapojumlishwa na kuwa nyingi mno kiasi cha maskini kuona ni mzigo mkubwa kulipa.

Ni vigumu kulipa hasa wakati ukusanyaji mapato haulingani na nyakati watu wanapokuwa na fedha. Kwa mfano, kaya nyingi zinaishiwa na fedha miezi michache tu kabla ya mavuno mapya; na watu wengi hawana fedha za kulipia leseni/ada za biashara na kodi kabla ya kuanza biashara ndogo za duka n.k. Kwa hali zote, washiriki wa utafiti wameonyesha kuwa mamlaka zinahitaji kubadili muda wa ukusanyaji wa mapato ili watu wasije wakalazimika kuuza akiba ya chakula au rasilimali nyingine.

Watu wanapokosa fedha za kulipa kodi zao, baadhi ya wakusanyaji huamua kutumia nguvu. Ushahidi ufuatao unatoa mfano halisi wa maisha ya namna matokeo yanavyoweza kuwa mabaya:

"Nimelipa kodi yangu ya maendeleo na kuomba nilipe kodi ya mke wangu baada ya kuuza mbuzi wangu katika mnada wa mifugo wa kijiji. Usiku uleule, wana mgambo walikuja nyumbani kwetu na kuvunja mlango wetu wakati mabinti wetu wawili na sisi wenyewe tumelala. Walianza kutupiga na kututaka tuonyeshe risiti ya kodi. Baada ya kuona yangu walitaka ya mke wangu. Niliwaeleza kuwa nilishaeleza suala hilo kwa viongozi wa kijiji. Hata hivyo, walisisitiza kuona risiti yake na kutaka atoke awafuate (ulikuwa usiku wa manene). Alikubali na kwenda kuwafunika mablanketi watoto wetu wawili na kuwataka wasilie. Mwanamgambo mmoja alirudi, kumkamata kwa nguvu na kumfunga mikono yake nyuma na kumpiga. Baadhi ya nguo zake zilianguka na kubaki na kipande cha nguo kifuani. Niliwafuata wanamgambo kwa mbali wakati wamemchukua mke wangu na watu wengine waliowakamata kutoka nyumba nyingine. Hii iliendelea mpaka saa 10 alfajiri wakati walipoanza safari ya kuelekea kwenye ofisi za Kata.

Kwa kuwa sikuwa na la kufanya, nilirudi nyumbani na kuchukua mbuzi wangu wote wanne kwa marafiki, ambao baada ya kujua kuwa nilikuwa na tatizo kubwa walinipa fedha kidogo sana, k.v. Tsh. 5,000 kwa mbuzi. Saa 4.45 asubuhi nilifika katika Ofisi za Kata na kuambiwa lazima nilipie gharama za mgambo; chumba alichofungwa mke wangu, kodi yake ya maendeleo na faini. Nililipa jumla Tsh.15,000. Baada ya hapo, walimtoa mke wangu – nilikuwa na wasiwasi sana kuwa walimfanya nini. Niliogopa zaidi baada ya kufikiria VVU/UKIMWI. Hivi sasa nina wasiwasi sana, tangu nilipouza mbuzi wangu mwaka jana, sina fedha za kununua mbolea kwa ajili ya shamba langu. Sijui mwaka huu nitafanya nini."

Matukio kama haya yanaweza kuleta matokeo mabaya kwa mali za watu, ustawi wa mwili na akili. Pia hujenga hofu na kutowaamini viongozi wa mtaa. Ni kutokana na malalamiko ya watu kama haya ndipo Serikali hivi karibuni ilipoamua kupunguza idadi kubwa ya kodi wanazolipa watu na kurekebisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato. Huu ni mwanzo unaotia moyo, na huenda utaleta mabadiliko mazuri kwa maisha ya watu. Sasa ni lazima tuhakikishe kuwa mabadiliko haya yanatekelezwa na hatua zinazofaa kuchukuliwa iwapo hayatekelezwi. Hasa, tunasubiri kuona iwapo:

- Maagizo ya kukataza matumizi ya nguvu/ukusanyaji kwa nguvu yatazingatiwa; na
- Kodi mpya (zilizo rasmi na zisizo rasmi) zitajitokeza kufidia zile zilizofutwa.

Uwezekano huu halisi hauna budi kufuatiliwa na kuzuiwa. Pengine moja ya njia muhimu zaidi, mtu anazoweza kufikiria kutokana na hoja zilizotolewa na washiriki wa utafiti, ili kuhakikisha kuwa mabadiliko yenye manufaa yanabaki ni kuelimisha umma – pamoja na viongozi – kuhusu nini wanachotakiwa watu kulipa na namna mfumo wa ukusanyaji unavyotakiwa kufanywa.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna njia kuu tatu ambazo watu binafsi, kaya na jamii wanafanya kukabili kodi, ushuru na ada zinazoongeza umaskini. Njia hizi ni:

Kulikimbia tatizo	Hatua hii inapunguza uzalishaji wa eneo na kufanya maisha kuwa magumu kwa watu wasio na uwezo katika kaya ambao wanaachwa nyumbani.
Kushughulikia tatizo kwa kuwahonga maofisa	Hatua hii huwafanya watu washiriki katika tendo lisilo halali, na kuwahusisha wakusanya kodi fulani tu wanaorudi kufuata malipo zaidi. Matokeo yake, watu mara nyingi wanaishia kulipa zaidi ya kodi halisi.
Kushawishi mabadiliko	Hii inahusisha kuwalalamikia viongozi wa umma waziwazi na wakati mwingine kufunga shughuli za biashara na kuandamana barabarani. Hii itategemea iwapo wananchi wamejiandaa vizuri na viongozi wa umma kuhusu athari ya vitendo hivyo. Hata hivyo, itasaidia kuwachukulia hatua viongozi, na wakati mwingine imesababsiha mabadiliko mazuri katika mfumo wa ukusanyaji kodi.

5.2. Huduma na Uongozi duni

Washiriki wa utafiti wamekubali kuwa kukosekana au uduni wa huduma (kama vile maji, umeme, barabara, walimu, na polisi) katika ngazi ya vijiji huchangia sana umaskini. Hali hii ina athari katika ustawi wa watu, kuathiri uwezo wao wa kuwa na afya bora, kupata elimu bora na inayofaa na kupata masoko.

Kushindwa kwa viongozi wa eneo kushughulikia matatizo ya wananchi au malalamiko nako huleta athari mbaya. Kwa mfano kukosa uwajibikaji na/au kushindwa kuwashtaki watu kama vile viongozi wa vijiji wenye kiburi, walimu watoro, watumishi wa afya na polisi wazembe mara nyingi wameweka maisha ya watu hatarini (km. wagonjwa) au kuwasababishia kunyanyaswa (km. watoto wa shule). Washiriki wa utafiti wameonyesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha uzembe, bila shaka ni kutokana na mmomonyoko wa maadili au viwango vya kazi. Mara nyingi, viongozi walikuwa hawachukuliwi hatua hata kama malalamiko yaliwasilishwa ngazi za juu. Katika baadhi ya jamii watoto walilalamikia walimu waliofika shule wamelewa lakini hakuna hatua iliyochukuliwa dhidi yao. Matatizo haya, yakichanganywa na rushwa, husababisha upataji wa huduma za jamii kuwa mgumu hasa kwa maskini.

Hali kama hizo wakati mwingine husababisha matokeo mabaya. Washiriki wengi walikuwa na wasiwasi kuwa lazima hatua ichukuliwe haraka ili kuboresha mifumo ya kupima uwajibikaji na kuongeza huduma.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna njia kuu tatu ambazo watu binafsi, kaya na jamii wanafanya ili kukabili mishtuko na mifadhaiko:

Kuwatumia watoa huduma wengine	Wakati huduma za afya za serikali si nzuri, watu ama wanakwenda kwa waganga wa jadi au hospitali binafsi. Kutumia waganga wa jadi ni nafuu na wapo wengi katika jamii nyingi. Tatizo ni kwamba ubora wa tiba yao hauaminiki. Huduma binafsi mara nyingi ni ghali kwa watu maskini kuweza kumudu.
Kuwawajibisha viongozi wa eneo	Viongozi wa eneo watawajibishwa ama rasmi kwa vikao halali au isivyo rasmi kutokana na tabia zao mbaya kwa kuwaita majina mabaya ya kuchafua heshima yao. Tatizo la hatua hii ni kwamba viongozi wa kijiji wanaweza kuacha kuitisha mikutano ya hadhara ili kuepuka maoni ya wananchi. Wakati mwingine, viongozi wanatumia wanamgambo kuwatisha wale watakaothubutu kusema.
Kukata rufaa ngazi za juu	Jamii lazima zijiandae vizuri ili kudhibiti hatua hii ingawa inaweza kufaa. Kwa mfano, ni kutokana na shinikizo la wanakijiji wa Twatwata mwaka 1995 ndipo Mkuu wa Mkoa alipoanzisha "Operesheni Makamba". Hii ilisaidia kuleta ubora wa huduma za msingi katika Wilaya ya Kilosa.

5.3. Usalama, Sheria na Utaratibu

Watu wanaona udumishaji wa sheria na utaratibu ni jukumu la serikali. Ndio maana wanaona ongezeko la viwango vya uhalifu na fujo kama suala la utawala kuliko kuwa la kijamii. Washiriki wa TzPPA wamehitimisha kuwa vitendo vya uhalifu na fujo vimechangia sana upotevu wa mali, ustawi wa mwili na jamii. Tatizo ni kubwa sana katika maeneo ya mijini na kwa wanawake, watoto, wazee na watu wenye matatizo ya akili na ulemavu mwingine.

Pia uhalifu unazuia ukuaji wa shughuli za uchumi za jamii. Kwa mfano, iliarifiwa na Maofisa Uvuvi wa Wilaya ya Kigoma vijijini kuwa athari ya wizi katika kijiji cha Mwakizega imekuwa kubwa kiasi cha kuathiri sekta ya uvuvi mpaka kufikia Mei 2002 na kupunguza hadi asilimia 20 ya kiasi kilichokuwepo mwaka 2001. Ofisa Uvuvi wa Kata alitoa ripoti ifuatayo:

Kati ya 1998 na 2002 zaidi ya nyavu 46 za kuvulia ziliibiwa kutoka eneo la kijiji; baadhi ya wizi ulihusu utekaji nyara na madhara ya mwili ya wavuvi. Wimbi hili la wizi wa kutumia silaha lilisababisha wavuvi 38 wa nyavu kuhamishia rasilimali zao Ziwa Viktoria ambako uvuvi wao ni salama zaidi. Hadi Mei 2002, ni vikundi 13 tu vya uvuvi wa nyavu vilibaki Mwakizega [kiasi cha asilimia 30 ya wavuvi kabla ya kuongezeka kwa wizi].

Uhalifu umesababisha watu wasijione salama, na kuathiri uhuru wa watu wa kutembea, kwa kuwa watu wana wasiwasi wa kufanya shughuli za uzalishaji zitakazowakaribisha wezi au kuwafanya wawe waathirika wa baadhi ya uhalifu.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Mwitikio kuhusu ukiukaji wa sheria na utaratibu, kama ilivyoonekana katika majadiliano ya washiriki wa utafiti; hutofautiana. Tofauti hutegemea aina ya uhalifu, uwezo wa mtu kujilinda, kiwango cha utaratibu wa kijamii katika ngazi ya jamii, na aina ya msaada unaopatikana kutoka mamlaka ya eneo. Kuna aina kuu tatu za mwitikio:

Kujihami	Watu walio hatarini zaidi (wazee, walemavu n.k.) wanaweza kuwaita "walinzi wa familia" kuwalinda. Hawa ni marafiki wenye uwezo na wanafamilia wanaokuwa hapo. Hii ni sehemu ya mtaji wa jamii. Katika maeneo mengine kuna vikundi vya ulinzi wa jadi vinavyoundwa kwa muda au kuwa vya kudumu. Mifano inajumuisha walinzi wa jadi (sungusungu) katika kijiji cha Nchenje au Limurani ili kulinda wizi wa mifugo miongoni mwa jamii za wafugaji. Lakini vikundi hivi vya kudumisha amani katika jamii vinaweza kuwa na matatizo. Vinaweza kuchukua hatua ambazo ni zaidi ya majukumu yao rasmi ya kuwalinda watu na kuruhusu kuendekeza maslahi binafsi. Hii inaweza kusababisha madhara na ukiukaji wa haki za binadamu.
Kuhama	Watu wanapokabiliwa na uhalifu au ugomvi wanaweza kuhama kwa muda au moja kwa moja. Hii ni hatua kali na mara nyingi ghali kwa kuwa inachukua muda na juhudi kujiandaa na kuwasiliana na eneo jipya.
Kushirikiana na viongozi wa eneo	Watu wanaweza kushirikiana na viongozi wa serikali ya mtaa na asasi ili kusaidia kujenga asasi zisizo na upendeleo na zinazofaa kama vile Vituo vya Polisi katika maeneo muhimu na mahakama zinazoweza kushughulikia matukio zaidi.

Hatua hizi na nyingine – hasa zinapochukuliwa kwa njia ya mazungumzo kati ya polisi, Serikali za Mitaa na watu wanaotarajia kuwahudumia – zinaweza kuboresha usalama wa watu. Hatua hizo zinaweza kuwa hazitoshi kukabili matatizo maalumu wanayopata watoto (hasa wasichana), wanawake, watu wenye ulemavu na wazee. Kwa hiyo ni muhimu kutambua mahitaji ya vikundi hivi vya jamii, kuyaelewa vizuri na kuyatafutia ufumbuzi.

5.4. Sera zisizofaa

Washiriki wa TzPPA waliona kuwa watu wa kawaida hawashirikishwi ipasavyo wakati wa kupanga sera na kanuni za msingi zinazowagusa watu na maisha yao. Watu wameamini kuwa hii ndiyo sababu kuu kwa nini sera nyingi "zinazotoka juu kwenda chini" hazilingani kabisa na hali halisi ya matakwa ya ngazi za chini na kwa nini zimekuwa zikiwanufaisha wenye uwezo zaidi kuliko maskini.

Wanajamii wamekuwa wakikerwa sana na sera na kanuni za kutoka juu kwenda chini zinazotawala usimamizi na upatikanaji wa maliasili. Kwa mfano Sera ya Uvuvi ya 1970 iliweka kanuni ya upigaji marufuku wa jumla wa baadhi ya zana za uvuvi. Kwa mujibu wa wavuvi, sera hii imeshindwa kuzingatia hali halisi ya mazingira mbalimbali ya maji ya ziwa. Mbinu shirikishi kwa ajili ya usimamizi wa maliasili – na utungaji sera kwa ujumla – huenda zikagusa mazingira tofauti na kushirikisha katika sera watakazozikubali watu kuliko kujaribu kuzunguka.

MBINU ZA KUKABILI MISHTUKO NA MIFADHAIKO

Kuna njia kuu nne ambazo watu binafsi, kaya na jamii hujaribu kushughulikia sera wanazoona kuwa zinachangia umaskini wao, nazo ni:

Kuondoka katika eneo (kuhamahama)	Hii ni hatua ya mwisho na ghali sana kuitekeleza.
Kupuuzia sera	Kuna matukio mengi ya wanajamii kujaribu kupuuza au kuhujumu maamuzi yaliyotolewa katika ngazi ya kijiji, kata na hata wilaya. Maamuzi haya kwa kawaida yanahusu ugawaji wa rasilimali pale watu wanapohisi kuwa watazipoteza rasilimali hizo. Katika hali hii viongozi wanakuwa na tabia ya kuhimiza maamuzi yao. Hii husababisha msuguano na wakati mwingine, hata kuleta ugomvi.
Kutumia asasi nyingine	Wakati watu hawaridhiki na maamuzi kutoka asasi au chama kimoja, wanaweza kujaribu nyingine zinazokubaliana na maoni yao. • Katika ngazi ya jamii, kutakuwa na asasi za asili zinazoweza kufanya maamuzi kuhusu masuala ya jamii ingawa hayatakuwa mazuri kushughulikia masuala makubwa ya siasa; • Watu wanaweza pia kuwafuata viongozi wa siasa au watawala katika ngazi mbalimbali za serikali za mitaa kadiri itakavyofaa; na • AZISE na VVK vinavyofanya kazi katika eneo pia vinaweza kuwasaidia wananchi wasikike sauti zao.
Kuinua sauti za wananchi	Wananchi wa kawaida wanahitaji kuhusishwa katika hatua za awali za utayarishaji sera ili sera zitungwe kwa njia isiyowaletea madhara. Hii ina maana kwamba wananchi wa kawaida wanahitaji kuwa na madaraka na sauti. Hali hii inagusa ngazi zote kuanzia taifa, na eneo hasa wanaposhughulika na mabenki, wakopeshaji, wenye mashamba, waajiri na mamlaka za masoko. Ni vyema kuzingatia kuwa sera za serikali za hivi karibuni zinapendekeza kuwa ubia huu utaundwa katika ngazi zote za jamii. Ubia huu utaundwa na wawakilishi wa serikali, sekta binafsi, wabia wa maendeleo, na wananchi.





5.5. RUSHWA

Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania wa hivi karibuni unakubali na kutoa kipaumbele haja ya utawala bora. Juhudi zilizofanywa zinalenga:

- Kupunguza tabia zinazoelekea kuleta au kuendeleza rushwa;
- Kuleta ubora na usimamizi wa fedha za umma na uwajibikaji; na
- Kuimarisha mfumo wa mahakama.

Mambo haya ni muhimu ingawa si vipaumbele vya watu katika ngazi ya kijiji. Washiriki wengi wa utafiti wanaamini kuwa ubadhirifu mkubwa na wa upendeleo wa kisiasa vinafanyika. Wanakasirishwa na hali hiyo kwa sababu wanaona kuwa ni kuharibu mustakabali wao na wa taifa kwa ujumla. Wanatamani kukomesha aina zote za rushwa ndogo zinazoathiri moja kwa moja ustawi wao. Hasa, watu wanataka kukomeshwa kwa hongo kama sharti la awali la:

> "Hospitalini, mahakamani, kituo cha polisi, wote wanataka rushwa kabla ya kukuhudumia."
> - Mtu wa Kijiji cha Wabada (Wilaya ya Muheza)

- Kupata huduma za muhimu, hasa afya;
- Kupata rasilimali za uzalishaji, hasa ardhi;
- Kupata haki katika mahakama za kiraia Tanzania;
- Kupata uhuru wanapokamatwa na Polisi; na
- Kuendesha biashara.

Mara nyingi kutoa hongo ni ghali. Ni mzigo wa kifedha na huathiri mali na ustawi wa mwili wa watu na kuwanyima haki zao za msingi. Unyanyasaji unaofanywa na viongozi wala rushwa pia huwafanya watu wajihisi kuwa hawana madaraka na kukosa usalama na matumaini. Wanajamii walioshiriki katika TzPPA walikerwa zaidi kuhusu rushwa miongoni mwa Polisi na watoa huduma za afya ya msingi. Haya ni makundi mawili ya watu yenye madaraka yasiyo ya kawaida kwa maisha ya wengine. Kama ilivyojumuishwa na kijiji cha Mkongo Kaskazini (Wilaya ya Rufiji).

Polisi hawatoi msaada wowote! Unapotoa taarifa ya wizi, watakusaidia tu iwapo una fedha za kuwalipa.

Hadithi kama hizo zinasemwa kuhusu watoa huduma za afya. Kwa mfano katika kijiji cha Twatwata (Wilaya ya Kilosa), wanawake walieleza kuwa inagharimu Tsh. 2,000 kupata huduma ya afya katika kituo kimoja cha afya kilichopo umbali wa kilometa 18 kutoka Kimamba. Baada ya gharama za usafiri, wanalipa Tsh. 1,500 kujiandikisha, na mara kwa mara huombwa hongo kabla ya kuhudumiwa. Wakati mshiriki mmoja wa utafiti alipokataa kutoa rushwa, alikemewa kuwa, "Kama hutaki kulipa, rudi nyumbani."

Kwa hiyo washiriki wamesema, "Iwapo una Tsh. 10,000, utapata huduma, lakini usitegemee kula. Iwapo una chini ya Tsh. 10,000 ni afadhali usipoteze muda wako kwenda". Badala yake, wanawake wanasafiri hadi hospitali ya Wilaya ya Kilosa au Morogoro. Hospitali hizi ingawa hazihitaji sana rushwa lakini unahitaji muda zaidi na fedha kufika huko.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kutokana na ushamiri wa matatizo haya washiriki wa utafiti wamesema hatua za kupambana na rushwa hazifai. Kujua kwa nini na kutafuta ufumbuzi havina budi kufanywa kwa utafiti shirikishi ili matokeo yaonyeshe hali halisi ya vijijini. Wakati huo huo, kuna njia kuu tatu ambazo watu binafsi, kaya na jamii zinashughulikia rushwa.

Kutoa taarifa kwa mamlaka husika	Washiriki wengi wamelaani matumizi mabaya ya fedha za umma kuwa inaelekea kuwa mbaya zaidi kama hongo, ingawa mara nyingi inakuwa vigumu kukusanya ushahidi unaotakiwa kutoa malalamiko yanayofaa. Watu hawana uhakika wa mtu wa kumlalamikia. Pia kuna hatari kwa wale watakaolalamika wataathiriwa.
Kuchukua hatua ya pamoja	Iwapo vitendo vya rushwa ni vikubwa, watu wanaweza kukutana na kumkataa na kumlaani ofisa anayehusika. Hii inaweza kuwa wakati wa mkutano wa hadhara au nyakati za uchaguzi.
Kutafuta namna ya kutayarisha malalamiko rasmi	Watu wanahitaji kujua kuna kanuni zipi ili wajue rushwa inatokea wakati gani na namna ya kukusanya ushahidi ili wathibitishe. Aidha wanahitaji kujielimisha namna ya kutayarisha malalamiko rasmi.

6. AFYA, VVU/UKIMWI NA UATHIRIKAJI

Sura hii inaanza kwa kuzingatia uhusiano uliopo kati ya kuugua na uathirikaji. Neno kuugua linajumuisha maradhi, ulemavu, utapiamlo na maumivu. Kwa hiyo kuna kupitia vipengele vitatu vinavyochangia katika mishtuko na mifadhaiko mikuu inayohusiana na afya: hali ya mwili kuugua, unyanyapazi, kutengwa na VVU/UKIMWI.



Neno kuugua linajumuisha maradhi, ulemavu, utapiamlo na maumivu. Aina hizi mbalimbali za kuugua zinaweza kuwa na matokeo ya msingi na ya baadaye. Matokeo ya msingi yanahusika moja kwa moja na kuugua na humwathiri mtu mgonjwa (yaani, aina mbalimbali za kuugua na wakati mwingine unyanyapazi). Matokeo ya baadaye ni matokeo ya namna mtu, kaya au jamii wanavyoshughulikia ugonjwa wa wenzao (yaani, kuhusu muda na gharama zinazohitajika kutoa huduma na matibabu). Matokeo haya hutoa mambo matatu makuu:

Uzoefu wa mtu kuhusu ugonjwa ni matokeo ya hali ya kijamii na kimwili	Hii ina maana kwamba wakati baadhi ya matokeo ni ya lazima (k.v. kupoteza ustawi wa mwili) mengine si hivyo (k.v. unyanyapazi).
Maradhi, ulemavu, utapiamlo na maumivu huathiri watu wengi kuliko mwathirika mkuu	Maradhi yanaweza kuwa matokeo mabaya kwa wahudumu na wategemezi. Kuugua kunaweza kudhoofisha ustawi wa jamii na hata taifa.
Ugonjwa una athari za muda mfupi na mrefu	Watu binafsi, kaya au jamii wanaweza kupona kutokana na maradhi, lakini si kutokana na matokeo yake. Kwa mfano wanapokuwa wametumia rasilimali zao zote kulipia matibabu na kutumbukia katika mtego wa umaskini.

6.1. Kuwa na Afya Mbaya

Kuna mambo matatu makuu yanayosababisha mtu awe na afya mbaya:

- Maradhi, ulemavu na utapiamlo;
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya; na
- Maumivu ya ajali au ajali za kazini.

Kuumwa na viungo, maumivu na dalili nyingine zinazohusiana na aina hizi mbalimbali za ugonjwa havifurahishi. Lakini vinahusiana na msongo au mfadhaiko kwa mgonjwa na kwa wanaowatunza na kuishi nao. Hii ni kwa sababu maradhi huathiri ustawi wa mgonjwa na familia yake, marafiki na pengine jamii yao.

Muda wa maradhi unaleta mabadiliko. Iwapo maradhi yanakuja wakati muhimu katika msimu wa kilimo, ina maana mavuno au upandaji vitaathirika. Matokeo ya ugonjwa kwa watu wasio walemavu ambao mara nyingi ni watoaji huduma ni mabaya zaidi wakati yanapompata mtoto au mzee.

Kanuni hiyo hiyo inatumika kwa mitandao mipana ya kijamii. Iwapo mwanasiasa muhimu anaugua, ofisa au mtu anayehusika na masoko, basi itaathiri vibaya jamii yote. Inaweza kuharibu uwezo wa jamii kujipanga na inaweza kupunguza sana uwezo wa kisiasa.

Kwa kuangalia suala la afya, hali ya kiafya ya kutisha inadhaniwa kuwa muhimu zaidi kuliko utapiamlo, maradhi sugu kama vile pumu na shinikizo la juu la damu au ulemavu. Bila shaka na athari za kipindupindu ni mbaya zaidi ya kisukari. Hata hivyo, kwa upande wa umaskini, ugonjwa wa muda mrefu wenye uzito mdogo unaweza kuleta uharibifu mkubwa. Maradhi haya huenda yasitibiwe kwa muda mrefu kwa sababu hakuna dalili za wazi zinazoonyesha kuwa mtu huyo mgonjwa. Hata hivyo, kadiri mtu anavyozeeka, huanza kuonyesha dalili za kimaumbile. Katika hatua hiyo, ugonjwa unakuwa mkali zaidi na afya ya mtu inaathiriwa kabisa. Wakati huo mtu analazimika kutumia fedha nyingi kwa matibabu ghali, na hivyo kuwalazimisha kuuza rasilimali wanazotumia kuendeshea maisha. Pia wanakuwa wagonjwa sana kiasi cha kutomudu kazi.

Ulemavu:

Kiasi cha watu 3,456,000 (asilimia 10 ya idadi ya watu) ni walemavu. Kati yao, 28% walemavu wa viungo; 27% macho; 20% viziwi; 8% wana ulemavu wa akili; 4% mchanganyiko; na 13% wanaishi na ulemavu mwingine.

Ulemavu huu unaweza kuwa ni matokeo ya maradhi ya kuzaliwa na hitilafu, maradhi yasiyoambukiza, maradhi yanayoambukiza, utapiamlo, majeraha na ajali, maradhi ya akili, na matumizi ya ulevi au dawa za kulevya.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Mishtuko na mifadhaiko inayosababishwa na hali mbaya ya afya, haina ufumbuzi mwepesi. Tusimfikirie mgonjwa kwa muda mfupi tu, bali matokeo mengine yote yanajitokeza kwa muda mrefu. Sehemu zifuatazo zinaangalia uchaguzi wa mwitikio kwa upande wa kinga, kupunguza kasi na kuhimili.

Kinga

1. Hatua za kinga mara nyingi zinagharimu fedha kwa hiyo maskini hawatakuwa na uwezo wa kuzitumia na ndio walio hatarini zaidi kuambukizwa.
2. Kampeni za kutoa Elimu, Taarifa na Mawasiliano zinafaa lakini hazina budi kuhusishwa na namna watu wanavyoweza kutumia elimu yao kwa vitendo. Pamoja na mambo mengine, hii ina maana ya kuhakikisha kuwa dawa ni nafuu na zinapatikana.
3. Ufumbuzi lazima uwe unaoweza kutekeleza katika ngazi ya eneo. Kwa mfano, katika kijiji cha uvuvi cha Mchinga II (Wilaya ya Lindi vijijini), vyoo vya shimo vilitumbukia kwa sababu udongo una mchanga sana na haukuhimili kuta. Njia bora zaidi wa mamlaka za serikali za mtaa si kuwapiga faini watu kwa kutojenga vyoo, bali ni kuwasaidia kubuni vyoo vitakavyofaa mazingira na hali ya mahali.
4. Ufumbuzi mwingi wa asili kwa matatizo hayo ni nafuu sana kutumia ingawa haufai na baadhi una madhara.

Kupunguza Kasi

Watu wanapougua wanahitaji tiba na matunzo. Vyote hivyo vinaweza kuwa ghali kwa upande wa kutumia fedha na rasilimali nyingine. Sehemu hii kwanza inaangalia baadhi hatua za kuchukua zinazohusiana na tiba na baadaye zinazohusiana na matunzo.

Tiba

Kutumia dawa za kujitibu au waganga wa jadi au tiba ya kisasa	Watu wanaweza kujitibia kwa kutumia ama tiba ya jadi au ya kisasa. Iwapo wana maarifa ya kutosha na fedha hii inaweza kufanikiwa.
Kuchangia gharama	Mwaka 1993/94 serikali ilianzisha uchangiaji gharama katika mfumo wa matibabu ya umma: Mara nyingi matokeo yake, kama ilivyoelezwa na washiriki wa utafiti, imekuwa kupandisha gharama za huduma za afya kiasi cha watu maskini kushindwa. Utafiti wa hivi karibuni wa Bajeti ya Kaya (HBS 2002) unaonyesha kuwa 58.7% ya watu waliohojiwa wamesema kuwa hawakwenda kwa daktari yeyote ingawa walitakiwa kufanya hivyo kwa sababu ni ghali mno.
Kupunguza matumizi mengine	Endapo kutakuwa na mgonjwa, watu wanapunguza matumizi mengine ili kulipia tiba. Kwa mfano, mwanamke kutoka kata ndogo ya Semtema A (Manispaa ya Iringa) alikuwa akimtunza mpwa mwenye VVU mpaka akafariki. Alieleza kuwa *"Tumeshindwa kugharimia madaftari na ada ya masomo kwa watoto wetu. Tulitumia kila senti kwa ajili ya kumtibia mgonjwa. Sasa tumeishiwa kabisa."*
Kuchukua mkopo	Watu wanaweza kukopa ili kulipia tiba. Tatizo ni kwamba riba ni kubwa sana, wakati mwingine inafika asilimia 100 au zaidi.
Kuuza rasilimali ili kuongeza fedha	Kuliko kuchukua mkopo watu wanaweza kuuza rasilimali zao ili kupata fedha wanazohitaji kwa tiba. Ingawa hii inaweza kutanzua tatizo kwa muda, huwatumbukiza katika mtego wa wimbi la umaskini baada ya muda mrefu kwa sababu wameuza zana walizotumia kuendeshea maisha.
Kuomba msamaha wa gharama	Serikali tayari imesamehe baadhi ya makundi ya watu yasichangie huduma. Hayo ni pamoja na watoto chini ya umri wa miaka mitano, maskini sana, watu wanaoumwa maradhi ya muda mrefu kama TB, ukoma, saratani, VVU/UKIMWI na maradhi ya akili. Hata hivyo, washiriki wamesema kwamba watu wengi wa makundi hayo wanaendelea kulipa kwa sababu: - hawajui haki zao; - wakati mwingine maofisa wa afya wanakataa kukubali haki hizo; na - taratibu za kuomba msamaha zinaweza kuwa ghali, hutumia muda na kuleta usumbufu.
Kutumia mitandao ya kijamii	Mara nyingi watu wanaomba msaada kwa familia na marafiki ili walipie gharama za matibabu. Mara nyingi msaada hutolewa hasa ikibainika kuwa ndugu wa karibu wa mgonjwa anafanya kila awezalo kumsaidia. Msaada hauwezi kutolewa iwapo wagonjwa wananyanyapaliwa kutokana na hali zao (kama vile walevi wa dawa za kulevya) au njia ya kuendeshea maisha (kama vile ukahaba). Lakini kwa hali yoyote ile, msaada unapungua polepole kadiri muda unavyopita kwa hiyo wagonjwa wenye maradhi ya muda mrefu, huona kuwa haiwezekani tena kuendelea na matibabu.
Kutafuta huduma za Serikali na Vyama vya Kiraia (VVK)	Walemavu wanaweza kupata msaada kutoka Vyama vya Kiraia na Serikali. Kwa mfano, hupewa viti vya magurudumu ili kuwaondolea upweke wa kutengwa na kuwapa fursa ya kutafuta ajira. Hata hivyo Shirikisho la Vyama vya Walemavu limesema kwamba misaada ya aina hii haina maana yoyote kwa sababu ya mnyanyapao na kutengwa kijamii.
Kusafiri kutafuta tiba	Takriban kaya 500,000 bado ziko umbali wa zaidi ya km 20 kutoka kwenye kituo cha afya kilicho karibu. Wakati kituo hicho hakina maana kutokana na wafanyakazi wasio na ujuzi na ukosefu wa dawa na vifaa. Kwa hiyo, watu inawabidi wasafiri ili kupata huduma wanazozihitaji.

Watu maskini sana, kama ilivyoonekana katika maelezo ya washiriki wa utafiti, hawapati tiba halisi, ina maana kuwa ugonjwa mdogo unaweza kuwa mkubwa au wa muda mrefu. Inapotokea hivyo, uwezo wa mgonjwa kufanya kazi na kuendesha maisha unapungua kadiri muda unavyopita, na hivyo kuchangia katika umaskini.

Matunzo

Mara nyingi wagonjwa wanahitaji kutunzwa na watu wengine. Matunzo yanaweza kuanzia kumhudumia mtu mara moja kwa siku hadi kuwa naye muda wote. Wakati unapomtunza mgonjwa, ni kazi ya muda wote, kwa hiyo mtunzaji hana muda wa kutumia nguvu zake kwa kufanya kazi za kujitafutia riziki.

Endapo mhudumiaji mgonjwa ndiye mtafutaji riziki wa kaya, basi kaya itakosa mapato na ustawi wake kupungua. Iwapo mhudumiaji ni mtoto mwenye umri wa kwenda shule, basi atashindwa kuhudhuria masomo. Hii inakwamisha uwezo wa mtoto kupata elimu bora na hivyo hata fursa nzuri za maisha bora ya hapo baadaye.

Kuhimili

Kama matibabu ni ghali mno au hayawafikii watu, hawana budi kuhimili kadiri iwezekanavyo. Mara nyingi ina maana ya kujifunza kupunguza matumizi na kuishi kwa kipato kidogo. Kama ilivyoelezwa mara kwa mara na washiriki wa utafiti, watu wanaweza kutegemea mitandao ya jamii kwa msaada. Hata hivyo, huu si ufumbuzi mzuri kwa watu wenye ugonjwa wa muda mrefu, kwa sababu watu katika mitandao yao ya jamii hawana uwezo wa kutosha kusaidia muda mrefu.

Miitikio mingi ya ubunifu na isiyo tegemezi inawezekana lakini ni michache sana. Kwa mfano, mtu ambaye ni mhudumiaji anaweza kuanzisha biashara ndogo nyumbani kwao ili amhudumie mgonjwa na kupata fedha wakati huo huo. Hata hivyo, huhitaji maarifa na fedha ambavyo watu wengi hawana. Watu wengine wanalazimishwa kuchagua shughuli isiyohitaji ustahimilivu mkubwa, kama vile kuuza maandazi au chapati, na mara nyingi huwa haiwatoshi kuendeshea maisha.

6.2. Unyanyapazi na Utengaji

Wakati watu wamenyanyapaliwa, wanaonekana kutokubalika na kuaibisha. Hawatendewi haki na mara nyingi kunyanyaswa, kufedheheshwa, kutelekezwa na/au kutengwa na jamii. Makundi yaliyonyanyapaliwa nchini Tanzania ni pamoja na watu wenye maradhi ya ngono, majipu na kutoweza kujizuia. Makundi mengine ni watu wanaotumia dawa za kulevya na aina zote za walemavu.

Kuna matokeo matatu makuu ya unyanyapazi:

1. **Kuongeza ukubwa wa tatizo:** Watu wanapoona aibu hawazungumzii matatizo yao wala kutafuta tiba. Kwa mfano, wanawake wenye maambukizo ya ngono wanaona aibu kukiri chanzo cha maambukizo, kwa hiyo hawapati matibabu mpaka dalili zinakuwa mbaya zaidi na ghali kutibika.
2. **Kuhatarisha watu:** Watu wengi wanahusisha maambukizo ya VVU/UKIMWI na kifo. Kwa hiyo, wanawaogopa watu wanaougua ugonjwa huo. Mara nyingi hali hii husababisha ukatili na kutohurumiwa kwa wagonjwa wa VVU/UKIMWI. Wazee walemavu nao wako hatarini hata kuwafanya wezi kuwaona kuwa lengo lao rahisi. Kuna taarifa za wanafamilia wanaowaua wazee wanaohusisha udhaifu wao na uchawi.
3. **Husababisha uepukaji na ufedheheshaji:** Washiriki wanaoishi na VVU/UKIMWI wanaeleza kuwa mara nyingi wanaepukwa mara watu wanapoelewa kuhusu afya zao. Hii huwasababishia kupoteza ajira zao ingawa bado wana uwezo wa kufanya kazi. Wakati mwingine, hata watu wenye afya katika familia wenye mtu aliyeambukizwa hutaniwa, kufedheheshwa na kulazimishwa wajifiche.

MBINU ZA KUKABILI MISHTUKO NA MIFADHAIKO

Kubadili fikra za watu wengine	Hatua hii inawahimiza wagonjwa kujieleza na kutetewa kushiriki katika kampeni za kufanya afya zao kuwa bora. Tatizo la njia hii ni kwamba watu wengi walionyanyapaliwa wanakosa stadi, kujiamini na fedha za kuendeshea kampeni zenye nguvu.
Kuanzisha Vyama vya Kiraia (VVK) kukabili matatizo ya makundi yaliyonyanyapaliwa	Miaka ya hivi karibuni VVK vimeundwa ili kukabili matatizo ya makundi mahususi yaliyonyanyapaliwa. Vikundi vya awali kabisa vililenga hasa kutoa mahitaji ya kimwili na huduma za afya zinazofaa, lakini hali hiyo inabadilika. Hivi karibuni, VVK, na idara za serikali, vimedhamiria kuhakikisha kuwa watu wanapata haki ya afya na maisha bora. Unyanyapazi wenyewe unapigwa vita.

6.3. VVU/UKIMWI

Wagonjwa wa kwanza wa VVU/UKIMWI nchini Tanzania waliripotiwa mwaka 1983. Makisio ya hivi karibuni yanaonyesha kuwa hadi sasa kuna watu milioni 2 wanaoishi na virusi.

Baadhi ya tabia za kimila, kama vile kushirikiana wapenzi, mitara, na ulevi kupita kiasi, zimechangia kuenea kwa kasi kwa janga hili. Lakini umaskini pia unahusishwa kwa sababu maskini mara nyingi hawapati taarifa na namna ugonjwa unavyoenezwa na namna ya kujikinga. Aidha, umaskini unawalazimisha watu wafanye biashara ya ngono ili wajipatie riziki.

Madhara ya VVU/UKIMWI kwa ngazi ya mtu au kaya yanaonyesha athari kubwa kiasi gani wakati ugonjwa unapochanganywa na unyanyapazi.

Matokeo ya VVU/UKIMWI

Sehemu hii inaangalia namna VVU/UKIMWI unavyoathiri ustawi wa watu, usalama wao na uhuru wao wa kuchagua na kutenda kisha na kufikiria uchaguzi wa mwitikio uliyopo.

Ustawi wa Mwili	Mwanzoni, athari zinazotokana na VVU huwa hazionekani kwa nje. Kipindi hiki kinaweza kuchukua miaka kadhaa. Hatimaye, athari inakuwa kubwa na maambukizo au uvimbe hukua. Mwishowe, mifumo ya kinga ya mwili hudhoofika kiasi cha kufa kutokana na mchanganyiko wa maambukizo yanayotumia udhaifu wa mwili na kuingia mwilini kwa urahisi.
Ustawi wa Vitu	Wakati mtu mzima mwanamume au mwanamke anapoambukizwa VVU/UKIMWI, uzalishaji wa kaya na fursa za kupata njia nyingine za mapato hupungua haraka kwa sababu wanakuwa dhaifu na wagonjwa. Watu hao wakifa huacha wajane na mayatima. Mzigo wa kuhudumia kaya unawaangukia watu wazima wachache zaidi. Wengi wao ni wanawake wajane na wazee. Watu wengi wanashindwa kuhimili kwa sababu kaya zimepoteza wazalishaji wao wakubwa.
Ustawi wa Jamii	VVU/UKIMWI huwapokonya watu marafiki nao na wanafamilia. Aidha husababisha hofu na kutoaminiana miongoni mwa watu. Kutokana na unyanyapazi, watu wanazuiwa kujitetea wao na wategemezi wao ili kuboresha hali zao.
Usalama	Wagonjwa wa VVU/UKIMWI, wahudumiaji, na wengine wanaonyesha kiwango kikubwa cha hofu na shauku. Wagonjwa watu wazima wana wasiwasi kuhusu walichonacho, na nani watatunza familia zao. Wahudumiaji wana wasiwasi kuhusu wagonjwa na wataishi vipi bila ya wao. Pia wana wasiwasi kama wameshaathirika au wamo mbioni kuathirika.

	Hata kaya zisizoambukizwa zinaathiriwa. Watu wana wasiwasi kuhusu kuambukizwa wao na watoto wao. Sasa hofu inakuwepo katika mahusiano ya wake wengi na waume zao.
Uhuru wa kuchagua na kutenda	Mara baada watu kuwa wagonjwa kabisa, wanakwepa kuonekana hadharani wanakoweza kubeuliwa au kufukuzwa. Wakati mwingine, familia zinahimiza hali hiyo kwa hofu ya kuaibishwa na kupewa jina la kaya iliyoambukizwa. Hata kabla mtu hajaugua hali yao ya afya inawazuia kusudi aina ya shughuli na kazi wanazoweza kufanya.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Baadhi ya watu, kaya na jamii wanajitahidi sana kuzuia kuenea kwa ugonjwa pamoja na kuwasaidia watu kuishi na ugonjwa na kustahimili athari zake. Kiasi cha shughuli hizi ni kikubwa mahali ambapo idadi ya wagonjwa ni kubwa. Hata hivyo, kuna matatizo na hatua hizi kwa sababu ya kukosa maarifa, stadi na rasilimali za kutosha.

Kinga

Uchaguzi wa mbinu za kukabidhi mishtuko na mifadhaiko ili kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI ni:

- **Kuwaelimisha watu wengi kadiri iwezekanavyo kuhusu ugonjwa na namna ya kuuzuia.** Serikali na VVK, mara nyingi hufanya kazi kwa kushirikiana, wameendesha kampeni nyingi za kutoa Taarifa sahihi, Elimu na Mawasiliano. Kampeni hizi zimefanikiwa kwa kuongeza maarifa ya watu kuhusu VVU/UKIMWI. Lakini taarifa peke yake haitoshi, lazima ihusishwe na ufumbuzi unaopatikana na una nafuu kiuchumi kwa jamii na utamaduni.
- **Kuainisha na kushughulikia hali za kijamii, kiutamaduni na kiuchumi zinazochangia kuenea kwa VVU/UKIMWI.** Nyingi ya hali hizi huwafanya wanawake wawe hatarini zaidi kuambukizwa VVU/UKIMWI. Kwa mfano, wanaume wana mamlaka ya kuamua iwapo wake zao au wapenzi wao watumie kondomu au hapana. Baadhi ya vyama vya kijamii vinatumia njia za ubunifu, kama vile maigizo ili kuinua mwamko na kubadili hali hizo.
- **Kukabili ukimya na unyanyapazi (mbinu ya kisaikolojia).** Watu wengi hawapendi kuzungumzia kuhusu VVU/UKIMWI. Hii ina maana kuwa watu hawaelewi kwa ukamilifu kile kinachoendelea, na hawawezi kutayarisha mipango ya awali kuhusu hali zao. Kwa hiyo, kupunguza mnyanyapao na ukimya ni hatua muhimu ya kuwapa watu uhuru wa kutumia rasilimali zao katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI.

Kupunguza kasi

Watu wanaoumwa VVU/UKIMWI wanahitaji tiba na matunzo.

Tiba

- Hakuna tiba ya VVU/UKIMWI. Hata hivyo, inawezekana kupunguza kasi ya athari kwa kutumia dawa ambazo ni ghali kwa muda mrefu. Gharama za dawa zimezisababisha kaya nyingi kutumia rasilimali zao zote na kutumbukia katika lindi la umaskini.
- Washiriki wanasema kuwa, katika maeneo ya vijijini, wafanyakazi wa afya hawawaambii watu kuwa wanashukiwa kuwa na VVU/UKIMWI na mara kwa mara hawatoi dawa zaidi ya vidonge vya “Paracetemol” kwa maumivu ya kichwa na mwili yanayohusiana na “ugonjwa wa kudhoofisha mwili”.
- Ukimya kuhusu VVU/UKIMWI unazuia unasihi wa tiba nzuri zaidi ambayo ni lishe bora yenye matunda mengi na protini. Aidha, hata watu wakipata ushauri huo, ni taabu sana kuufuata kwa sababu hawawezi kumudu kununua vyakula hivyo mara kwa mara.

Matunzo

- Watu wanaweza kuishi na VVU/UKIMWI kwa miaka mingi. Kwa hiyo, matunzo yanachukua muda mrefu sana na yanaweza kuwa ya kina zaidi kuliko maradhi mengine. Matunzo ya namna hiyo yanachosha kimwili na kiakili na kusababisha mabadiliko ya majukumu ya kaya. Mara nyingi watoto wanaachishwa masomo. Hii inawaathiri wasichana zaidi ya wavulana kwa sababu wasichana hutakiwa kubaki nyumbani ili kusaidia kumhudumia mgonjwa

Mikakati ya kuhimili ya ngazi ya jamii inatayarishwa katika baadhi ya maeneo ambapo vifo vinavyohusiana na VVU/UKIMWI ni vingi sana. Kwa mfano kijiji cha Maliwa (Wilaya ya Makete) wameanzisha kituo cha mayatima ili kupunguza mzigo wa kuwatunza mayatima 35. Hata hivyo jitihada kama hizo hazina uhakika kwa sababu zinategemea sana ufadhili na michango ya kaya katika eneo lenye tatizo kubwa la janga hilo.

Kuhimili

Njia kuu za kuhimili VVU/UKIMWI katika ngazi ya kaya ni sawa na za maradhi mengine.

Tofauti ni kwamba VVU/UKIMWI unadumu kwa muda mrefu sana na dawa zake ni ghali mno kuliko maradhi mengine. Kwa hiyo, unatumia rasilimali nyingi za kaya.



7. MZUNGUKO WA MAISHA NA UATHIRIKAJI

Sura hii inaangalia mishtuko na mifadhaiko mingi ambayo watu wataikabili kutokana na umri wao na hatua waliyopo katika mzunguko wa maisha. Mzunguko wa maisha una vipindi mbalimbali vya maisha ya mtu, kama vile utoto, ujana, miaka ya kuzaa (utu uzima) na uzee. Sura hii inashughulikia uzoefu wa watu utotoni, wanawake katika miaka yao ya kuzaa na wazee pamoja na athari za kifo katika kaya.

Utotoni, miaka ya wanawake kuzaa na uzee ni vipindi vya maisha ambapo watu wanakabiliwa na vikwazo maalumu katika ustawi wao. Watu wanakuwa hatarini zaidi kuwa maskini katika vipindi hivi vya maisha kwa sababu *wanawategemea sana watu wengine* kukinga, kupunguza kasi na kuhimili sababu zinazowaingiza watu katika lindi la umaskini, hata hivyo washiriki wa utafiti wameona kuwa serikali haitilii mkazo sana kuwasaidia watu katika umri huu.



7.1. UTOTONI

Utotoni ni miaka mitano ya kwanza ya maisha ya mtu. Maendeleo mazuri kimwili na kiakili ni muhimu sana katika hatua hii. Aidha watoto wanajenga stadi muhimu za kujifunza na za kijamii wakati wakiwa wadogo sana.

Maradhi, utapiamlo na matunzo yasiyofaa kutokana na umaskini wa kaya na imani za utamaduni ni vikwazo kwa ustawi wa watoto wadogo. Aidha washiriki wa utafiti nao wameongeza kuwa huduma za afya zilikuwa mbaya na sera ya msamaha wa kuchangia gharama za tiba kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano haikutekelezwa ipasavyo. Mambo haya yanaweza kuathiri utaratibu wa watoto kukua na kujifunza. Watoto wasiopata msingi mzuri wa maisha hawataweza kutumia uwezo wao wote, hali hii inaathiri ustawi wao wenyewe na wa jamii kwa ujumla.

Maradhi

Watoto wa chini ya umri wa miaka mitano wako hatarini kuathiriwa na “maradhi mengi ya utotoni” kama vile surua na dondakoo. Aidha, wako hatarini kupata na kuathiriwa au kufa kwa maradhi yanayowapata pia watoto wakubwa na watu wazima. Hata kama watoto hawafi na maradhi haya, watapata athari ya ubongo au watadumaa.

Utapiamlo

Watoto wanahitaji chakula bora ili wawe na afya, kuishi maisha ya furaha, na kuwa watu wazima wenye uwezo na wazalishaji. Lakini utapiamlo umeenea sehemu nyingi za Tanzania kutokana na umaskini wa kaya. Hii inaathiri uwezo wa watoto kuzingatia masomo, kujihisi wenye nguvu na kupambana na maradhi. Utapiamlo mara nyingi husababishwa na ukosefu wa chakula bora na maji safi, lishe ya kiasili na tabia za ulaji, na matunzo yasiyofaa ya mtoto.

Kati ya asilimia 20 ya familia maskini sana, asilimia 11.6 ya watoto wana uzito mdogo.

Kati ya asilimia 20 ya familia tajiri ni asilimia 2.8 ya watoto tu ndiyo wenye uzito mdogo.

Matunzo duni

Baadhi ya tabia za kiasili zinaonyesha kwamba watoto wadogo hawapati matunzo na upendo wa kutosha kuliko wanavyohitaji. Imani kuwa wanaume hawana jukumu la kushiriki katika malezi na matunzo ya mtoto mdogo imelalamikiwa na wanawake wengi. Kwa sababu wanawake wana majukumu mengi na hawapati msaada wowote kutoka kwa waume wao, mara nyingi inakuwa vigumu kwao kuwapa watoto uangalizi wa kutosha. Wakati mwingine wanaume wanakataa kutoa fedha za kusaidia kulea watoto.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Watoto wa chini ya umri wa miaka mitano wanawategemea sana watu wengine kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao ya chakula, nyumba, upendo na wakati mwingine matibabu. Miitikio ifuatayo imelengwa kusaidia watu wenye jukumu la ustawi wa watoto.

Kuwasamehe watoto gharama za matibabu	Programu zinatekelezwa za kuwapa watoto wadogo matibabu ya bure, ingawa washiriki wa utafiti wamelalamika kuwa programu hizo hazitekelezwi ipasavyo kwa sababu watu hawajui haki zao.
Kuhakikisha kuwa viini lishe vidogo vya kujazia vinapatikana	Serikali tayari ina mpango wa kuwapatia watu virutubisho vya kujazia vya mara kwa mara kwa watoto . Hata hivyo, juhudi hizi zinatakiwa zienezwe zaidi.
Kuimarisha programu za kuwasaidia watoto maskini zaidi	Vikundi vingi vya kiraia (VVK) na idara za serikali vina programu za kusaidia familia maskini zaidi kulea watoto wenye afya. Juhudi hizi zinahitaji kuimarishwa na kuwianishwa ili ziwafikie watoto wengi maskini nchini Tanzania.
Kufuatilia utapiamlo miongoni mwa watoto	Zaidi ya vijiji 4,000 vinashiriki katika programu ya UNICEF ya kufuatilia kukua kwa watoto wao kwa sababu wana wasiwasi na utapiamlo. Programu hii inasaidia njia za kiasili za kufuatilia ukuaji wa watoto.

7.2. Miaka ya Kuzaa

Wanawake wengi wanaona miaka yao ya kuzaa ni wakati wao wa mifadhaiko na hatari sana. Hii ni kutokana na huduma duni za afya ya mama mjamzito, kupata mimba katika umri mdogo, uwezo mkubwa wa kuzaa na kupunguza nyendo. Zaidi ya mwanamke 1 kati ya 20 wenye umri wa kuzaa hufa kwa sababu za uzazi. Hali ni mbaya zaidi katika baaadhi ya mikoa kuliko mingine na katika maeneo ya vijijini na kaya maskini.

Huduma duni au chache za afya ya mama mjamzito

Huduma duni na chache za afya ya mama mjamzito huongeza sana hatari ya afya kwa wanawake wajawazito na wanaojifungua. Hii ni dhahiri kwa wanawake maskini na wanawake wa vijijini.

Takwimu za uzazi

Miongoni mwa 20% ya kaya maskini sana ni 4% tu ndio wanaokwenda kuonana na daktari kwa huduma ya wajawazito. Kwa 20% ya matajiri sana, takwimu zinaonyesha 12.7%.

Miongoni mwa 20% ya kaya maskini, ni 26.7% ya wanaojifungua wanahudumiwa na wahudumu waliopata mafunzo. Kwa 20% ya familia matajiri sana, takwimu ni 80.9%.

Wanawake wengi wanaogopa kufa wakati wa kujifungua. Hofu hii inawagusa hasa wanawake (a) wasiohudhuria kliniki za wajawazito (b) wasio na wakunga wenye ujuzi wakati wa kujifungua na (c) wanaoishi mbali na kituo cha afya chenye vifaa vya kutosha watakakopelekwa itokeapo dharura. Idadi ya wanawake wanaojifungua katika mazingira hayo inaongezeka.

Idadi ya akinamama wanaozalia katika vituo vya afya imepunguasana. Utafiti wa hivi karibuni na maelezo ya washiriki wa utafiti walihitimisha kupungua huko kuwa huenda ni kutokana na:

- Kuanzishwa kwa ada kupata ya huduma;
- Huduma duni; na
- Vifaa na zana chache.

Matokeo ya utafiti wa TzPPA yanapendekeza kuwa baadhi ya sababu muhimu ni pamoja na:

- Umbali wa kufikia vituo vya afya vyenye zana zinazofaa;
- Umaskini wa kipato; na
- Madaraka waliyonayo wanaume ya kuamua lini rasilimali za kaya zitumike kwa mahitaji ya matunzo ya afya ya uzazi.

Aidha utapiamlo miongoni mwa wanawake wajawazito, hasa ukosefu mkubwa wa vitamini A na upungufu wa damu, husababisha matatizo makubwa wakati wa kujifungua na wakati mwingine hata kifo.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko zimo katika makundi mawili – kuimarisha huduma za akinamama wajawazito kabla ya kujifungua na wakati wa kujifungua ili ziwe bora zaidi.

Kuimarisha Huduma za Wajawazito (kabla ya kujifungua)

Sehemu kubwa ya mikakati ya wanawake wengi ya kuhimili inahusisha matumizi ya ujuzi asilia kutoka kwa watu wanaowaamini (marafiki, mama, bibi). Ushauri wa ndugu na marafiki ni rahisi na hauna gharama. Hata hivyo, wakati baadhi ya taarifa hizi zinasaidia, nyingine zinaweza kuleta madhara kwa afya ya mama na mtoto. Aidha wanawake wanaweza kwenda kwenye vituo vya afya vya mbali mapema wakati wa ujauzito ili kupima afya zao na mtoto.

Wakati mwingine wanawake wanajiwekea akiba zao ili kugharimia huduma ya ujauzito. Katika jamii moja, wanawake walichangisha fedha kutoka kila kaya ili kulipia ziara za mara kwa mara zinazofanywa na kitengo cha huduma ya mama na mtoto kinachowatembelea. Jamii nyingine zimeweza kupata msaada kutoka kwa Serikali za Mitaa au AZISE ili kuboresha huduma za afya za mama wajawazito.

Kuimarisha Huduma za Uzazi (wakati wa kujifungua)

Wakunga wa jadi wanaweza kutoa huduma bora kwa usalama wa mama na mtoto katika uzazi wa kawaida kwa kutumia usafi, ufungaji kitovu, n.k. Lakini zitokeapo dharura wakati wa kujifungua nyumbani, mama mjamzito lazima apelekwe haraka sana katika kituo cha afya chenye vifaa vya kutosha. Huu unaweza kuwa utaratibu wenye gharama sana ambao watu wengi hawawezi kumudu.

Uchunguzi umeonyesha kuwa serikali na AZISE wamekuwa wakijitahidi kutoa huduma bora zaidi stadi za wakunga wa jadi na kupanua huduma za rufaa za dharura kwa jamii za mbali. Na kuna uwezekano wa kuanzisha “Nyumba za kusubiria” za gharama nafuu karibu na vituo vya afya vyenye watumishi na vifaa bora. Wanawake kutoka jamii za mbali wanaweza kuishi pale katika siku zao za mwisho kabla ya kujifungua.

Mimba katika umri mdogo

Wanawake wanaopata ujauzito katika umri mdogo mara nyingi wanapata matatizo wakati wa ujauzito na kujifungua kwa sababu miili yao bado haijakomaa vizuri. Matatizo haya ni pamoja na uharibikaji mimba, kushindwa kujizuia (kutokwa mkojo) na hata kifo. Hata hivyo wanawake wengi wanazaa wakiwa wadogo, kuliko ilivyokuwa zamani. Kuna sababu tatu za hali kama hiyo:

- Usalama mdogo wa wanawake wenye umri mdogo umesababisha ongezeko kubwa la ubakaji;
- Usalama mdogo wa mali umewafanya wasichana watafute watu wazima matajiri ili “kuwasaidia”; na

- Wazazi maskini wanawauza mabinti wao kwa wazee wanaoweza kulipa mahari.

Maadili ya kiutamaduni yanaweza pia kusababisha matatizo kwa wanawake wajawazito vijana. Kwa mfano, katika kijiji cha Maliwa (Wilaya ya Makete) wazazi wanatarajiwa kuwafukuza mabinti waliozaa nje ya ndoa. Katika jamii nyingine, ni jambo la kawaida kwa wazazi kuwapiga, kuwanyima chakula au kuwatelekeza wasichana wajawazito wasioolewa hata kama mimba zao zimetokana na kubakwa.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Hatua zilizochukuliwa na wazazi na wasichana watoto kuepuka mimba ni pamoja na:

- Kuwatoa shule wasichana baada ya kuvunja ungo na kudhibiti nyendo zao. Hata hivyo, hii inamfanya msichana awe katika hatari zaidi ya umaskini kwa kumzuia asipate elimu na kuunda mitandao mizuri ya kijamii;
- Wasichana kukaa pamoja usiku; na
- Kutumia mbinu za kuzuia mimba za kiasili na za kisasa.

Wakati hatua hizi za kinga zinaposhindwa, mbinu za kiasili kama vile ndoa za kulazimishwa wakati mwingine zinatumika wakati mwanamke asiyeolewa anapopata mimba. Katika baadhi ya jamii, kuzaa nje ya ndoa si tatizo, na wanaume wanalazimishwa kutoa gharama za matunzo ya watoto wao. Mara nyingi hatua hizi hazileti matokeo yanayotarajiwa.

Lakini haitoshi kuwatenga wanawake vijana au kuwapatia mbinu za kuzuia mimba. Mkakati mzuri ni kujaribu kubadili hali za uchumi na tabia za kiutamaduni zinazoleta matatizo.

Kiwango kikubwa cha Uzazi

Mwanamke wa kawaida wa Tanzania atakuwa amezaa watoto watatu anapofikia mwishoni mwa umri wa miaka 20; watano mwishoni mwa miaka 30; na saba mwishoni mwa miaka yake ya kuweza kuzaa. Kuna sababu kuu mbili za kiwango kikubwa namna hiyo cha uzazi.

Washiriki wameeleza kuwa "*Wanaume wa hapa wanataka daima wake zao wawe wajawazito au wanalea*", kwa hiyo, wanaume hawako tayari kutumia njia za uzazi wa mpango. Sababu nyingine ni kwamba wanawake wanaweza kuongeza heshima zao na usalama ndani ya familia au ukoo kwa kuwa na watoto wengi.

Kiwango kikubwa cha uzazi maana yake ustawi wa mwili wa mwanamke kuugua kutokana na lishe duni, kutokwa na mkojo na kuchanika mfuko wa uzazi. Wanawake walioshiriki wameeleza namna wanavyochoka kimwili na kiakili kwa kukosa muda wa kupumzika kati ya ujauzito na wana watoto wengi wa kuwatunza.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Huduma za uzazi wa mpango ni njia muhimu sana ya kudhibiti viwango vikubwa vya uzazi na upangaji mbaya wa uzazi. Kuwepo kwa huduma za aina hiyo, ukichanganya na mbinu za uzazi wa mpango za asili, kumesaidia kupunguza viwango vya uzazi. Kampeni za kupashana habari, elimu na mawasiliano zinazoendelea pia zitasaidia kuhimiza kupunguza viwango vya uzazi na kupanga uzazi.

Hata hivyo, tatizo ni kwamba wanaume daima ndio wenye mamlaka ya kuamua kutumia au kutotumia mbinu za kuzuia mimba. Washiriki wanawake wamesema kuwa kukosa kwao elimu rasmi kumeathiri uwezo wao wa kufanya maamuzi kuhusu kutumia uzazi wa mpango. Wamesema elimu inaweza kuwapa kujiamini na uwezo wa kujadili maslahi yao.

Kwa hiyo, huduma za uzazi wa mpango hazina budi kuhusishwa na hatua kama vile kuwapa uwezo wanawake kwa njia ya elimu na kubadili uhusiano wa kijinsia katika kaya ili wanawake waweze kutoa maamuzi kuhusu uzazi wao.

Kutoweza Kutembea

Wanawake wajawazito na wanaowalea watoto wadogo wanaona vigumu kutembea. Hii husababisha kutengwa kijamii na kuwa vigumu kujitafutia riziki. Hali hii inawafanya wanawake wawe wategemezi wa wanaume na wanafamilia wengine. Matokeo yake ni kwamba wanawake wengi wanakuwa na njaa wakati miili yao inahitaji sana chakula na hawana uhakika kuwa mlo mwingine wataupata wapi kulisha familia zao. Kutoweza kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kuna maana ya kuwa masoko, kliniki na mahakama ni taabu kuzifikia wakati wa shida.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Wanawake wanatumia mitandao yao ya kijamii kwa ajili ya msaada. Wakati wa ujauzito marafiki na wanafamilia wanaweza kutafuta misaada hapa na pale ili kusaidia kukidhi mahitaji ya msingi. Mitandao hiyo hiyo inaweza kusaidia malezi ya watoto. Wanawake wanaojiweza kiasi wa mjini wanaweza kumudu kulipia mlezi binafsi.

Baadhi ya wanawake wana mitandao mizuri kuliko wengine, hasa wale wenye ndugu zao karibu. Kiasi cha msaada wanachopata wanawake kinategemea sana namna wanavyoishi (wako karibu kiasi gani na wanawake wengine), hadhi na uwezo wa kulipa fadhila.

7.3. Kuzeeka

Wazee wanakabiliwa na mabadiliko ya kimwili na kijamii wakati wanapozeeka. Baadhi ya mabadiliko ya kimwili hayaepukiki, lakini ya kijamii yanategemea sana mitazamo na maadili ya kitamaduni. Mabadiliko ya aina zote mbili husababisha kupungua kwa *ustawi wa mwili, mali na jamii* kwa wazee wengi.

Mabadiliko ya kimwili

Wazee wanakabiliwa na mambo yafuatayo yanayoathiri *ustawi wa miili* yao:

- Kupungua kwa nguvu na uwezo;
- Matatizo ya afya yanayowakabili wazee, kama vile, yabisi kavu, baridi yabisi, ugonjwa wa mifupa n.k.;
- Mfumo wa kinga ya mwili kupungua, na kuwafanya wawe hatarini zaidi kuambukizwa maradhi ya kawaida kama vile malaria na mafua; na
- Majeraha ya ajali yanakuwa mengi na huchukua muda kupona.

Kutokana na mabadiliko haya ya ustawi wa mwili, *ustawi wa mali* wa wazee hupungua kwa sababu hawawezi tena kufanya kazi, kujitafutia riziki na kujihudumia. Wengi wao wanatumbukia katika lindi la umaskini.

Mabadiliko ya mwili pia yana athari mbaya kwa *ustawi wa jamii*. Kwa mfano kukoma kwa hedhi, uhanithi na kutojizuia haja ndogo/kubwa vinaweza kuharibu hadhi na heshima ya mtu. Aidha, inaweza kuwafanya washindwe kuhudhuria mikutano ya jamii kunakotolewa maamuzi muhimu. Udhaifu pia unawafanya wazee wawe rahisi kuibiwa. Baadhi yao wanaogopa kuibiwa na vibaka usiku au wanapokwenda kusali alfajiri.

Mabadiliko ya Kijamii

Hali ya maisha ya wazee inategemea namna wanavyoonekana au kutendewa na watu wengine. Ni kawaida kwa Tanzania kuonyesha heshima kwa wazee na kuwapa upendeleo maalumu. Hata hivyo, mara nyingi haiwi hivyo. Wazee bado wanaheshimiwa lakini vikongwe wanabeuliwa na kunyanyaswa, hasa wanapokuwa na elimu rasmi ndogo, kuwa na upungufu wa uwezo wa akili na mwili na hawapati matunzo mazuri. Busara za vikongwe hazithaminiwi tena kama ilivyokuwa zamani, na mara nyingi wanaonekana kama watu wazima waliofikia upeo wa maisha.

Kwa kuwa wanaume ndio wanaoendesha uchumi, wanapozeeka na kushindwa kufanya kazi, wanashindwa kutoa mchango muhimu katika kaya. Wanawake vikongwe wakati mwingine wanaweza kusaidia kulea watoto na kazi nyingine za nyumbani. Hata hivyo, siku hizi wazee wasiochangia chochote wana uwezekano wa:

- Kutelekezwa na watoto wao;
- Kukosa mawasiliano na mitandao mingine ya misaada; na
- Kupoteza hadhi yao ya kijamii na heshima.

Uhamaji na VVU/UKIMWI pia huleta athari kubwa kwa maisha ya wazee, hasa katika jamii za wakulima na wavuvi ambapo idadi kubwa ya watu wenye umri wa kati hawapo tena katika nguvukazi. Wazee inawabidi wabebe mzigo wa uzalishaji na wa kuwatunza mayatima.

Washiriki wameona kuwa wanaume vikongwe wameonyesha kuwa na afadhali zaidi kuliko wanawake vikongwe. Hii ni kwa sababu wanawake wanaelekea kuishi kuliko waume wao, na kwa hiyo wanamudu maisha bila wenzi wao katika hatua za mwisho za maisha. Aidha wamo hatarini kutuhumiwa kwa uchawi na kunyang'anywa rasilimali zao. Katika mikoa ya Rukwa, Tanga na Shinyanga hili linaonekana kuwa ni tatizo kubwa kwa ustawi wa wazee na hata tishio kwa maisha yao.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Mabadiliko ya mwili ya kuzeeka hayaepukiki; hata hivyo kushuka kwa ustawi wa jamii na vitu wanakokabiliwa nako vikongwe kunaweza kubadilika. Baadhi ya uchaguzi wa mwitikio wa washiriki umeonyeshwa hapa chini:

Kutumia njia za kuendeshea maisha zisizochosha	Wanaume katika kijiji cha Mwakizega (Wilaya ya Kigoma Vijijini) wanaanza kusokota kamba na kusuka majamvi wakati hawawezi tena kuvua. Bahati mbaya, shughuli hiyo haina kipato kikubwa na inakuwa vigumu kwao kutokana na macho kupungua nguvu na ugonjwa wa yabisi kavu, n.k.
Kutegemea vitegauchumi na rasilimali	Watu wanaweza kutumia vitegauchumi walivyoweka na rasilimali walizojenga walipokuwa vijana. Kwa mfano, baadhi ya watu walipanda kahawa na korosho ili wavune wakati wa uzee. Hata hivyo, huu uwekaji akiba wakati wa ujana si wa kutegemea sana kwa vile hali ya soko inaweza kubadilika na rasilimali zinaweza kupotea iwapo hazitasimamiwa vizuri.
Kutegemea msaada kutoka kwa wengine	Wakati rasilimali zinapokuwa zimetumika, wazee wanakuwa wategemezi wa msaada wa familia na majirani. Kiasili, familia imekuwa chanzo muhimu sana cha msaada na bado ni tegemeo – hata hivyo siku hizi kiwango cha msaada hakitoshi. Hata kama msaada wa fedha unatosha, kuna mahitaji mengine. Wazee wanaweza kuhitaji msaada wa kupika, kuoga, kupata huduma za jamii n.k. Aidha wanahitaji mazungumzo na kuwa na rafiki.

Kutoa njia za kutatua tatizo	Vikundi vya Kijamii (VVK) na mashirika mbalimbali ya Serikali kutoa njia za kutatua tatizo. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kiislamu, msikiti huwa unasambaza misaada kwa vikongwe vyenye upweke. Hata hivyo, kuna haja ya kuwa na utaratibu mzuri zaidi wa njia za kutatua matatizo ya umma.
Kuwa na msamaha unaofaa kwa vikongwe	Maofisa wa Serikali hawatakiwi kuwatoza vikongwe gharama za matibabu au kuwalazimisha kulipa kodi ya maendeleo. Hizi ni sera nzuri wakati zinapotumika. Lakini washiriki wamesema zitawanufaisha wazee iwapo tu: • Habari kuhusu programu hizo zinatangazwa sana • Taratibu za kutoa msamaha zinarahisishwa na kutangazwa • Viongozi wa eneo wanaheshimu na kufuata utaratibu huo

7.4. KIFO

Kifo cha mwanafamilia kinaweza kuleta mshtuko mkubwa na chanzo cha mfadhaiko kwa wale wanaoachwa. Kunaweza kuathiri ustawi wa vitu, lakini pia kinaweza kuathiri ustawi wa kijamii na usalama, na kuzuia uhuru wa watu wa kuchagua na kutenda. Matokeo ya kifo katika familia yamo katika makundi matano yafuatayo:

Gharama za mazishi	Taratibu za asili za mazishi huchukua siku nyingi na kuhusisha kutoa chakula na vinywaji kwa idadi kubwa ya wageni. Hii ni ghali sana na watu wengi hivi sasa wanafupisha siku za maombolezo.
Nguvu kazi iliyopotea	Nguvu kazi ni rasilimali muhimu sana ya kaya maskini. Hata kama mzalishaji mali mmoja akifa, waliobaki wanaathirika. Athari inakuwa kubwa zaidi iwapo aliyefariki ndiye mtafutaji mkuu.
Rasilimali zinachukuliwa	Wakati waume, baba na wazazi wanakufa, wanafamilia mara nyingi wanachukua rasilimali za kaya kutoka kwa wanawake na watoto, wakidai kuwa wamo katika familia kubwa. Baadhi ya hawa wanaochukua mali, hasa inapohusu ardhi, wanaweza kuwa katili na wakali.
Hisia ya majonzi na kukosa usalama	Wakati mwingine kifo cha mwanafamilia kinaweza kuharibu kabisa ulimwengu wa kijamii wa waliobaki na kuwaondolea hisia yao ya usalama na ulinzi. Kifo cha mume au mzazi kinaweza kuwaacha wanawake na watoto bila mtu wa kuwakilisha maslahi yao wakati maamuzi muhimu yanapofanywa.
Mayatima wanaachwa peke yao	Mara nyingi wazazi wanapofariki wanawaacha mayatima peke yao. Mayatima wanakuwa hawajui kusoma na kuandika kwa sababu walezi wao hawana uwezo wa kuwalipia shule. Wale wasio na walezi inabidi wajihudumie tangu wakiwa na umri mdogo.

Watu wazima wengi wa umri wa kati hivi sasa wanafariki kutokana na VVU/UKIMWI. Hii inasababisha matatizo mengi ambayo yanaathiri ustawi wa watoto wao na taifa. Baadhi ya matokeo ni:

- Urithishaji wa maarifa na stadi kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto haufanyiki tena;
- Watoto wanarithi madeni badala ya rasilimali kutoka kwa wazazi wao; na
- Kwa sababu watoto wanaacha shule ili kujitafutia kazi za kukidhi mahitaji yao ya lazima, kutakuwa na watu wazima wachache wenye elimu rasmi baadaye.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kifo ni sehemu ya kawaida ya maisha. Watu wanaweza kujiandaa kwa kifo na kuwasaidia wengine kumudu au kuhimili matokeo ya kifo. Taratibu za mazishi ni matukio ya kijamii yanayowaruhusu waliobaki kupunguza majonzi yao. Mitandao ya kijamii inaweza kusaidia kaya husika kuhimili/ kumudu gharama za taratibu hizo.

Kuna njia za kiasili za kushughulikia kifo cha mume, mke na mzazi. Kwa mfano, katika baadhi ya sehemu za Tanzania, kaka wa mume aliyefariki anatakiwa amtunze mjane na watoto wake. Baadhi ya washiriki wamesema hii inaweza kusaidia, hata hivyo wakati mwingine ndugu wenye uchoyo wamechukua rasilimali za mjane na kutomhudumia. Wanawake wanaopokufa, waume wao wanaweza kuoa wanawake wengine na dada au wake wenza watawatunza watoto. Iwapo wazazi wote wanakufa, shangazi au mjomba mara nyingi atakuwa na jukumu la watoto yatima.

Hata hivyo mifumo yote hii inakabiliwa na mfadhaiko mkubwa wa VVU/UKIMWI, unaoendelea kupunguza watu wenye umri wa kati nchini Tanzania na hivyo kuzimaliza baadhi ya koo au familia. Hii ina maana kuwa watoto lazima walelewe na vikongwe ambao mara nyingi hawawezi kuwatimizia mahitaji mengi watoto hao vijana. Kaya za namna hii ziko katika hatari kubwa ya kuwa maskini.

Kutokana na mabadiliko makubwa ya sasa ya mila na desturi yaelekea, hakuna ufumbuzi uliotolewa na njia za asili kwa tatizo hili jipya, kwa hiyo mashirika ya jamii yanajaribu kuziba pengo. Kwa mfano, katika jamii moja, watu walijiandaa kupeleka chakula na kuni kwa kaya za vikongwe wanaolea mayatima.

8. MILA NA DESTURI NA UATHIRIKAJI

Imani na desturi nyingi za kiasili zinatumika katika hali au njia zinazosababisha matatizo kwa baadhi ya watu. Serikali imepitisha sera nyingi na sheria za kuweka hali hiyo kuwa bora zaidi (angalia kisanduku), lakini sheria hizi zimesemwa na washiriki wa utafiti kuwa si mara zote kufanikiwa kubadili desturi mbaya. Kwa sababu desturi hizi zimo ndani ya mamlaka za jamii nyingi.

Sheria za serikali zinazoshughulikia mazingira ya mila na desturi kuwa bora zinajumuisha vitu kama:
- Sera ya Ajira Mbaya ya Watoto
- Kuanzishwa kwa vyombo vya mikopo vilivyolengwa kwa vijana na wanawake kupitia Halmashauri za Serikali za Mitaa
- Sheria ya Ardhi ya 1999
- Sheria ya Ndoa Na. 5 ya 1971 na marekebisho yake
- Sheria ya Ubakaji na Unyanyasaji Kijinsia ya 1998
- Sera ya Maendeleo ya Vijana

Mila na desturi zinazosababisha kero zaidi ni zile zinazokwaza:

- Nyendo za watu;
- Uhuru wao wa kutenda; na
- Uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu maisha yao.

Desturi hizi zinakwaza zaidi wanawake kuliko wanaume, ndio maana wao kama kikundi wamo hatarini zaidi kuwa maskini kuliko wanaume. Hata hivyo, watoto, vijana wa walemavu pia wanakwazwa na desturi hizi.

Sura hii inajadili mishtuko na mifadhaiko inayosababishwa na imani za kitamaduni na mila na desturi kwa kuvigawa kwenye makundi mawili makuu:

Masuala yanayoathiri vikundi mahususi vya jamii	**Masuala yanayohusu desturi na imani**
• Watoto • Vijana • Wanawake • Vikongwe • Walemavu	• Sherehe • Mahari • Miiko • Kaya kubwa • Imani za kichawi • Ulevi

8.1. MASUALA YANAYOATHIRI VIKUNDI MAHUSUSI VYA JAMII

Baadhi ya mila na desturi hupunguza ustawi wa watoto, vijana, wanawake, vikongwe na walemavu. Hii ni kwa sababu vikundi hivi vimeathiriwa vibaya kwa:

- Kuwekewa masharti kwa rasilimali za uzalishaji;
- Mamlaka yasiyo sawa katika kufanya maamuzi; na
- Unyanyasaji na utumiaji nguvu vilivyohalalishwa kimila.

Masuala yanayoathiri watoto

Watoto wenye umri wa kwenda shule wamesema kuwa mara nyingi wanafanyiwa mambo mabaya, kama vile kubaguliwa, kuonewa na kutelekezwa nyumbani, shule na katika jamii. Wakati mwingine watoto wananyanyaswa kimwili na kingono au kutelekezwa. Unyanyasaji wa aina hiyo unaleta mfadhaiko wa mwili na akili. Unyanyasaji ni sababu mojawapo ya watoto kuondoka nyumbani na kuishi mitaani.

Wasichana wanakabiliwa na hatari nyingi kuliko wavulana. Hawana uhakika wa kwenda shule na kujisomea kutokana na kazi za nyumbani. Kuna uwezekano mkubwa wa kubakwa au kunyanyaswa kingono, kunakowafanya wawe hatarini kuambukizwa maradhi ya ngono, VVU/UKIMWI, na mimba katika umri mdogo. Wakati mwingine, wanalazimishwa kufanya mapenzi na wanaume ili kupata zawadi au fedha. Kutokana na matatizo haya, mara nyingi wanaacha shule, na kukosa kwao elimu kunaharibu ustawi wao wa baadaye.

MBINU ZA KUKABILI MISHTUKO NA MIFADHAIKO

Ni vigumu kwa watoto kukabili unyanyasaji peke yao kwa sababu ni wadogo, hawana uwezo wa kuchagua, na wanakosa sauti ya kujitetea dhidi ya unyanyasaji. Watoto wamesema kuwa unyanyasaji wao unaendelea kwa sababu wanakosa kinga na mahali watakakojitetea dhidi ya unyanyasaji.

Zifuatazo ni hatua kuu wanazochukua baada ya kushindwa kabisa kustahimili unyanyasaji:

- Kuacha kwenda shule;
- Kukimbia na kwenda kuishi na ndugu;
- Kukimbilia mijini na kuishi kama watoto wa mitaani (au kulazimishwa katika ajira mbaya ya watoto); na
- Kuwa ombaomba au vibaka.

Mwaka 1996 Serikali ilitunga Sera ya Maendeleo ya Mtoto inayosisitiza haki za watoto. Serikali pia imetia saini Mkataba wa ILO Dhidi ya Aina Mbaya Zaidi za Ajira ya Mtoto, mwaka 1999, inayowalinda watoto wanaofanya kazi katika mashamba makubwa ya biashara, migodini na uvuvi. Sera hizi ni nzuri, lakini mara nyingi hazifai kwa sababu ya umaskini na viwango vidogo vya elimu katika kaya na imani kwamba “Watoto lazima watii amri na si kuhoji watu wazima.” Aidha hakuna hatua zinazofaa za kuzuia unyanyasaji wa watoto.

Baadhi ya Vikundi vya Kiraia (VVK) vinashughulikia masuala haya kwa kuwapa nafasi watoto ya kujadili kuhusu unyanyasaji. Kwa mfano, wanandaa Bunge la Watoto kila mwaka tarehe 16 Juni.

Masuala yanayowaathiri vijana

Hali ya vijana inaathiriwa na hali ya kiuchumi, mazingira na utawala. Aidha vijana wanaathiriwa na ubaguzi kutoka kwa watu wazima kutokana na desturi. Ubaguzi wa aina hii una athari kuu mbili kwa vijana:

1. **Hukwaza udhibiti wao kwa rasilimali za uzalishaji.** Vijana hawana nafasi kubwa ya kupata wala kumiliki mali na rasilimali katika kaya na jamii. Hii ni kwa sababu kuna mila zinazowakataza vijana kumiliki au kudhibiti rasilimali, kwa hiyo rasilimali nyingi zinamilikiwa na kudhibitiwa na watu wazima. Matokeo yake, wanapata taabu sana kuishi kwa kujitegemea.
2. **Huwazuia kushiriki katika kutoa uamuzi.** Mara nyingi vijana wanazuiwa wasishiriki katika utoaji wa maamuzi kuhusu matumizi au usimamizi wa rasilimali za jamii. Kwa mfano, katika kijiji kimoja wilayani Bagamoyo, vijana wanalazimika kusafiri mbali kutafuta kazi za msimu kwa sababu hawapati mgao wa ardhi ya familia mpaka baba afe.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kutumia sheria za kimila	Wakati mwingine sheria hizi zinaweza kuwasaidia vijana kupata rasilimali lakini haitokei mara nyingi. Kwa mfano katika baadhi ya jamii, watoto wakubwa au wadogo kabisa hurithi rasilimali na mali ya wazazi. Lakini uamuzi huu unawabagua wasichana kwa sababu urithi mara nyingi unakwenda kwa wanaume.
Kujaribu njia mpya za kujitafutia riziki	Wakati mwingine vijana wanakopa au kukodi mali kupanua shughuli zao za kujitafutia mapato au wanafanya kazi zisizohitaji rasilimali nyingi. Kwa mfano, badala ya kulima, vijana wanafanya biashara ndogondogo au uvuvi.
Kuhamia mijini	Vijana wengi wa vijijini wanakimbilia mijini ili kujitafutia kazi. Hata hivyo, mara nyingi wanapata kipato kidogo, kazi za mikono ambazo mara nyingi ni ngumu. Mara nyingi hulipwa kutwa, kwa hiyo hawana usalama.
Kukaa bila ajira	Vijana wa vijijini wasioweza kuhamia mijini wanabaki vijijini na kukosa kazi. Vijana katika hali hii hustahamili kwa kutumia dawa za kulevya.
Kuwalaumu wazazi na wazee	Kutokana na kukata tamaa, baadhi ya vijana wanapingana na wazazi wao na kuwalaumu viongozi wa jamii, mara nyingi hali hii huathiri amani na utulivu wa jamii. Katika baadhi ya matukio, vijana wanajiunga na vyama vya upinzani ili kupinga hatua za jamii zilizoamuliwa na wazee.

Masuala yanayowaathiri wanawake

Mila na desturi kuu zinazowabagua wanawake ni:

- Sheria za upendeleo za mirathi;
- Mamlaka yasiyo sawa ya kufanya maamuzi; na
- Unyanyasaji na utumiaji nguvu vilivyohalalishwa kimila.

Sheria za upendeleo za mirathi

Inapokuja suala la kumiliki mali na kudhibiti rasilimali, sheria za kimila zinawapendelea sana wanaume kuliko wanawake katika sehemu nyingi za Tanzania. Kuna aina mbili za mirathi zinazoathiri wanawake:

1. **Mali inaporithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.** Mara nyingi wanaume ndio wanaorithi. Siku hizi kuna rasilimali ndogo hata kwa wanaume kurithi, kwa hiyo uwezekano wa wanawake kunufaika na urithi ni mdogo.
2. **Wakati mali inaporithiwa na mjane baada ya kifo cha mume.** Kuna sheria inayosema kuwa mali yoyote iliyochumwa wakati wa maisha ya wanandoa itamilikiwa sawa na mume na mke. Hata hivyo, mila na desturi za jamii nyingi haziitambui sheria hiyo, kwa hiyo wajane wengi wananyimwa kwa sababu ndugu zao wanachukua rasilimali zao zote. Matokeo yake, wajane wanapata taabu sana kuishi na kuwalisha watoto wao.

Wanawake waliotalikiwa pia wanaweza kuteswa sana ingawa kuna sheria za kimila na rasmi zinazolinda haki zao. Mara nyingi wana matatizo mengi ya kupata malipo kutoka kwa waume wao waliowataliki.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Kuna ukomo wa kile wanachoweza kufanya wanawake kwa sababu wengi wao:

- Wana rasilimali chache sana za kuwekeza katika shughuli za uzalishaji;
- Wanakosa stadi za kuajirika;

- Wana viwango vidogo vya elimu; na
- Hawana mtaji wa kuanzisha biashara zao.

Baadhi ya mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko ni:

Kutafuta msaada wa sheria ya kimila au dini	Mara nyingi sheria hizi hazina manufaa kwa wanawake. Sheria za kimila katika baadhi ya jamii zinalinda haki ya wajane kwa mali. Hata hivyo katika jamii hizi ndugu wanaweza kunyang'anya mali kutoka kwa wajane wasio na watoto kwa waume waliokufa.
Kutumia sheria rasmi	Sheria rasmi zinasema kuwa wajane wana haki ya mali. Baadhi ya wanawake wanatumia sheria hizi, lakini mfumo wa sheria umeonekana kuwa mgumu kutumiwa na watu maskini. Hawajui haki zao za kimila na sheria au namna ya kupata msaada wa kisheria. Rushwa katika mfumo wa mahakama pia ni kikwazo kwa wanawake kupata haki zao.
Kupata msaada kutoka VVK	Vyama vya Kiraia kama vile Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Msaada wa Sheria kwa Wanawake (TWLA) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) wanatetea haki za wanawake. Hata hivyo, si wanawake wote wenye uwezo kwa kufikia huduma hizo wala haziwezi kuwa badala ya taasisi za serikali.

Mamlaka yasiyo sawa katika kutoa maamuzi

Wanawake wengi wanajikuta wakinyimwa nafasi ya kufanya maamuzi yanayohusu maisha yao kutokana na mitazamo ya kimila kuhusu jinsia. Matokeo yake, wanawake wanaathiriwa kwa njia zifuatazo:

Kukosa udhibiti wa mapato ya kaya	Katika sehemu nyingi za Tanzania, rasilimali nyingi za kaya (zikiwemo fedha taslimu) hudhibitiwa na wanaume, hata kama mapato yanaingizwa na wanawake. Katika kaya zinazoongozwa na wanawake, wanawake wana uwezo zaidi kwa sababu wanadhibiti rasilimali.
Kazi nyingi	Hakuna usawa wa mgawanyo wa kazi katika kaya nyingi. Hii ina maana kuwa wanawake wana sehemu kubwa ya majukumu ya kaya. Hii inaweza kusababisha maradhi na uzalishaji mdogo.
Kukosa udhibiti wa uzazi wa mpango	Katika jamii nyingi wanaume bado wanawazuia wanawake kutumia mbinu za uzazi wa mpango. Hii husababisha matatizo ya afya kutokana na mimba nyingi na huongeza hatari ya kuambukizwa maradhi ya ngono au VVU/UKIMWI. Mwanamke wa kijiji kimoja katika Wilaya ya Muheza alisema kuwa iwapo mume atagundua kuwa mke wake ametumia mbinu ya uzazi wa mpango, atapigwa au kuachwa.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Wanawake wengi wanajaribu kuepuka njia zenye upinzani na mabishano zinazoweza kusababisha mgogoro katika kaya. Wanatumia mila na desturi zinazowaruhusu kuwa na udhibiti wa kiasi fulani kwa utaratibu wa shughuli za kuingiza mapato na mapato yenyewe.

Ili kuhimili, wanawake wanaanzisha shughuli zao za uchumi. Kwa mfano, wanawake wanauza maziwa, wanatengeneza pombe au kushiriki katika upatu au utaratibu wa kukopa na kukopesha. Wanawake wanatumia mapato yao kulipia mahitaji ya msingi katika kaya zao, chakula na matibabu. Huwaongezea uhuru wao wa kutoa maamuzi kuhusu kitu cha kununua bila ya kuwauliza waume zao. Hata hivyo, njia hizi si kwa wanawake wote. Baadhi ya wanawake hawana fedha za kutosha kushiriki katika

mipango ya mikopo na wanashindwa kufanya kazi kutokana na kuumwa, uzee au ulemavu.

Serikali imekuwa ikijaribu kukabili matatizo ya ubaguzi dhidi ya wanawake katika kutoa maamuzi. Kwa mfano, Sheria ya Serikali za Mitaa ya 1982 inahitaji angalau asilimia 25 ya wanawake katika vyombo vya utawala. Washiriki wanawake walikaribisha juhudi hizi. Hata hivyo, hata kama wanawake wamo katika vyombo vya Serikali, mara nyingi hawahimizwi kushiriki. Viongozi wanawake jasiri wameitwa "wakorofi" na wakati mwingine wanapuuzwa katika mikutano ijayo.

Baadhi ya wanawake wanaona vigumu sana kushiriki katika utaratibu wa kufanya maamuzi kwa sababu ya kiwango kidogo cha elimu, kukosa maarifa kuhusu haki zao, na aibu wanapotakiwa kuzungumza katika mikutano ya hadhara.

Unyanyasaji na utumiaji nguvu unaotokana na mila na desturi

Unyanyasaji na utumiaji nguvu dhidi ya wanawake husababisha wapoteze ustawi wa miili yao na uhuru kutenda. Kuna viwango vikubwa vya utumiaji nguvu wa majumbani, unyanyasaji wa ngono na ubakaji nchini Tanzania. Ukeketaji wanawake pia bado unaendelea. Wanawake wengi hawajiamini kutokana na unyanyasaji unaowazuia kushiriki katika jamii.

Katika kijiji cha Mwakizega (Wilaya ya Kigoma vijijini) wanawake walilalamika kuwa matukio mengi ya kupigwa wanawake yanachochewa na ulevi wa wanaume. Kuna shinikizo za kijamii zinazowalazimisha wanawake wabaki katika ndoa hata kama wananyanyaswa mara kwa mara na waume zao.

Utumiaji nguvu wa majumbani, au upigaji wake, ni miongoni mwa aina ya unyanyasaji wa wanawake inayowaathiri sana (angalia kisanduku). Baadhi ya wanawake walioshiriki utafiti wa TzPPA pia wameripoti ubakaji na aina nyingine za unyanyasaji. Unyanyasaji wa kijinsia ni tatizo kubwa maofisini pia, shule na katika jamii kubwa.

Baadhi ya washiriki walizungumzia aina mbaya zaidi za ukeketaji wa wanawake (FGM) kuwa si ubinadamu. Wanawake wanaambiwa ni desturi muhimu kwa uzazi na kuolewa. Wakati mwingine hufanyiwa wakiwa bado wasichana wadogo sana. Baadhi ya wanawake pia hufa wakati wa ukeketaji, na wengi wao wanapata maumivu makali na matatizo wakati wa kujifungua.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Wanawake wana uchaguzi mdogo wa kushughulikia wanaume wanyanyasaji, kwa hiyo wengi wao wanaishia kubaki katika ndoa zinazonyanyasa. Hata hivyo, washiriki wanawake wameeleza miitikio mingi wanayotumia kushughulikia unyanyasaji:

Kulalamika kwa ndugu na viongozi wa jamii	Mwanamke anayenyanyaswa nyumbani anaweza kulalamika kwa wazazi wa mume wake. Iwapo hii haileti mafanikio anaweza kulalamika kwa balozi wa nyumba kumi na baadaye kwa viongozi wa kijiji na jamii. Lakini kulalamika kwa viongozi wa jamii kunaweza kusumbua utaratibu wa umma, na wakati mwingine wanahitaji ada ili kusikiliza malalamiko ya wanawake.
Kumwacha mume mnyanyasaji	Wanawake vijana kutoka kaya tajiri wanaweza kurudi kwa wazazi wao na kurudisha mahari. Wanawake vijana wana nafasi kubwa ya kuolewa tena. Wanawake wakubwa kutoka kaya maskini hawana uchaguzi mwingi na mara nyingi wanabaki katika ndoa ili kuhakikisha maisha ya watoto wao.
Kwenda polisi	Wanawake huenda polisi kwa matukio machache sana. Mara nyingi wanasita kufungua mashtaka dhidi ya waume wao kwa sababu wanawategemea sana waume wao kwa maisha yao.

Sheria ya Kubaka na Unyanyasaji ya Mwaka 1998 inatarajiwa kusaidia kuwalinda wanawake wasinyanayswe, kuteswa na kukeketwa. Hata hivyo, wanawake wachache sana wanaelewa sheria hii na kujua namna ya kutumia mfumo wa sheria ili wapate haki zao. Aidha, taasisi mbalimbali hazijahimiza ipasavyo sheria hizi.

Masuala yanayoathiri walemavu

Walemavu wanakabiliwa na unyanyasaji, ubaguzi na kutelekezwa, na hivyo kuathiri vibaya ustawi wao. Wakati chanzo cha ulemavu ni hali ya mwili, ubaguzi kuhusu walemavu hutoka kwa jamii (angalia kisanduku).

Mara nyingi walemavu hukosa ajira. Kwa mfano, katika Kata ndogo ya Sokoni (Manispaa ya Ilala) mwanamke anasema *"Waajiri wala hawataki kutupa ajira kama vile za mapokezi na kupokea simu"*. Na ni vigumu kufanya kazi katika sekta isiyo rasmi. Mwanamke mmoja ameeleza kuwa, katika soko anakofanya kazi watu wakati mwingine wanakataa kulipa, na mara nyingi walimwambia *"We mlemavu! utanifanya nini?"*

> Watu wanalemazwa na jamii zao na si ulemavu wao. Wanakoseshwa uwezo na jamii na si vitu.
>
> Ulemavu ni aina ya kutengwa na kukandamizwa kijamii... Tunapozungumzia 'mtu kulemaa,' si kutokana na ulemavu wao, bali ni kutokana na namna watu wanavyofanya au kushindwa kuwafanyia.
>
> - Shirikisho la Walemavu Tanzania Vyama vya Wananchi

Mara nyingi watoto walemavu huchekwa, kunyanyaswa na kutengwa na michezo shuleni, ambayo mara nyingi huwafanya waacha shule. Na walimu wameshindwa au kutokuwa tayari kuwalinda watoto walemavu. Hata hivyo, hii inawazuia watoto kupata elimu, na hivyo kufanya maisha yao ya baadaye yawe magumu zaidi.

8.2. Mifumo ya Mila na Imani

Baadhi ya mila na imani vina athari mbaya kwa ustawi wa watu. Sura hii inaangalia sherehe, mahari, miiko, kaya kubwa, uchawi na ulevi. Desturi hizi zimetokea kuwa ndani ya maisha ya watu, kwa hiyo ni vigumu kwa watu kwenda kinyume nazo. Hata hivyo, baadhi ya watu wanaangalia mbadala wa mila na imani mbaya kulinda ustawi wao wenyewe.

Sherehe

Kimila kuna sherehe za wazi au maalumu kwa ajili ya matukio kama vile balehe (kuvunja ungo), harusi, mavuno na mazishi. Hizi huwahusisha wageni wengi, ni ghali na kutumia muda mwingi. Watu katika baadhi ya jamii wanatumia akiba zao na kuuza rasilimali ili kulipia gharama. Halafu baada ya sherehe, wanashindwa kugharimia mahitaji ya msingi ya kaya.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Baadhi ya watu wanapunguza gharama kwa kuzifanya ziwe za mara chache au za muda mfupi. Mkakati huu ni muhimu kwa kaya nyingi maskini. Hata hivyo baadhi ya washiriki wanaona kuwa kubadili sherehe hizi maana yake mila na desturi haziheshimiwi. Hii inaonyesha ugumu wa kuwianisha desturi za kitamaduni na ustawi wa watu.

Mahari

Mahari (hasa inapokuwa kubwa) husababisha familia kupoteza rasilimali za thamani. Kwa kaya zenye watoto wengi wa kiume, kulipa mahari mara nyingi kunaweza kusababisha hasara kubwa ya uchumi. Aidha, mahari kubwa mara nyingi huchangia kunyanyasika ndani ya nyumba. Iliarifiwa kuwa baadhi ya wanaume wanaona kuwa baada ya kulipa mahari, wako huru kudhibiti na kuwanyanyasa wake zao.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Vijana kutoka kaya maskini katika jamii zinazohitaji mahari kubwa mara nyingi huoa wanawake wa makabila tofauti yenye mahari ndogo. Uchaguzi mwingine ni kwamba mwanaume na mwanamke wanakubaliana kuishi pamoja na kuoana baadaye. Uchaguzi huu hufanya ndoa na familia kuwa rahisi kwa watu wengi.

Miiko

Ilibainika kuwa miiko mingi mibaya ya asili imekuwa ikitoweka na kwamba hivi sasa watu wanakutana na fikra mpya. Miiko inaweza kusababisha kupungua kwa ustawi wa mwili na kuwafanya watu wawe katika hatari ya kuwa maskini. Kwa mfano, wanawake wajawazito, kimila walikuwa hawaruhusiwi kula baadhi ya vyakula ambavyo wakati mwingine huwasababishia lishe duni kwa mama na mtoto. Hata hivyo, desturi hiyo imetoweka kutokana na kampeni za elimu zinazofanywa na wafanyakazi wa maendeleo ya jamii na kliniki za afya ya mama na mtoto. Lakini baadhi ya miiko ya zamani bado inatumika na kusababisha athari kubwa.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Serikali na vyama vya kiraia vimeshirikiana kupambana na miiko mibaya kwa njia ya kampeni za habari na elimu. Hata hivyo juhudi hizi zinahitaji msaada zaidi ili zifae.

Kaya Kubwa

Ukubwa wa kaya unaweza kuchangia umaskini, hasa wakati kuna mtafutaji mmoja anayetegemewa na watu wengi. Kaya kubwa zipo kwenye jamii nyingi. Washiriki wamesema kuwa kaya kubwa ni matokeo ya:

- Wanawake kuwa na watoto wengi;
- Ndoa ya wake wengi (mitala);
- Kaya zisizo rasmi za familia nyingi (nyumba ndogo au “Bloku B”); na
- Ukoo mkubwa.

Kuna baadhi ya manufaa ya kuwa na kaya kubwa kama vile kuwa na wanafamilia wengi katika kaya kwa nguvu kazi kubwa na uwezo wa kuwahudumia wagonjwa, walemavu, na wazee. Hata hivyo, kaya kubwa zenye watoto wengi wadogo zimo hatarini zaidi kupata umaskini.

Matatizo yanayozikabili kaya kubwa ni pamoja na:

- Kupungua kwa hali ya chakula, hasa kwa kaya zenye mtafutaji mmoja;
- Kukosekana kwa rasilimali za familia kutokana na kugharimia mahitaji ya kila siku ya familia kubwa; na
- Maendeleo ya watoto na ustawi wa baadaye vinaweza kuathirika – wazazi wenye watoto wengi wanaposhindwa kuwapa elimu inayofaa, chakula au mavazi watoto wanapokuwa wadogo.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Mbinu zinazotumika kukabili hali hii hutegemea sana idadi ya watafutaji na idadi ya wategemezi, lakini mara nyingi mwitikio ni pamoja na:

- Kupunguza idadi ya milo kwa siku;
- Kutumia ajira ya watoto; na
- Kutafuta njia mpya za kujitafutia riziki.

Wakati mwingine mzigo wa familia kubwa umechochea tabia mbaya. Wakati mwingine wanaume na akinababa wametoroka na kuwaacha wake zao peke yao na mzigo wa kutunza watoto wengi.

Kampeni za uzazi wa mpango na elimu dhidi ya kuwa na familia kubwa ni mbinu nyingine. Hata hivyo, mara nyingi mbinu hizi hazifai sana kwa sababu haziwezi kubadili tabia kama kuoa wake wengi (mitala), nyumba ndogo na kuzaa watoto nje ya ndoa. Aidha, watu wana majukumu ya kijamii ya kulea familia maskini.

Watoto wanapokua, wazazi wanatarajia kusaidiwa fedha, mahari au aina nyingine za misaada ili kuongezea kile kinachopatikana katika familia. Lakini siku hizi aina hii ya msaada haina uhakika kwa sababu watoto hawana rasilimali za kutosha.

Uchawi

Washiriki wa vituo vyote 30 vya utafiti wamesema kuwa uchawi umekuwa sehemu ya maisha ya watu. Imeonekana kwamba watu wanatumia uchawi kukabili matatizo mbalimbali yanayoelekea kuwatumbukiza katika umaskini.

Katika jamii nyingi, imani za uchawi zimeathiri utoaji maamuzi kuhusu masuala ya utawala wa eneo na umesababisha mgongano wa mamlaka. Watu wengine wameingia katika umaskini kwa kutumia muda wao mwingi, fedha na rasilimali nyingine kujaribu kutanzua matatizo yao kwa njia ya uchawi.

Shutuma za uchawi pia hutumika kuharibu uhusiano wa kijamii katika jamii kwa sababu zinasababisha shaka na chuki miongoni mwa watu. Watu ambao wametuhumiwa kwa uchawi wanajaribu kujisafisha kwa kuwashutumu watu wengine kuwa ni wachawi. Matokeo yake wanajamii hawako tayari kushirikiana pamoja kwa masuala muhimu.

Wakati mwingine, imani za uchawi zimesababisha watu kupata udhaifu wa mwili. Kwa mfano katika sehemu moja ya mkoa wa Morogoro, watu wanaamini kuwa watoto wenye malaria wamelogwa. Kwa hiyo, hirizi kutoka kwa waganga wa jadi hutumiwa kuzuia malaria, badala ya kutumia vyandarua.

Unyanyasaji, kukosa usalama na umaskini miongoni mwa wanawake na wazee ni matokeo mengine ya shutuma za uchawi. Katika kijiji kimoja cha Wilaya ya Muleba, shutuma za uchawi mara nyingi hutumika kwa sababu za uchoyo, kwa mfano kuwatishia au kuwaua ndugu wazee wanaodai kurithi mali.

Mbaya zaidi, kuua wazee wanaoshutumiwa uchawi ni kawaida katika jamii nyingi. Wanawake wazee (vikongwe) wamo hatarini zaidi kushutumiwa uchawi, na wengi wao wanaishia kukimbilia kuomba mitaani kwa sababu wanahofia usalama wao.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Mara nyingi ni vigumu sana kwa watu kujitetea dhidi ya shutuma za uchawi, kwa sababu ya kiwango kidogo cha elimu katika ngazi ya kaya na jamii. Mwitikio mkuu wanaotumia watu ni kukimbia nyumba zao na kujilinda na unyanyasaji na vitisho vya kifo. Mwitikio huo unapunguza tu kutokuwa salama na unyanyasaji na wakati mwingine kuwafanya watu wawe hatarini nyingine zaidi.

Kwa kuwa uchaguzi wa mwitikio wa watu ni mdogo, kuna haja kubwa ya juhudi za pamoja na mikakati ya kulaani imani za uchawi na desturi. Jamii za vijijini hazijafanikiwa kushughulikia suala hili wao wenyewe.

Unywaji wa Pombe

Unywaji wa pombe ni sehemu ya utamaduni wa sherehe nyingi na sehemu ya shughuli za burudani ya kila siku kwa watu wengi. Pombe inaponywewa kwa kiasi kikubwa, inawafanya watu wawe hatarini kuingia katika umaskini.

Kwanza, ulevi unahusiana na ugomvi wa nyumbani, kwa hiyo una athari mbaya kwa ustawi wa jumla wa kaya. Wanawake katika jamii nyingi amesema kuwa wanaume walevi wanarudi nyumbani usiku na kuwapiga wake zao bila sababu.

Pili, ulevi huathiri vibaya ustawi wa uchumi wa kaya. Hii inatokea wakati wakuu wa kaya wanapotumia mapato yao kununulia pombe badala ya kulisha familia zao. Katika kijiji kimoja, Wilaya ya Kigoma vijijini, baadhi ya wanawake wamesema kuwa waume walevi huishia kuzitelekeza familia zao.

Aidha ulevi pia unachangia katika umalaya na hivyo kuongeza hatari za maambukizo ya ngono na VVU/UKIMWI.

Mbinu za Kukabili Mishtuko na Mifadhaiko

Uchaguzi wa mwitikio waliotumia wanawake kushughulikia waume walevi ni kama ifuatavyo:

- Kuomba ushauri kutoka kwa ndugu wa karibu;
- Kuwaomba ndugu wa karibu au mamlaka kuzungumza na mume;
- Kuomba talaka au kutenganishwa;
- Kuomba fedha zao au rasilimali za uzalishaji kama vile ardhi kwa matumizi ya kaya; na
- Kuanza shughuli mpya za uzalishaji mali ili kuhudumia familia.

9. MAHITIMISHO

Kwa Muhtasari

- Sababu kuu za kuleta umaskini ni ukame, uharibifu wa mazingira, masharti mabaya ya biashara, rushwa, kodi zisizostahili, ukosefu wa usalama wa kimwili, VVU/UKIMWI, malaria na uzee. VVU/UKIMWI ni sababu moja ya kuleta umaskini mkubwa inayotishia watu binafsi na kaya nchini Tanzania hivi sasa.
- Baadhi ya "vikwazo" huathiri watu wa baadhi ya vikundi vya kijamii. Matokeo yake, watu hawa wanakabiliwa na mzigo mkubwa wa matatizo mengi yanayozuia kuwepo kwa mbinu za kutosha ili kukabili mishtuko na mifadhaiko.
- Ili kupata athari kubwa ya jumla kwa upunguzaji umaskini, Serikali na wabia wa maendeleo walishauriwa (i) kupunguza idadi, marudio, na kiwango cha sababu za umaskini zilizoainishwa katika Ripoti hii, wakati huohuo (ii) kuongeza uwezo wa vikundi mbalimbali vya jamii kukabiliana na sababu hizo kwa usalama na ubora.
- Ili kuimarisha mifumo ya usalama kwa jamii vijijini fedha zaidi zinahitajika (kununulia chakula na dawa) ikilinganishwa na muda (unaohitajika kupalilia shamba la mtu, kutayarisha chakula chao n.k.). Hii inasaidia kueleza kwa nini jamii maskini haziwezi kubuni mambo ya kuimarisha mifumo ya usalama wa maisha kwa haraka kiasi cha kutosha/kuzieneza vya kutosha ili kusimamia matatizo kama ya VVU/UKIMWI.
- Kupunguza athari ya sababu zinazoleta umaskini kutapunguza, lakini hakutatokomeza idadi ya kaya zinazozidi kutumbukizwa katika lindi la umaskini. Wale wasioweza kukwepa vipindi vigumu wanahitaji hatua za kulindwa za kijamii ili kusaidia waishi maisha ya heshima.
- Hatua za kulindwa za kijamii hazina budi kutoa kipaumbele cha utoaji wa msaada kwa watu katika vikundi vya kijamii ambavyo mara kwa mara vinalazimishwa kunyanyapaliwa na kutengwa na mitandao ya misaada.

9.1. UTANGULIZI

Mwanzoni mwa Ripoti hii, kielelezo cha ngazi kilitumika kueleza maana ya uathirikaji wakati watu wanapojitahidi kupanda wakitafuta ustawi. Wakati wa mchakato, sababu mbalimbali zimetishia kuwateremsha.

Sababu za msingi zinazoleta umaskini zilizoainishwa na washiriki wa utafiti wa TzPPA ziliwasilishwa katika makundi sita. Aidha ripoti inaonyesha watu binafsi, kaya na jamii zinazojitahidi kupinga au kukabili sababu hizi. Wakati baadhi ya watu wanaposhindwa kukabili sababu zinazoleta umaskini, wanazidi kuteremshwa chini kabisa ya ngazi ya ustawi isipokuwa kama watasaidiwa na mambo yanayowaokoa. Sura hii inahitimisha, kama ilivyoelezwa na washiriki wa utafiti, kuhusu hali ya utaratibu huu na kujibu maswali mahususi kuhusu uathirikaji yaliyotolewa na wadau muhimu katika utafiti huu TzPPA. Sehemu inayofuata ya sura hii inalenga kuonyesha matarajio kwa kuunganisha mahitimisho kwa juhudi zilizopo katika kupunguza maskini.

***Umaskini* ni kuhusu kwa kiasi gani mtu yuko katika kiwango cha chini kabisa cha ustawi sasa, ikilinganishwa na uathirikaji ni uwezekano mkubwa wa kutumbukia chini (au chini zaidi) yakiwango cha chuo wakati ujao.**

Hitimisho lake kuu ni kwamba mkabala wa pande mbili ni muhimu kukabili uathirikaji:

Mishtuko & mifadhaiko

1) ***Kupunguza idadi, marudio na kiwango cha sababu kuu za umaskini;***
2) ***Kuongeza uwezo wa watu katika vikundi mbalimbali vya jamii ili kukabiliana na mishtuko na mifadhaiko kwa usalama na vizuri.***

Mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko

9.2. SABABU ZINAZOLETA UMASKINI

Washiriki wa utafiti wa TzPPA walikuwa na wasiwasi sana na sababu zinazotishia ustawi wao wa mali, ambao unajumuisha fedha, ardhi, zana za uvuvi na/au nyumba. Hata hivyo, walikuwa na wasiwasi pia kuhusu afya yao, usalama wa kuishi, utu na uhuru wa kuchagua na kutenda. Vitisho vilivyoainishwa ni pamoja na ***mishtuko*** (kama ugonjwa wa ghafla) na ***mifadhaiko*** (kama vile kuharibika kidogo kidogo kwa maliasili). Njia mojawapo ya kutofautisha kati ya mishutuko na mifadhaiko ni kwamba ya kwanza inaharibu rasilimali na ustawi na ya pili huviondoa kidogo kidogo.

Si rahisi kuainisha ***kundi lililo muhimu zaidi*** la sababu zinazoleta umaskini kwa sababu athari ya mishtuko na mifadhaiko hutofautiana kutoka jamii moja na nyingine na kwa muda mrefu. Kwa mfano, watu wa kijiji cha Loborsoit (Wilaya ya Simanjiro) walisema kuwa vitisho vikubwa hivi sasa ni matokeo ya hali ya uchumi mkubwa; lakini wasiwasi wa mazingira ulikuwa muhimu zaidi miongo mingi iliyopita wakati walipokuwa wakihangaika namna ya kuishi na ukame wa muda mrefu. Kinyume chake, watu wa kijiji cha Ikombe (Wilaya ya Kyela) kwa sasa wanaona sababu za mazingira ni muhimu wakati utawala umesisitizwa katika Kata-ndogo ya Sokoni (Manispaa ya Kinondoni). Mifano hii mitatu ni ushahidi wa mtindo unaojitokeza kutokana na michango ya washiriki wa TzPPA ambapo sababu za ***utawala, uchumi mkubwa na mazingira zimekuwa na athari kubwa kwa ustawi wa jamii na ustahimilivu wa umaskini.***

Kama ilivyoonyeshwa katika kijitabu hiki, kuna mambo mengi yanayowaingiza watu katika lindi la umaskini. Kwa mujibu wa kilichoelezwa na washiriki wa utafiti wa TzPPA, s***ababu moja mbaya kabisa inayoleta umaskini katika kaya ni janga la VVU/UKIMWI.*** Kwa sababu unajumuisha matatizo ya ugonjwa wa muda mrefu na unyanyapazi na kutengwa na jamii, watu wanaoishi na ugonjwa na kushindwa kabisa kumudu maisha yao bila msaada kutoka kwa watu wengine. Kutokana na ukweli kwamba Ripoti ya Uchunguzi ya Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi inaonyesha kuzidi kushamiri, ni dhahiri kuwa haitakuwa rahisi kuondoa kabisa umaskini ***bila kwanza kuainisha, kukabili na kuzuia janga la VVU/UKIMWI.***

Mishtuko na mifadhaiko mingine mikuu iliyotajwa katika ripoti hii na washiriki wa utafiti ni pamoja na:

- **Ukame**
- **Uharibifu wa mazingira**
- **Masharti mabaya ya biashara**
- **Rushwa**
- **Kodi zisizofaa**
- **Kukosekana kwa usalama wa mali**
- **Malaria na magonjwa mengine**
- **Uzee**

9.3. MBINU ZA KUKABILI MISHTUKO NA MIFADHAIKO

Watoto, wanawake na wanaume katika mazingira yote wanapinga kutumbukizwa katika lindi la umaskini. Jinsi wanavyofanya hivyo, wanachagua kutoka katika hatua za kufaa. Baadhi ya uchaguzi wa ***mbinu za kukabili*** hali zilizopo, mara nyingi ni kudhamiria, kuwa mbunifu na kufaa daima. Kwa muhtasari watu wanajaribu:

- Kuzuia baadhi ya sababu za umaskini zisitokee;
- Kuziepusha nyingine;
- Kupunguza athari ya zile wasioweza kuzizuia au kuziepusha;
- Kuhimili matokeo; na
- Kurudia kupanda ngazi ya ustawi.

Hata hivyo baadhi ya mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko zinaweza kuchukuliwa na kuweza kuzuia athari zisitokee, kwa mfano kununua vyandarua vya kitanda ili kuzuia malaria. Aina hii ya hatua za kabla ya kutokea zinafaa, hata kama baadhi (kama vyandarua) hutoa kinga ya chini ya asilimia 100 lakini zinatoa mchango mkubwa na muhimu katika kupunguza uathirikaji.

Baadhi ya mishtuko na mifadhaiko haiwezi kuzuilika. Kwa hali hiyo, kama ilivyoonekana katika maelezo ya washiriki wa utafiti, watu wanazingatia ***upunguzaji kasi***, au njia za kupunguza athari za

mishtuko na mifadhaiko. Baadhi ya juhudi hizi hufanyika kabla ya kuanza kwa shida. Kwa mfano wafugaji huwa na mifugo ya aina mbalimbali na wakulima wanapanda mazao maalumu kumudu kaya zao wakati wa ukame. Aidha watu wanajaribu kujenga msingi wa rasilimali utakaowasaidia wakati wa uzee. Kinyume chake, mikakati mingine ya kupunguza kasi, kama vile matumizi ya mbolea za kemikali ili kufidia kupungua kwa rutuba ya udongo, hufanyika wakati mishtuko au mifadhaiko inapojitokeza.

- ***Hatua za kinga*** **zinalenga kuzuia mishtuko na mifadhaiko kutokea**
- ***Hatua za kupunguza kasi*** **zinalenga kupunguza athari zake**
- ***Mikakati ya kuhimili*** **inalenga kuyafanya matokeo yawe bora**

Ingawa shughuli hizi hazizuii shida isitokee, zinaweza kupunguza athari yake. Halafu watu lazima **wahimili** matokeo. Katika ngazi ya mtu binafsi na kaya, imesababisha watu kuuza rasilimali (zikiwemo rasilimali za uzalishaji kama vile ng'ombe na ardhi) kwa ajili ya kupata fedha na kuwaachisha watoto shule ili wachangie mapato ya familia. Katika ngazi ya jamii, imewafanya watu kukusanya pamoja rasilimali ili waweze kuwatunza mayatima wa VVU/UKIMWI. Mikakati hii ya kuhimili ya kabla/au baada huwasaidia watu kuishi ingawa pia huunda hatua muhimu katika kuwatayarisha kuepukana na sababu zinazoleta umaskini na kurudia juhudi zao za kupanda ngazi ya ustawi.

VIPENGELE VINAVYOZUIA

Sababu mbalimbali zinazoleta umaskini – kama vile ugonjwa na kushuka kwa uzalishaji wa udongo – zinahitaji mwitikio mbalimbali. Swali ni iwapo kweli watu wataweza kutekeleza mwitikio unaofaa usiohatarisha ustawi wao au wa wenzao. Mara nyingi jibu linategemea:

- Rasilimali wanazozimiliki
- Sababu zinazoelekea kuzuia au kukwaza matumizi yake

Umaskini katika hali zake zote – ni jambo gumu kushawishi kutokana na sababu zote kuweka vikwazo kuhusu namna watu wanavyoweza au kutoweza kumudu mishtuko na mifadhaiko.

Aina ya rasilimali watu wanazohitaji ili kukabili sababu zinazoleta umaskini ni pamoja na mtaji wa watu, jamii, siasa, asili, mali na fedha. Maskini wana rasilimali chache, na matokeo yake kuwa na uchaguzi na fursa chache kuliko wenye uwezo. Hii inaweza kuwalazimisha kuchagua mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko kuwa na manufaa ya muda mfupi, lakini wana uwezo wa kuleta matatizo mapya baadaye. Ndio maana wanakuwa hatarini zaidi kushuka kwa ustawi.

Hata hivyo, kuwa na rasilimali nyingi si lazima kuwa na uhakika wa kuweza kutumiwa kukabili sababu zinazoleta umaskini. Bila shaka watu wanafanya shughuli zao ndani ya mazingira magumu yanayokwaza kinachoweza kufanyika – wakati mwingine kwa gharama isiyotarajiwa – na kile walichonacho. Mazingira hayo yanaonyesha:

- Sifa bainifu za mtu, kaya na jamii
- Hali ya mazingira, uchumi, siasa na uchumi wa jamii

Kulingana na wanajamii waliochangia mawazo katika TzPPA, baadhi ya vipengele muhimu vinavyokwaza ni:

VIPENGELE VINAVYOKWAZA	MAELEZO
Kukata tamaa	Katika mishtuko na mifadhaiko iliyopo na pamoja na njia chache zilizopo za kumudu ustawi wao, baadhi ya watu wanakata tamaa na kuacha kujaribu. Itokeapo hali hii watu wanashindwa kutumia ipasavyo rasilimali walizonazo.
Rushwa, utawala mbaya wa umma na sera/sheria	Washiriki wa TzPPA mara nyingi wametaja rushwa, umbali mpaka kwenye vituo vya huduma za jamii, pamoja na sera/sheria zisizofaa kama vipengele muhimu vinavyokwaza. Kwa hiyo wanajamii walihitimisha kuwa: • Huduma za jamii zina jukumu kubwa katika juhudi zao na kuepuka kuwa umaskini zaidi. Ingawa mara nyingi wanakabiliwa na changamoto nyingi katika kupata rasilimali hizi, kikwazo kikubwa walichotaja ni rushwa.

	• Mambo kama utoro kazini kwa baadhi ya watu na watoa huduma za afya, upungufu wa dawa muhimu, ukosefu wa vifaa vya elimu, na mabomba mabovu kusababisha umbali halisi hadi kwenye huduma za jamii kuwa mkubwa kuliko mafanikio ya kitakwimu yaliyoonyeshwa katika Utafiti wa Bajeti ya Kaya wa 2000/1. • Sheria, sheria ndogo na kanuni mara nyingi huathiri uchaguzi wa mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko kwa watu mbalimbali. Mfano hai kabisa ni ule wa sheria zinazokataza moja kwa moja baadhi ya hatua za kuchukuliwa kwa baadhi ya adhabu za kutisha endapo zitakiukwa. Zinaweza kutokana na umuhimu kwa kuwa serikali inahitaji kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali za wote, kulinda afya ya umma, n.k. Hata hivyo, watu wanaona kuwa sheria nyingine zinahudumia maslahi ya wachache na kuchangia bila sababu kuongezeka kwa umaskini wao.
Mifumo ya kiuchumi na kijamii katika kumiliki, kuwa na mamlaka na upendeleo	Wakati mwingine mila na desturi huamua nani anamiliki rasilimali na namna zinavyoweza kutumika, nani anapata stadi za thamani, na nani anashawishi maamuzi muhimu. Kwa maneno mengine, mitindo ya uchumi wa jamii katika kumiliki, kuwa na mamlaka na upendeleo huzuia uchaguzi wa mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko kwa baadhi ya watu huku ikikuza ya wengine. Mitindo hii ipo katika kaya, jamii na ngazi za juu zaidi na husababisha baadhi ya uathirikaji unaohitaji msaada maalumu.

VIKUNDI VILIVYO HATARINI ZAIDI

Baadhi ya sababu zinazokwaza, kama zilivyotolewa wakati wa majadiliano na washiriki wa utafiti, kama vile matatizo ya uchumi-mkubwa, huathiri watu wote. Sababu nyingine kama vile mila na desturi zinazozuia nyendo za wanawake au ubaguzi dhidi ya walemavu, huathiri baadhi tu ya vikundi vya jamii ndani ya jamii fulani. Matokeo yake, watu waliyomo kwenye makundi haya ya jamii, hawana budi kushughulikia mzigo mkubwa zaidi wa matatizo yanayoonyesha namna (au hata iwapo) wataweza kushughulikia mishtuko na mifadhaiko.

Watu katika vikundi vya jamii wenye uhuru mdogo zaidi wa mwitikio ndio walio hatarini zaidi. Kwa hiyo, baadhi ya ***vikundi vya jamii vilivyo hatarini zaidi nchini Tanzania***, kama vilivyoainishwa na washiriki wa TzPPA ni pamoja na:

- Watoto (hasa mayatima)
- Wanawake wa umri wa kuzaa/wanawake wenye watoto wadogo
- Wajane
- Wazee
- Walemavu
- Watu wenye maradhi sugu
- Watu waliyomo kwenye kaya zilizoathiriwa na VVU/UKIMWI
- Mafukara

HATUA ZA KUJIOKOA

Kupunguza sababu za umaskini na kuongeza uchaguzi wa hatua za kujiokoa miongoni mwa watu kulingana na majadiliano ni njia bora zaidi ya kutanzua umaskini ulioenea Tanzania. Hata hivyo hatua hizo peke yake haziridhishi kwa sababu watu katika baadhi ya vikundi vya jamii – kama vile mayatima na wazee – wataendelea kuwa katika hatari kubwa ya kutumbukia katika kundi la ustawi hafifu. ***Watu hawa wanahitaji hatua za kujiokoa endelevu na zilizolengwa ili kuepuka kutumbukia katika ufukara wasioweza kuukwepa.***

Hatua za kujiokoa zinahakikisha kuwa mahitaji ya msingi ya kaya yanapatikana kunapotokea shida. Hatua za kujiokoa zisizo rasmi zilizotolewa na jamii, zimekuwa ni jambo la kawaida la maisha ya jamii ya Tanzania na bado ni muhimu mpaka sasa. Washiriki wa TzPPA wametoa mifano mingi:

- Katika ngazi ya kaya: watu wazima wanapeleka misaada kwa wazee; na
- Kwa kiwango cha familia pana: kaya zisizo na fedha hupewa kiasi kidogo cha kulipia matibabu, kodi ya maendeleo, n.k.; ndugu wanawapelekea chakula wale walioathiriwa na ukame, kina bibi na babu, shangazi na wajomba wanaoishi na mayatima.

Ingawa hatua hizi na nyingine za kujiokoa ni za kawaida watu wanasema kuwa watu wengi hivi sasa wanashindwa kuzingatia hatua hizi kuliko ilivyokuwa hapo nyuma. Hii inaweza kuwa ni kutokana na idadi kubwa ya watu wenye shida, bali pia kutokana na kudhoofika kwa ushirikiano wa mitandao ya kijamii. Hatua za kujiokoa za vijijini hushindwa wakati mishtuko, kama vile ukame mkubwa, unapoikumba mikoa yote. Kwa hali hiyo, hakuna atakayeweza kumsaidia jirani yake au familia zao. Katika baadhi ya jamii, VVU/UKIMWI hivi sasa unarudisha nyuma juhudi za watu za kusaidiana.

Kwa mfano, watoto mayatima katika kijiji cha Makiwa (Wilaya ya Makete) hawakuwepo na walikuwa wakihudumiwa na familia zao kwa urahisi. Hata hivyo sasa idadi yao imeongezeka sana, na matokeo yake, kuzidi uwezo wa zamani wa kudhibiti mambo. Katika kukabili hali hiyo, watu wameamua kushirikiana na kuanzisha kituo cha mayatima ambapo watoto watasaidiwa kwa michango kutoka kwenye kaya mbalimbali. Ingawa hii inatoa nafasi kwa kutunza watoto wengi, baadhi ya waathirika wa hali hiyo bado hawapati msaada wa kutosha kuepuka ufukara.

Hali hii ni ya kawaida kwa hatua za kujiokoa za jamii zinazohitaji msaada wa nje. Serikali na washiriki wengine wenyeji watoe kipaumbele cha kuzisaidia jamii zenye mfadhaiko ambazo hatua zao za kujiokoa haziwezi tena kumudu juhudi za sababu mbalimbali zinazoleta umaskini (k.v. maradhi ya mlipuko na majanga ya asili). Juhudi za pamoja za wadau hazina budi kulenga:

- Kutoa ***msaada kwa wakati unapotakiwa*** ili maisha ya watu yaokolewe na kumudu kupanda ngazi ya ustawi wao wenyewe;
- ***Kuimarisha, badala ya kupunguza juhudi za vijijini***; na
- Kushughulikia ***mahitaji mbalimbali*** ya watu katika kaya moja.

Pamoja na kusaidia na kuimarisha namna jamii zinavyoweza kusaidiana, juhudi za serikali na wengine hazina budi ***kuweka kipaumbele kwa misaada ya*** vikundi vya jamii ambavyo mara kwa mara hukabiliwa na unyanyapazi na kutengwa na msaada wa jamii. Hizi zinawajumuisha:

- Watu wenye ulemavu, na hasa watu wenye maradhi ya akili;
- Wazee na hasa wajane wazee;
- Kaya zilizoathiriwa na VVU/UKIMWI; na
- Kaya fukara.

9.4. Athari za Upunguzaji Umaskini

Ripoti inawakilisha mawazo au imani za washiriki wa utafiti kwamba kupunguza uathirikaji kwa kujaribu kudhibiti mishtuko na mifadhaiko na kuongeza uchaguzi wa hatua za kujiokoa kutapunguza idadi ya watu wanaokuwa maskini au wanaoingia kwenye lindi la umaskini. Kupunguza uathirikaji ni mkabala wa utendaji wa kupunguza umaskini. Mishtuko na mifadhaiko iliyoandikwa na watu tuliowasiliana nao katika tathmini hii inaweza kudhibitiwa kwa kuhakikisha kuwa serikali na wabia wa maendeleo wanaendeleza mkabala wenye:

- Kupunguza idadi, marudio na kiwango cha sababu kuu za umaskini; na
- Huongeza uwezo wa watu katika vikundi mbalimbali vya jamii kwa usalama zaidi wa maisha na kukabili ipasavyo mishtuko na mifadhaiko.

KUPUNGUZA MISHTUKO NA MIFADHAIKO: KUKABILI SABABU ZINAZOLETA UMASKINI

Baadhi ya sababu zinazoleta umaskini zinaweza kukabiliwa vizuri kwa kutekeleza mipango iliyolengwa. Kwa mfano, kinga na vyakula vya kuongezea virutubisho vinaweza kuzuia maradhi yanayotishia maisha ya watoto wadogo.

Washiriki wa utafiti pia walikuwa na wazo kwamba kuanzisha sera za kusaidia maskini na kuhakikisha kuwa zinafanya kazi ipasavyo kunaweza kusaidia pia mishtuko na mifadhaiko mingine. Sheria ya Ardhi ya 1999 inatambua haki za mjane kumiliki raslimali za msingi za kaya. Utekelezaji wake unaweza kuzuia kundi hili la walio hatarini kuathirika katika jamii ili lisipoteze rasilimali wanayotegemea kuendeshea maisha. Aidha Serikali imetunga sera zinazokataza uvuvi usio endelevu na kuhakikisha usafi wa msingi wa kaya. Iwapo zitahimizwa, sheria hizi zinaweza kulinda rasilimali za asili za Tanzania kwa vizazi vijavyo na kulinda afya ya jamii.

Sera na mipango kama hii haina budi kuendelea na kuimarishwa kwa kuwa inapunguza idadi, marudio na kiwango cha sababu zinazoleta umaskini ambazo wadau wengine hawana uwezo wala mamlaka ya kushughulikia.

Sababu za msingi za baadhi ya vyanzo muhimu vya umaskini, kama vile masharti mabaya ya biashara kwa wakulima wadogo na mabadiliko ya hali ya hewa, yanakwenda nje ya mipaka ya Tanzania na yanaweza kushughulikiwa tu na taasisi zenye ujuzi na rasilimali za kutosha kufanya kazi kitaifa na kimataifa. Pamoja na jukumu la kusaidia na kuimarisha juhudi za vijijini, watu wengi wamesema kuwa serikali na wabia wake wanalazimika kutanzua matatizo wasiyoweza. Kwa hiyo, kwa mfano, washiriki wa TzPPA wamesema Serikali ina jukumu la kufanya marekebisho ya uchumi na masoko yanayowahudumia maskini kuliko kuongeza umaskini wao.

KUIMARISHA UCHAGUZI WA MBINU ZA KUKABILI MISHTUKO NA MIFADHAIKO

Baadhi ya sababu za umaskini, zikiwemo rehema ya Mungu na athari za mwili za uzee, haziwezi kuzuiwa. Kwa hiyo, ni muhimu kuimarisha uchaguzi wa mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko wa aina mbalimbali na zinazofaa uliyopo kwa vikundi mbalimbali vya jamii. Kwa watu wa vijijini ni muhimu sana wakati wa msimu wa mvua wakati hawana mambo mengi ya kuchagua na huenda wakakubali maamuzi yatakayowalazimisha kutumbukia katika mitego ya umaskini.

Hatua mbalimbali zimekwishachukuliwa ili kuepuka matokeo haya kwa kuanza kupanda mazao yanayostahamili ukame pamoja na kufanya kazi kwa malipo ya chakula na mipango mingine ya ajira nyakati za matatizo. Ingawa zinasaidia, hatua kama hizi, hatimaye haziwezi kuhimili ukubwa wa mahitaji ya watu. Kwa hiyo ni muhimu pia:

- Kupanga vipaumbele vya mipango inayoimarisha mtaji wa watu; na
- Kupunguza njia ambazo zinafanya mazingira, maamuzi ya uchumi mkubwa, utawala, na mila na desturi kuzuia uwezo wa watu kulinda ustawi wao na wa wategemezi wao.

HATUA ZA KUJIOKOA, ULINZI WA JAMII

Ingawa hupunguza mishtuko na mifadhaiko na ongezeko la uchaguzi wa hatua za kujiokoa kutakuwa na athari muhimu kwa kupunguza umaskini uliokithiri, peke yake haitaridhisha kwa sababu watu katika baadhi ya vikundi vya jamii watabaki:

- Kuwa hatarini zaidi kutokana na umri, ukosefu wa uhusiano wa kijamii ulio muhimu (km. wazazi au mwenza wa ndoa), afya au imani za utamaduni zinazoathiri uhuru wao wa kuchagua na kutenda; na
- Kutelekezwa na kaya na jamii zao kutokana na ubaguzi (km. utengaji wa jamii unaowakabili wanaume na wanawake wengi walemavu).

Watu hawa wanahitaji hatua za kijamii zilizolengwa, endelevu na zilizolindwa ili kuepuka ufukara. Kwa hiyo, ***mwitikio wa Serikali kwa uathirikaji hauna budi kuwa wa sehemu mbili. Kwanza haina budi kulenga katika kupunguza uathirikaji na ya pili ni kuwahakikishia watu kupata mahitaji muhimu hata kama wameathiriwa sana na mishtuko au mifadhaiko.***

Hatua za ulinzi wa jamii hazina budi kutoa mahitaji ya msingi ya watu kwa wakati ili kuzuia wasiuze rasilimali za uzalishaji.

Kwa kutoa kipaumbele kwa mipango inayoimarisha mtaji wa watu na sera zinazolinda haki na rasilimali za wote, Serikali itajenga ***mazingira yanayowezesha*** ambapo wadau wengine hupewa uwezo wa kutoa mchango wao kushughulikia uathirikaji. Kama ilivyoelezwa katika kitabu chote, Vikundi vya Kijamii (VVK), mitandao ya kijamii isiyo rasmi, kaya na watu binafsi tayari wanashughulikia kufanikisha hilo. Hata hivyo, washiriki wa utafiti wamekuwa na wazo kwamba Serikali haina budi: (i) kubuni fursa mpya zinazowawezesha watu kuchukua hatua zinazofaa; (ii) kuhakikisha kuwa watu wanaweza kufanya "uchaguzi mzuri" (kama vile kuwaacha watoto wasome, kuwekeza katika kuongeza uzalishaji, kutumia kondomu, n.k.) wanapokabiliwa na mishtuko na mifadhaiko inayoweza kuwaletea umaskini.

Kwa muhtasari, jukumu la serikali, kwa mujibu wa washiriki wa utafiti, ni pamoja na:

- Kuainisha na kufanya mambo muhimu ambayo wadau wengine hawawezi kuyafanya;
- Kuhimiza na kuwawezesha wengine kufanya wanachoweza kufanya; na
- Kuwawezesha na kuwasaidia wafanye hivyo.

Ujumbe muhimu kutoka kwa washiriki wa utafiti wa TzPPA na kutoka katika taarifa hii ni kwamba **hatua zote** kuanzia ngazi ya kaya, jamii, taifa na kimataifa zina matokeo ya moja kwa moja kwa uathirikaji. Wakati mwingine uathirikaji unapungua na sehemu nyingine unaongezeka. Majadiliano ya washiriki wa utafiti yaliyomo katika ripoti hii yameturuhusu kujifunza mambo mengi kuhusu njia na namna ilivyotokea. Kwa hiyo sasa ni muhimu kuchukua msimamo wetu wa sasa wa sababu na matokeo ya uathirikaji, kuendeleza zaidi na kuhakikisha kuwa yanawianishwa katika hatua zote za umma za kusaidia kupunguza umaskini. Ripoti hii ni mwanzo tu. Kadiri sera na mipango vinavyotungwa, itakuwa muhimu kuchukua hatua za makusudi za mara kwa mara za kutafuta maoni ya vikundi tofauti vya jamii na kutoa maamuzi yanayoheshimu mahitaji yao mbalimbali na mazingira.



FAHARASA: Maana za maneno yaliyotumika katika kitabu hiki

hamasisha	Kuunga mkono hadharani au kupendekeza juhudi fulani au sera.
hatua za hifadhi ya jamii	Hatua za hifadhi ya jamii huhakikisha kuwa mahitaji ya kaya yanatimizwa wakati shida inapotokea na kaya haziwezi kujikimu zenyewe (angalia pia hatua za kuokoa).
hatua za kuokoa	Hatua zinazomlinda maskini na aliye hatarini. Zinaweza kuhusisha miradi ya ujenzi, mafao ya wasio na ajira, hatua za uhakika wa chakula, n.k. Kimila hatua za kuokoa zilikuwa zikitolewa na familia na jamii.
hazina ya serikali	Inahusiana na mapato ya serikali na hasa kodi na matumizi.
kinga	Dawa au hatua inayochukuliwa kuzuia ugonjwa usitokee.
kipengele	Kipengele ni moja ya mambo yanayoathiri uamuzi au jambo linalotokea.
kitegauchumi	Kama unawekeza fedha au kufanya uwekezaji, unatumia fedha zako (au rasilimali nyingine) kwa njia unayodhani kuwa itaongeza thamani yake/ kuingiza faida.
kupiga kampeni	Kufanyakazi kwa mpango na kwa ufanisi ili kutimiza lengo maalumu.
maadili	Mawazo kuhusu kilichosawa na kisicho sawa.
maendeleo endelevu	"Maendeleo yanayokidhi mahitaji ya sasa bila ya kuathiri uwezo wa kizazi kijacho kukidhi mahitaji yao." - Azimio la Rio la mwaka 1992 kuhusu Mazingira na Maendeleo.
mambo yanayosababisha umaskini	Mambo makuu sita yanayoleta umaskini ni mazingira, sera za uchumi mkubwa, utawala bora, hali ya afya, mzunguko wa maisha na hali ya uzee, na imani na mila na desturi.
matunzo kabla ya kujifungua	Matunzo anayopewa mwanamke anapokuwa mjamzito na kabla ya kujifungua.
matunzo ya uzazi	Matunzo anayopewa mwanamke wakati wa kujifungua.
mbinu za kukabili mishtuko na mifadhaiko	Watu wana uchaguzi wa aina tatu wa hatua za kujiokoa ili kukabili mishtuko na mifadhaiko. Wanaweza kujaribu kuona ikija na kuchukua hatua ya kujikinga (KINGA); wanaweza kujaribu kadiri wawezavyo kushughulikia hali mara zinapotokea (KUPUNGUZA KASI); na wanaweza kujaribu kadri wawezavyo kuhimili hali hizo baada ya kufanya uharibifu (KUHIMILI).
mdau	Mtu mwenye maslahi au kuhusika na jambo fulani.
mifadhaiko	Sababu za umaskini za hatua kwa hatua na zinazotabirika. Zinaweza kuwa za jumla na kumwathiri kila mtu (km. mmomonyoko wa udongo) au mahususi na huathiri watu binafsi (km. kuzeeka).
mishtuko	Sababu za kuleta umaskini za ghafla na zisizotabirika. Zinaweza kuwa za kawaida na kumwathiri kila mtu (km. tetemeko la ardhi) au mahususi na huathiri watu binafsi (km. ajali ya gari).
miundombinu	Majengo na vitu vya msingi vya uendeshaji vinavyohitajiwa kuendeshea shughuli za nchi kwa mfano majengo, barabara na nguvu za umeme.
mkakati	Ni mpango wa ngazi ya juu kwa kufikia lengo fulani.
mtaji	Rasilimali zinazotumika kuzalisha bidhaa au huduma. Rasilimali zinaweza kumilikiwa na wazalishaji (km. viwanda na mashine) watumiaji (km. nyumba) au jamii (km. majengo ya umma na barabara). Aina za mtaji ni pamoja na fedha, watu, maliasili, vitu, siasa na jamii.
rasilimali	Kinachomilikiwa na mtu binafsi, kaya, jamii au taifa kama vitu vilivyopo kwa matumizi yao, kwa mfano ardhi, fedha, watu wenye miili yenye nguvu.
rasilimali	Rasilimali za mtu ni vitu vyote anavyomiliki pamoja na sifa, stadi na uhusiano alionao na wengine. Rasilimali iliyo wazi zaidi ni fedha (mtaji wa fedha) lakini pia kuna miliki zingine muhimu zinazojumuisha mtaji wa asili, siasa, watu, vitu na jamii.
sababu za umaskini	Mishtuko na mifadhaiko inayowafanya watu binafsi, kaya au jamii kushuka chini ya ngazi ya ustawi.

shirika la umma	Muundo wa taasisi ambayo inajitegemea lakini ina uhusiano wa karibu na serikali.
suhula	Mpango unaowezesha/kitu au jengo au vifaa vinavyotolewa kwa madhumuni maalumu.
takwimu	Hoja zinazowasilishwa kwa tarakimu na kupatikana kwa kukusanya na kuchambua taarifa.
uathirikaji	Mtu, kaya au jamii inakuwa hatarini iwapo wanaelekea kuwa maskini zaidi kesho kuliko walivyo leo.
uchumi	Uchumi wa nchi au eneo ni mfumo unaotumia kuendeshea na kusimamia fedha, viwanda, na biashara, au utajiri iliyonao kutokana na biashara na viwanda.
uchumi mkubwa	Inahusika na mifumo ya uchumi ya nchi au vikundi vya nchi, kuliko ya makampuni au viwanda.
umaskini usio wa kipato	Iwapo una fedha kidogo lakini unakosa baadhi ya vitu vingine vya ustawi.
umaskini wa kipato	Wakati unapoishi chini ya dola moja kwa siku. Mara nyingi hupimwa kwa kuzingatia chakula na kiwango cha mahitaji ya msingi ya umaskini.
unyanyapazi	Iwapo mtu amenyanyapaliwa anaonekana kama mtu asiyekubalika au mtu wa aibu. Ama wanadhalilishwa na kunyanyaswa au kutelekezwa na kutengwa kijamii.
upungufu wa akili na mwili	Ugonjwa wa akili unaosababisha akili kushindwa kufanyakazi, mabadiliko ya tabia na kushindwa kufikiri vizuri.
upunguzwaji kazini	Wakati shirika linapoachisha kazi wafanyakazi ili kupunguza gharama.
ustawi	Unakuwa na ustawi iwapo huathiriwi na sababu ziletazo umaskini. Hapa hujumuisha vifaa, ustawi wa mwili na jamii na usalama na uhuru wa kujichagulia na kutenda.
vipengele vinavyokwaza	Vitu vinavyowazuia watu wasitumie rasilimali ipasavyo. Hali zinazosababisha umaskini ni vipengele vikuu vinavyokwaza na vinaweza kuwa vya jumla au maalumu kwa namna vinavyofanya kazi.

RAMANI YA TANZANIA BARA INAYOONYESHA SEHEMU AMBAMO UTAFITI WA TzPPA ULIFANYIKA



SHUKRANI

Ripoti hii inatoa muhtasari wa lugha nyepesi kwa Tathmini Shirikishi ya Umaskini Tanzania (TzPPA) iliyofanyika mwaka 2002/2003. Taasisi na watu mbalimbali katika utafiti wamebainishwa katika ripoti kamili. Hatuna budi kuwashukuru washiriki hao wote kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Tunatoa shukrani kwa watu wote walioshiriki kikamilifu katika kuandaa mwongozo huu wa lugha nyepesi kwa TzPPA. Shukrani za pekee zinatolewa kwa Kamati ya Utafiti na Uchambuzi (KUU) ambayo wajumbe wake walisaidia sana shughuli ya kuhariri ripoti hii.

Aidha tunatoa shukrani za pekee kwa shirika la Hakikazi Catalyst kwa kuwezesha utayarishaji wa mwongozo huu na Deo Simba aliyeshughulikia uhariri wa kina kutokana na mawazo mbalimbali ya KUU.

Arthur Mwakapugi
Mwenyekiti – Kamati ya Utafiti na Uchambuzi
Oktoba 2004

Mchoraji wa Vikaragosi:
Ally Masoud

Usanifu na Uchapaji:
Colour Print (T) Ltd.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

Idara ya Kuondoa Umaskini
Ofisi ya Makamu wa Rais
S.L.P. 5380
Dar es Salaam
Simu: 022-2113857
Tovuti: www.povertymonitoring.go.tz

Research on Poverty Alleviation (REPOA)
157 Mgombani Street, Regent Estate
P.O. Box 33223
Dar es Salaam
Simu: 022-2700083 / 2772556
Barua pepe: repoa@repoa.or.tz
Tovuti: www.repoa-or.tz